JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

WIZARA YA HABARI, UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO

# MKAKATI WA TAIFA WA KUKABILIANA NA MMOMONYOKO WA MAADILI

## 2026/27 - 2036/37

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

WIZARA YA HABARI, UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO

# MKAKATI WA TAIFA WA KUKABILIANA NA MMOMONYOKO WA MAADILI

2026/27 - 2036/37

# YALIYOMO

YALIYOMO........................................................................ ii
UJUMBE WA RAIS WA JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA ....................vii
UJUMBE WA WAZIRI ........................................................................ viii
DIBAJI YA KATIBU MKUU........................................................................x
SHUKRANI ........................................................................xi
VIFUPISHO ........................................................................xiii
SURA YA KWANZA........................................................................1
1 UTANGULIZI ........................................................................1
1.1 DHANA ZA MSINGI........................................................................2
1.1.1 Maadili........................................................................ 2
1.1.2 Maadili ya Mtanzania ........................................................................3
1.1.3 Mila na Desturi ........................................................................3
1.1.4 Urithishaji na Usimamizi Maadili ........................................................................3
1.2 MMOMONYOKO WA MAADILI ........................................................................4
1.3 HISTORIA YA MMOMONYOKO WA MAADILI........................................................................4
1.4 SERA, SHERIA, KANUNI NA MIONGOZO INAYOSIMAMIA MAADILI.........6
1.5 UHALALI WA KUANDAA MKAKATI ........................................................................10
1.6 METHODOLOJIA ZILIZOTUMIKA KUANDAA MKAKATI............................12
1.6.1 Mapitio ya Nyaraka........................................................................12
1.6.2 Mahojiano ya Ana kwa Ana ........................................................................12
1.6.3 Ujazaji wa Dodoso........................................................................13
1.6.4 Vikao vya Wadau........................................................................13
1.6.5 Kuangalia Hali Halisi........................................................................13
1.6.6 Majadiliano ya Makundi........................................................................13
1.7 NUKUU NA MITIZAMO YA VIONGOZI KUHUSU MAADILI NA UZALENDO ........................................................................14
1.8 MATUMIZI YA SEMI ZA KISWAHILI KATIKA KUJENGA MAADILI KWA WANAJAMII........................................................................17
1.8.1 Uchambuzi wa Methali Kimaadili ........................................................................18
1.9 MSINGI WA KINADHARIA WA MKAKATI........................................................................20
1.9.1 Nadharia ya Mabadiliko ya Kijamii na Kimfumo (Social–Ecological Theory of Change-SETC)........................................21
1.9.2 Nadharia ya Mabadiliko ya Kijamii Yanayojengwa juu ya Maadili (Value-Based Social Change Theory - VBCT) ........................................21

1.9.3 Muunganiko wa Nadharia Mbili Katika Mkakati ..... 22
1.9.4 Mfumo wa Dhana wa Mkakati ..... 23

**SURA YA PILI**

**HALI HALISI YA MAADILI ILIVYO NCHINI ..... 24**

2 UTANGULIZI ..... 24
2.1 KUPOROMOKA KWA MAADILI NCHINI ..... 25
2. 1.1 Sababu za Kuporomoka kwa Maadili Nchini ..... 25
2.2 VIASHIRIA VYA KUPOROMOKA KWA MAADILI NCHINI ..... 26
2.2.1 Mapenzi ya Jinsia moja ..... 26
2.2.2 Matumizi ya dawa za kulevya na pombe kupita kiasi ..... 27
2.2.3 Mimba za Utotoni na Kutupa Watoto Wachanga ..... 27
2.2.4 Rushwa, Ufisadi, na Uhujumu Uchumi ..... 28
2.2.5 Ujambazi, Wizi, na Uporaji wa Mali ..... 28
2.2.6 Ukatili wa Kijinsia: Ubakaji, Ulawiti na Ukeketaji ..... 28
2.2.7 Mauaji ya vikongwe na watu wenye ulemavu wa ngozi ..... 29
2.2.8 Uvaaji Usio na Stara ..... 29
2.2.9 Uongo na Udanganyifu ..... 29
2.2.10 Wizi na Uharibifu wa Miundombinu ya Maendeleo ..... 30
2.2.11 Makosa ya Usalama Barabarani ..... 30
2.2.12 Ukahaba na Madanguro ..... 30
2.2.13 Usafirishaji haramu wa binadamu ..... 31
2.3 ATHARI ZA KUPOROMOKA KWA MAADILI NCHINI ..... 31
2.3.1 Athari za Kijamii ..... 31
2.3.2 Athari za Kiutamaduni ..... 33
2.3.3 Athari za Kiuchumi ..... 33
2.3.4 Athari Kisiasa ..... 34
2.3.5 Athari za Kiteknolojia ..... 34
2.4 JITIHADA ZILIZOFANYIKA KATIKA KUKABILIANA NA MMOMONYOKO WA MAADILI NCHINI ..... 35
2.4.1 Mwongozo wa Maadili na Utamaduni wa Mtanzania ..... 35
2.4.2 Mwongozo wa Uzingatiaji wa Maadili katika Kazi za Sanaa ..... 35
2.4.3 Kuendesha Makongamano ya Kukabiliana na Mmomonyoko wa Maadili ..... 36
2.4.4 Kutoa Elimu ya Maadili na Utamaduni Kupitia Vyombo vya Habari ..... 36
2.4.5 Kujumuishwa kwa Somo la Maadili katika Mitaala Mipya ya Kufundishia kwa Shule za Msingi ..... 36

2.4.6 Programu ya Malezi kwa Vijana....37
2.4.7 Urithishaji wa Elimu ya Maadili, Mila na Desturi Kutoka kwa Wazee....37
2.4.8 Kampeni za Kijamii zinazolenga Kuhamasisha Ushiriki wa Jamii....37
2.4.9 Kuwajengea uwezo Wataalamu wa Sekta Mbalimbali....37
2.4.10 Uanzishaji wa vituo vya kulelea watoto mchana na huduma ya malezi mbadala....38
2.5 CHANGAMOTO ZINAZOKABILI JITIHADA ZA KUKABILIANA NA MMOMONYOKO WA MAADILI....38

**SURA YA TATU**

**MALENGO YA MKAKATI....41**

3 UTANGULIZI....41
3.1 LENGO KUU....41
3.2 MALENGO MAHSUSI....42
3.3 AFUA ZA KIMKAKATI....43
3.4 MIKAKATI YA UTEKELEZAJI KWA KILA LENGO MAHUSUSI....47

**SURA YA NNE**

**MAJUKUMU YA WADAU....56**

4 UTANGULIZI....56
4.1 MGAWANYO WA MAJUKUMU YA WIZARA NA WADAU MBALIMBALI KATIKA UTEKELEZAJI WA MKAKATI....56

**SURA YA TANO**

**URATIBU....64**

5 UTANGULIZI....64
5.1 MUUNDO WA URATIBU WA UTEKELEZAJI WA MKAKATI....64
5.2 UCHAMBUZI WA MAJUKUMU YA VIKAO VYA KITAIFA....65
5.2.1 Kamati ya Mawaziri wa Wizara Wadau wa Mkakati....65
5.2.2 Kamati Elekezi ya Taifa ya Utekelezaji wa Mkakati....66
5.2.3 Kamati Tendaji ya Taifa ya Uratibu wa Mkakati....67
5.2.4 Sekretarieti ya Taifa ya Uratibu wa Mkakati....68
5.2.5 Uratibu katika ngazi Ya Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa....70

**SURA YA SITA**

**MWONGOZO WA MAWASILIANO....79**

6 UTANGULIZI....79
6.1 MASUALA MUHIMU KATIKA MWONGOZO WA MAWASILIANO....79
6.2 LENGO KUU NA MALENGO MAHSUSI KATIKA MWONGOZO WA MAWASILIANO....79
6.2.1 Lengo Kuu....79
6.2.2 Malengo Mahsusi....80

6.3 WAHUSIKA WA MWONGOZO WA MAWASILIANO ....80
6.3.1 Wasimamizi wa Mwongozo wa Mawasiliano ....80
6.3.2 Walengwa wa Mwongozo wa Mawasiliano ....80
6.4 MBINU NA NJIA ZA MAWASILIANO ....81
6.4.1 Mbinu za mawasiliano ....81
6.4.1 Njia za mawasiliano ....81
**SURA YA SABA**
**UFUATILIAJI, TATHMINI NA KUJIFUNZA ....83**
7 UTANGULIZI ....83
7.1 MADHUMUNI YA UFUATILIAJI NA TATHMINI ....83
7.2 MISINGI YA KUZINGATIA KATIKA UFUATILIAJI NA TATHMINI ....84
7.3 VIASHIRIA VYA UTENDAJI ....84
7.4 UKUSANYAJI NA UCHAMBUZI WA TAKWIMU ....84
7.5 TAARIFA YA UFUATILIAJI NA TATHIMINI ....85
7.5.1 Aina za Taarifa za Ufuatiliaji na Tathmini ....85
7.5.2 Uwasilishwaji wa Taarifa ....85
**SURA YA NANE**
**MAPENDEKEZO YA KISERA YA KISEKTA KATIKA KUKABILIANA NA MMOMONYOKO WA MAADILI ....91**
8 UTANGULIZI ....91
8.1 SEKTA YA ELIMU ....91
8.2 SEKTA YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA ....91
8.3 SEKTA YA SHERIA NA HAKI JINAI ....92
8.4 SEKTA YA AFYA ....92
8.5 SEKTA YA HABARI NA MAWASILIANO ....92
8.6 SEKTA ZA FEDHA, UCHUMI, BIASHARA NA MANUNUZI YA UMMA ....93
8.7 SEKTA YA VIJANA ....93
8.8 SEKTA YA UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO ....94
8.9 SEKTA YA MALIASILI NA UTALII ....94
8.10 SEKTA YA TEKNOLOJIA YA HABARI NA MAWASILIANO (TEHAMA) ....94
8.11 SEKTA YA MIUNDOMBINU NA USAFIRISHAJI ....95
8.12 SEKTA YA SERIKALI ZA MITAA NA JAMII ....95
8.13 SEKTA YA ARDHI NA MAZINGIRA ....95
8.14 SEKTA YA DINI NA ASASI ZA KIRAIA ....96
8.15 HITIMISHO ....96
**MAREJELEO ....97**

UJUMBE WA HAYATI, MWALIMU JULIUS KAMBARAGE
NYERERE RAIS WA KWANZA WA JAMHURI YA
MUUNGANO WA TANZANIA ........ 98

UJUMBE WA WIZARA YA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA,
WANAWAKE NA MAKUNDI MAALUM ........ 100



*''Tunapokaa tu kwenye majukwaa tukilalamika, mmomonyoko wa maadili,mmomonyoko wa maadili, hakuna anayechukua hatua, HATUTAFIKA, tutafikia kule kule kwenye Taifa ambalo tunaliimba kwa kusema  Taifa litakuwaje? Niombe twendeni tukachukue hatua''*

*"Tuamue kujenga jamii ya watu mahiri, makini, waadilifu na wenye maadili"*

**Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan**
**RAIS WA JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA.**



# " UJUMBE WA WAZIRI "

Msingi mkuu wa kuwapo kwa Mkakati huu wa Taifa wa Kukabiliana na Mmomonyoko wa Maadili ni kuikumbusha jamii kuwa Tanzania ni Taifa linaloenzi maadili, miiko, na misingi iliyoliasisiwa na wazee wetu. Jitihada hizi zina mizizi ya kihistoria; Baba wa Taifa, Hayati Mwalimu Julius K. Nyerere, alianzisha miongozo ya maadili ndani ya TANU (1971) na CCM (1981) akiamini kuwa, bila mwongozo madhubuti wa tunu za Mtanzania, ni vigumu kuongoza Taifa lililotoka katika misukosuko ya ukoloni.

Ni imani yangu kuwa, Mkakati huu utatoa fursa adhimu kwa Watanzania kutambua wajibu wao kwa jamii na Serikali. Hali kadhalika, Serikali inatambua wajibu wake wa kuhakikisha mkakati huu unakuwa nuru ya Tanzania, ukiangaza na kupambana na giza la mmomonyoko wa maadili unaoukabili ulimwengu wa sasa uliotawaliwa na kasi ya mabadiliko ya kidijiti na akili unde.

Tutahakikisha kila kundi katika jamii linawajibika kurithisha, kulinda na kuenzi maadili yetu, tukiongozwa na msingi imara uliyowekwa na waasisi wa taifa letu pamoja na Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Kupitia uzalendo wao, wamekuwa kinara wa kuhimiza maadili katika sekta zote, ikiwemo kuyashirikisha makundi mbalimbaliili kuimarisha ushirikiano kati ya wananchi na Serikali katika kulinda tunu za Taifa.

Kwa msingi huo, Wizara itahakikisha Mkakati huu uliopata baraka za Mheshimiwa Rais unazaa matunda, na kuchochea ustawi wa nchi kijamii. kiutamaduni na kiuchumi tukitambua kuwa maadili na utamaduni ndio utambulisho wa nchi yetu. Nitumie fursa hii kuwasihi wadau wote kutekeleza majukumu yao kama ilivyobainishwa katika mkakati kwa ufanisi kwa maslahi ya Taifa letu teule la Tanzania.

**Mhe. Paul Christian Makonda (Mb)**
**WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO**

# DIBAJI YA KATIBU MKUU



Sera ya Utamaduni ya mwaka 1997 inaipa mamlaka Wizara yenye dhamana ya utamaduni kusimamia, kulinda, na kuendeleza urithi wetu wa kitaifa. Aidha, sera hiyo inasisitiza kuwa hili ni jukumu la jamii nzima. Vile vile, inatoa fursa na wajibu kwa asasi mbalimbali, zikiwamo za kijamii na kimila, kuendeleza maadili, elimu, na mafunzo kuhusu utamaduni wa Mtanzania. Halikadhalika, sera hii inashuka hadi ngazi ya familia kwa kuwahimiza wazazi kuenzi mila, desturi, na misingi ya malezi bora.

Katika kutekeleza jukumu hili la msingi, Wizara imeandaa Mwongozo wa Maadili ya Utamaduni wa Mtanzania, ambao unatumika nchini kote kama nyenzo muhimu ya kutoa elimu ya maadili kwa jamii. Katika muktadha huo, Wizara pia imeandaa Mkakati wa Kitaifa wa Kukabiliana na Mmomonyoko wa Maadili, unaoshirikisha makundi yote ya kijamii, ili kuhakikisha utekelezaji wa Serikali unakuwa shirikishi, wenye tija, na wenye uwezo wa kudhibiti viashiria vya mmomonyoko wa maadili vinavyojitokeza.

Uandaaji wa Mkakati huu umehusisha makundi mbalimbali, ili kuufanya uwe hai na wenye uwezo wa kutumika kwa kipindi cha muda mrefu (miaka 10). Aidha, Mkakati huu unatoa nafasi ya kufanya maboresho kulingana na mabadiliko ya kisera, kisheria, au miongozo mingine ya kitaifa.

Tuna imani kubwa kuwa makundi yaliyobainishwa katika mkakati huu yatatekeleza majukumu yao ipasavyo ili kudumisha misingi ya maadili ya taifa letu. Natoa rai kwa viongozi wa ngazi zote kutekeleza wajibu wao kama ilivyoelekezwa katika Mkakati huu.

**Bw. Gerson P. Msigwa**
**KATIBU MKUU NA MSEMAJI MKUU WA SERIKALI**

# SHUKRANI



Kwa heshima na taadhima na kwa niaba ya Sekta ya Maendeleo ya Utamaduni, ninapenda kutoa shukrani zangu za dhati kwa Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa kuendelea kutoa msisitizo wa kisera na kiuongozi juu ya umuhimu wa kuenzi mila, desturi na maadili kama msingi wa maendeleo endelevu, utawala bora, ustawi wa jamii na kulinda tunu za Taifa letu. Aidha, ninamshukuru Mheshimiwa Paul Christian Makonda (Mb.), Waziri wa Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo, pamoja na Ndugu Gerson P. Msigwa, Katibu Mkuu wa Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo na Msemaji Mkuu wa Serikali na Menejimenti yote ya Wizara kwa kutambua umuhimu wa kuandaliwa kwa Mkakati wa Kitaifa wa Kukabiliana na Mmomonyoko wa Maadili. Ni hakika pasi na shaka kuwa, kazi hii isingekamilika kwa wakati pasipo nasaha, miongozo na maelekezo yao ya kimkakati.

Mkakati huu umeweka bayana kwa ushahidi wa kijamii, kisheria na kihistoria changamoto ya mmomonyoko wa maadili inayolikabili Taifa letu, pamoja na mizizi yake katika mabadiliko ya kijamii, kiuchumi, kiutamaduni na kiteknolojia. Aidha, umeonesha kwa uwazi namna kupuuzwa kwa mila na desturi zetu za asili kumedhoofisha misingi ya malezi, mshikamano wa kijamii na utu wa Mtanzania. Kwa muktadha huo, ninatoa shukrani za pekee kwa wadau mbalimbali walioshiriki kutoa maoni, michango, na mapendekezo kupitia vikao kazi, semina, warsha, na majukwaa ya kijamii. Ushiriki wao umehakikisha kuwa mkakati huu unakuwa shirikishi na unagusa makundi yote ya kijamii, ikiwemo Wizara mbalimbali, taasisi binafsi na za Serikali, mashirika ya kimataifa, pamoja na asasi za kiraia ambazo zimeunga mkono mstakabali huu wa Taifa.

Vilevile, tunatambua mchango mkubwa wa watekelezaji wakuu wa mkakati huu ambao ni jamii yote ya Tanzania, ikijumuisha viongozi wa dini, viongozi wa kimila na viongozi wa kijamii ambao dhamira, usimamizi na uwajibikaji wao ni msingi wa mafanikio ya utekelezaji wa Mkakati huu. Halikadhalika,

tunawashukuru Maafisa Utamaduni kutoka mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa kwa maoni yao ya kitaalamu na jukumu lao la moja kwa moja katika kusimamia utekelezaji. Wizara ina imani thabiti kuwa wasimamizi hawa wataufanya mkakati huu kuwa hai na wenye tija kupitia utekelezaji makini katika ngazi ya mikoa na halmashauri kote nchini, ili kuleta mabadiliko chanya yanayokusudiwa.

Kwa namna ya pekee, ninatoa pongezi na shukrani kwa Sekretarieti ya Maandalizi ya Mkakati huu kutoka Idara ya Maendeleo ya Utamaduni, pamoja na kikosi kazi cha wataalam kutoka Idara na Vitengo mbalimbali vya Wizara Timu hii, ikiongozwa na Dkt. Julieth Kabyemela, Mkurugenzi Msaidizi wa Sehemu ya Urithi wa Utamaduni na Maadili ya Taifa, imeonesha weledi, uzalendo, na kujitoa kwa hali ya juu. Shukrani hizi ziwaendee pia Dkt. Resani Mnata, Mkurugenzi Msaidizi wa Sehemu ya Lugha, pamoja na Maafisa Utamaduni waandamizi na wakuu akiwemo Tito Lulandala, Sefania Motela, Elizabeth Hizza, Danieli Chilonzi, Hadija Kisubi, Emanueli Mlingo, Christopher Mhongole, Paschal Enoce, na Semeni Likomwa. Pia, tunatambua mchango wa Amina Nguli, Aron Msigwa, Sofia Limbu, Lenjima Mapenzi, Lucy Minungu, na Godfrey Manyama, ambao historia itaendelea kuwatambua kwa mchango wao katika kuweka msingi wa kitaasisi wa kulinda maadili ya Taifa.

Mwisho, shukrani zangu za dhati ziwaendee wataalamu kutoka Kituo cha Urithi wa Ukombozi wa Bara la Afrika na Baraza la Kiswahili la Taifa (BAKITA) kwa kufanya uhariri wa kina na kuhakikisha lugha iliyotumika ni fasaha, sanifu, na inayolinda hadhi ya Kiswahili kitaifa na kimataifa. Ni matarajio yangu kuwa mkakati huu utatumika kama rejea muhimu katika kupanga na kutekeleza mikakati madhubuti ya urithishaji maadili kuanzia ngazi ya familia, taasisi za elimu, hadi katika matumizi ya teknolojia na vyombo vya habari. Naamini utachochea mjadala mpana wa kitaifa unaojikita katika suluhisho, uwajibikaji wa pamoja, na uzalendo wa kweli kwa ajili ya vizazi vya sasa na vijavyo.

**Bw. Boniface L. Kadili**
**MKURUGENZI WA IDARA YA MAENDELEO YA UTAMADUNI**

# VIFUPISHO

| | |
|---|---|
| OR – IKULU | Ofisi ya Rais, Ikulu |
| OR – MUUB | Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora |
| OR – MV | Ofisi ya Rais, Maendeleo ya Vijana |
| OWM- TAMISEMI | Ofisi ya Waziri Mkuu, Tawala za Mikoa na Serikali za Mtaa |
| OWM - KAM | Ofisi ya Waziri Mkuu, Kazi, Ajira na Mahusiano |
| WHUSM | Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo |
| WEST | Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia |
| WMNN | Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi |
| WA | Wizara ya Afya |
| WMJJWMM | Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum |
| WMTH | Wizara ya Mawasiliano na Teknolojia ya Habari |
| WVB | Wizara ya Viwanda na Biashara |
| WK | Wizara ya Kilimo |
| WMU | Wizara ya Mifugo na Uvuvi |
| TCRA | Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania |
| UMT | Umoja wa Machifu Tanzania |

# SURA YA KWANZA

## 1. UTANGULIZI

Maadili ya Taifa ni msingi mkuu wa maendeleo ya Taifa lolote kwa sababu hubainisha viwango vya usahihi wa fikra na mienendo kuhusu mambo yote yanayohusu Taifa husika ili kulinda maslahi ya Taifa husika katika Nyanja zote za kiuchumi, kijamii, kisiasa na kimazingira.

Kwa kutambua umuhimu huo, Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, imebainisha katika Katiba yake ya Mwaka 1977 misingi na viwango ya maisha ya Watanzania vinavyoutambulisha utanzania wao. Misingi hiyo ambayo imebainishwa katika Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Sehemu ya Pili, Ibara ya 9 ni Utu, Umoja, Usawa, Utaifa na Uwajibikaji.



DIRA ya Taifa ya Maendeleo 2050 imebainisha kuwa, moja ya misingi inayoongoza maono ya Nchi kwa miaka 25 ijayo ni msingi wa kuwa na Taifa linalohifadhi, kukuza na kulinda maadili na tamaduni chanya. Hitaji la uelekeo huo, linatokana na changamoto ya mmomonyoko wa maadili inayolikabili Taifa na kuwa kikwazo kwa ustawi wa Nchi kwa sababu ya kukosa idadi toshelevu ya wananchi wazalendo, waadilifu na wanaowajibika vyema kiuchumi, kijamii na kimazingira.

Mkakati huu ni sehemu ya jitihada na mikakati ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa ajili ya kuunda jamii ya watu waadilifu na wenye maadili yanachochea uwajibikaji kijamii, kiuchumi na kimazingira.

## 1.1 DHANA ZA MSINGI

### 1.1.1 Maadili

Kanuni za Maadili ya Utendaji katika Utumishi wa Umma (2023), zinafafanua maadili kuwa ni viwango vilivyoainishwa vya kipi ni sahihi na kipi siyo sahihi ambavyo vinapaswa kuzingatiwa na wanajamii.

Kwa mujibu wa Kamusi Kuu ya Kiswahili (toleo la tatu), maadili ni mwenendo au utendaji unaokubalika na wengi.

Kwa mujibu wa Mwongozo wa Maadili (2022), maadili ni misingi na kanuni zinazoongoza mienendo inayokubalika na kuratibu mahusiano miongoni mwa makundi ya kijamii. Maadili ni zao la moja kwa moja la mila na desturi za utamaduni wa jamii husika.

Hivyo, kwa muktadha wa Mkakati huu, maadili ni kanuni za kiutamaduni zilizokubalika na jamii kutoa tafsiri ya kipi ni sahihi na kipi si sahihi katika masuala yote ya kimaisha ndani ya jamii hiyo. Maadili hutoa mwongozo wa fikra na mienendo sahihi kwa wanajamii ili kulinda maslahi ya wenye maadili yao na jamii yenyewe.

### 1.1.2 Maadili ya Mtanzania

Katika muktadha wa kitaifa, Maadili ya Mtanzania ni uzingatiaji wa misingi ya kijamii inayoutambulisha utanzania ambayo hutoa tafsiri ya namna ya maisha inayokubalika katika jamii zote nchini. Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania (1977), katika Sehemu ya Pili, Ibara ya 9, inabainisha kuwa misingi ya maisha ya Watanzania imejengwa juu ya nguzo kuu za Utu, Umoja, Usawa, Utaifa, na Uwajibikaji. Aidha, Ibara ya 30(2)(b) ya Katiba hiyo inalinda maadili ya jamii kama kipimo cha uhalali wa haki na uhuru wa mtu binafsi.

Tanzania ina utajiri wa urithi wa utamaduni unaojumuisha zaidi ya jamii 120 zenye lugha na historia tofauti, ambazo zimeunganishwa na lugha ya Kiswahili kama kitambulisho cha mshikamano wa kitaifa. Hivyo, maadili ya Mtanzania yanajumuisha nidhamu, utii, uaminifu, bidii ya kazi, na kutokubaguana kwa misingi ya kabila, dini, jinsia, wala rangi.

### 1.1.3 Mila na Desturi

Mila ni taratibu za kimaisha zinazoongoza mwenendo na jinsi ya kufanya mambo katika jamii fulani kulingana na historia na utamaduni wa jamii husika.

Kwa mujibu wa Sera ya Utamaduni (1997) Mila ni taratibu za kiutamaduni zinazohalalisha fikra na mienendo ya jamii fulani ambazo zimerithishwa kutoka kizazi kimoja kwenda kingine.

Desturi ni namna au tabia iliyozoeleka katika jamii inayoanza kama tabia ya mtu au kundi la watu na kisha kuenea na kukubalika katika jamii nzima. Desturi inakomaa na kurithishwa kwa kizazi kingine katika jamii hugeuka kuwa mila

Mjumuiko wa Mila na Desturi huzaa maadili ya jamii ambayo huongoza fikra na mienendo ya jamii hiyo katika masuala yote ya kimaisha.

### 1.1.4 Urithishaji na Usimamizi Maadili

Kwa muktadha wa Mkakati huu, urithishaji maadili ni utekelezaji wa afua zote zinazolenga kurithisha fikra na mienendo sahihi kwa watoto, vijana

na wanajamii kupitia malezi, makuzi, mafundo na mazingira yote ambayo humjenga mtu kuwa na mtindo wa maisha unaokubalika katika jamii.

Afua hizo hutekelezwa na taasisi za kijamii zenye wajibu wa malezi na makuzi pamoja na ushawishi kwa watoto, vijana na wanajamii kwa ujumla. Taasisi ya msingi katika orodha ya taasisi tajwa ni familia, ambayo ni taasisi yenye nafasi ya kwanza katika ukuaji wa mwanajamii yenye wajibu wa kutoa fursa kwa mwanajamii kujifunza na kufundwa fikra na mienendo sahihi hususani wakati wa utoto (umri wa miaka 0-7). Taasisi nyingine ni zile zinazotumia muda mrefu kukaa na watoto na vijana ikiwemo vituo vya malezi, shule, vyuo na jamii inayowazunguka.

Usimamizi wa maadili ni utekelezaji wa afua zote zinazolenga kulinda maadili ya jamii kupitia maelekezo, mahubiri/mawaidha, maonyo na uwajibishaji wa kijamii na kisheria kwa wanajamii wanaokiuka maadili ya jamii husika. Afua hizi hutekelezwa na taasisi za kijamii zinazorithisha maadili ikiwemo familia, shule, vyuo, jamii, taasisi za dini, vyombo vya ulinzi na mamlaka za udhibiti wa uharifu wa namna mbalimbali, na mahakama.

## 1.2 MMOMONYOKO WA MAADILI


Mmomonyoko wa maadili ni hali ya kuporomoka au kukiukwa kwa tabia njema, misingi, kanuni na mienendo inayokubalika katika jamii. Hali hii hujidhihirisha kupitia vitendo na mienendo inayokiuka matarajio ya kijamii na misingi ya maisha ya pamoja. Mmomonyoko wa maadili huonekana katika nyanja mbalimbali, ikiwemo matumizi yasiyofaa ya lugha, malezi duni ya watoto na vijana, mitindo ya mavazi isiyozingatia staha, pamoja na kuongezeka kwa vitendo vya ukiukwaji wa sheria na maadili ya jamii.

## 1.3 HISTORIA YA MMOMONYOKO WA MAADILI

Tanzania imepitia vipindi mbalimbali vya kihistoria, vikiwemo kipindi cha kabla ya ukoloni, wakati wa ukoloni, baada ya uhuru na kipindi cha sasa cha utandawazi. Vipindi hivyo vimekuwa na athari tofauti katika ujenzi na

mabadiliko ya maadili ya Mtanzania. Kabla ya ukoloni, jamii za Kitanzania ziliishi kwa mshikamano, zikitekeleza shughuli za kijamii na kiuchumi kwa misingi ya ushirikiano. Malezi ya watoto na vijana yalikuwa jukumu la jamii nzima, ambapo wazazi na walezi walirithisha maadili kupitia hadithi, mafundisho ya kijadi pamoja na elimu ya jando na unyago kutoka kizazi kimoja hadi kingine.

Kuingia kwa wakoloni katika ardhi ya Tanganyika kulileta mifumo mipya ya utawala, elimu na dini (Utamaduni Chombo cha Maendeleo, 1979). Mfumo wa elimu ya kikoloni ulilenga kukuza na kutukuza tamaduni za kigeni huku ukipunguza thamani ya utamaduni wa asili wa Waafrika. Aidha, elimu hiyo iliandaa rasilimali watu kwa ajili ya kuhudumia maslahi ya wakoloni. Vilevile, kuenea kwa dini za Kiarabu na Kimagharibi kulichangia kubadilisha mitazamo ya jamii kuhusu mila na desturi zao. Hatua hizi kwa pamoja zilisababisha kupungua kwa kuenzi na kurithisha maadili ya asili ya Mtanzania.



Baada ya kupata uhuru, Serikali ya Awamu ya Kwanza chini ya uongozi wa Hayati Mwalimu Julius Kambarage Nyerere ilianzisha Wizara ya Utamaduni wa Taifa na Vijana kwa lengo la kutambua, kukuza na kuendeleza mambo mema yaliyomo katika mila na desturi za Tanzania (WUTV, 1979). Lengo kuu lilikuwa kurithisha utamaduni na maadili ya Mtanzania kwa kizazi cha vijana. Hata hivyo, pamoja na jitihada hizo, mabadiliko ya sayansi, teknolojia na mifumo ya kijamii yameathiri kwa kiasi kikubwa urithishaji wa maadili, na hivyo kuchangia kuendelea kwa mmomonyoko wa maadili katika jamii.

## 1.4 SERA, SHERIA, KANUNI NA MIONGOZO INAYOSIMAMIA MAADILI

Suala la maadili limepewa uzito mkubwa katika nyanja mbalimbali za maendeleo ya Taifa, likihusisha sekta ya umma, sekta binafsi na taasisi za kidini. Kwa nyakati tofauti, viongozi wakuu wa Serikali wamekuwa wakisisitiza umuhimu wa kulinda na kuimarisha maadili ya Mtanzania. Mathalani, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, amekuwa akihimiza Watanzania kuzingatia mila na desturi njema kama msingi wa kulinda maadili ya Taifa.

Aidha, Dira ya Taifa ya Maendeleo 2050, imebainisha swala hili katika Msingi wa Tano (5), inalenga kujenga Taifa linalohifadhi, kukuza na kulinda maadili na tamaduni faafu ili kuimarisha umoja na utambulisho wa kitaifa. Nguzo ya Pili ya Dira hiyo inasisitiza uwekezaji katika malezi bora, elimu jumuishi na urithishaji wa maadili kuanzia utotoni hadi uzeeni kama msingi wa maendeleo endelevu ya rasilimali watu.

Pamoja na Dira ya Taifa ya Maendeleo 2050 na matamko ya viongozi, zipo Sera, Sheria, Mikakati na Miongozo mbalimbali ya usimamizi wa maadili, ambazo ni pamoja na:

### a) Sera ya Maendeleo ya Mtoto ya Mwaka 1993

Aya ya 8 inatamka kwamba, kwa sababu ya kuporomoka kwa maadili na kupuuza mila na desturi zetu, kumekuwa na ongezeko la kesi za ubakaji na unajisi wa watoto

**b) Sera ya Utamaduni ya Mwaka 1997**

Aya ya 6.1.6 inatamka kuwa Serikali itahakikisha kwamba shughuli za burudani zitolewazo hazipotoshi maadili ya taifa. Vilevile, Aya ya 8.1.1 inatamka kuwa, familia itatambuliwa kuwa ni asasi ya msingi na muhimu katika mfumo wetu wa jamii na itakuwa chimbuko na msingi wa kuendeleza maadili, elimu, mafunzo na utamaduni wetu.

**c) Sera ya Habari na Utangazaji ya Mwaka 2003**

Aya ya 1.2 na 2.2.1 za Sera ya Habari na Utangazaji ya Mwaka 2003; zinaeleza malengo ya Sera ni kulinda wanahabari wanaotekeleza wajibu wao kwa mujibu wa maadili ya taaluma na ya jamii; na kuhamasisha vyombo vya habari kutoa huduma kwa kuzingatia maadili ya taaluma na maadili ya jamii.

**d) Sera ya Taifa ya Wazee ya Mwaka 2003 Toleo la 2024**

Aya ya 5.2.26 inatamka kwamba mabaraza ya wazee yatakuwa na jukumu la kuchochea malezi chanya, uzalendo, maadili katika jamii na kusaidia katika utatuzi wa migogoro na changamoto mbalimbali katika jamii.

**e) Sera ya Taifa ya Maendeleo ya Vijana ya Mwaka 2007**

Aya ya 2.4.2 inaeleza malengo mahsusi ya Sera hii ni kukuza utamaduni na maadili mema kwa malezi na makuzi bora ya vijana.

**f) Sera ya Elimu na Mafunzo ya Mwaka 2014 Toleo la Mwaka 2023**

Aya ya 2.4.1 inatamka kuwa, elimu ya awali inalenga kumwandaa mtoto kimakuzi, kimwili, kiakili, kimaadili, kijamii na kijinsi.

**g) Sera ya Taifa ya Jinsia na Maendeleo ya Wanawake ya Mwaka 2023**

Aya ya 3.2.2 inahamasisha na kuendeleza malezi na makuzi chanya yanayozingatia jinsia katika ngazi ya familia na jamii katika kukabiliana na mmonyoko wa maadili.

### h) Sera ya Taifa ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya ya Mwaka 2024

Aya ya 3.3 inatamka kuwa, matumizi ya dawa za kulevya yanaathiri nguvu kazi ya taifa na kusababisha mmomonyoko wa maadili na ustawi wa jamii kwa ujumla.

Pamoja na kuwa na matamko ya Sera mbalimbali yanayoelekeza utekelezaji wa masuala ya maadili, pia usimamizi wa maadili umebainishwa katika Sheria mbalimbali za kisekta zikiwa ni pamoja na:

### a) Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, 1977

Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya 1977 inaeleza maadili hasa kupitia Sura ya Pili, ambapo, Ibara ya 8: Inasisitiza misingi ya uendeshaji wa nchi, ikiwemo uadilifu, uwajibikaji, haki, na heshima kwa utu wa binadamu katika uongozi na utawala. Ibara ya 9: Inaelekeza Serikali na vyombo vyake kuzingatia maadili ya jamii, haki za binadamu, usawa, kupinga rushwa, na kuendeleza maadili mema katika matumizi ya madaraka na rasilimali za umma. Ibara ya 26: Inaweka wajibu kwa kila raia kuheshimu Katiba na sheria za nchi, jambo linalojumuisha mwenendo wa kimaadili katika jamii na utumishi wa umma. Kimsingi, Katiba inaweka misingi ya maadili na uadilifu kama dira ya uongozi na utawala bora, huku utekelezaji wa kina, hasa kwa viongozi wa umma ukifanywa kupitia sheria maalum kama Sheria ya Maadili ya Viongozi wa Umma.

### b) Sheria ya Mtoto, Sura ya 13

Kifungu cha 9(3)(a); Kifungu cha 12 na 82 (2) kinazuia ajira zinazoweza kuwa na madhara kwa afya, elimu, akili, mwili au kwa maendeleo ya kimaadili ya mtoto.

### c) Sheria ya Ndoa, Sura ya 29

Kifungu cha 14(1) kinazuia mahusiano au ndoa baina ya ndugu ambapo kwa kufanya hivyo ni kinyume cha Sheria ya Ndoa na Sheria ya Kanuni ya Adhabu Sura ya 16.

### d) Sheria ya Makosa ya Mtandao, Sura ya 443

Kifungu cha 13(1) (a) na (b) kinaainisha makosa na adhabu zinazohusiana na matumizi ya mfumo wa kompyuta na Teknolojia ya Habari na Mawasiliano. Sheria hii inaeleza makosa ya mtandao kama vile kuingilia mawasiliano ya kompyuta au mifumo ya kompyuta kinyume cha sheria, wizi wa taarifa kimtandao, usambazaji wa ponografia, ponografia ya watoto na kamari mitandaoni kinyume cha Sheria. Matendo haya ni kinyume na maadili ya Mtanzania.

### e) Sheria ya Huduma za Habari, Sura ya 229

Kifungu cha 26(2) kinaanzisha Baraza la Habari Tanzania ambalo katika utekelezaji wa majukumu yake linatakiwa kuzingatia umoja wa kitaifa, usalama wa taifa, uhuru, uadilifu na maadili ya umma.

### f) Sheria ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa, Sura ya 329

Kifungu cha 15-39 kinasisitiza uadilifu, uwajibikaji na haki katika jamii, viongozi na watumishi wa umma kwa kuzuia masuala ya rushwa.

### g) Sheria ya Filamu na Michezo ya Kuigiza, Sura ya 230

Kifungu cha 2 kinaipa mamlaka Bodi ya Filamu Tanzania kukagua na kutoa madaraja ya filamu kwa kuzingatia jinsi, umri, muda wa kuoneshwa ili kulinda maadili katika jamii. Aidha, Kanuni za Filamu na Michezo ya Kuigiza, 2019 zinataka filamu zote zinazoandaliwa na kuoneshwa kwa jamii lazima zihakikiwe kwa lengo la kuzingatia maadili ya Mtanzania kutokana na maudhui iliyonayo na ujumbe inayokusudia kufikisha kwa jamii.

### h) Sheria ya Maadili ya Viongozi wa Umma, Sura ya 398

Kifungu cha 19(2) kinaainisha majukumu ya Sekretarieti ya Maadili ya viongozi wa umma katika kusimamia tabia na mienendo ya Viongozi wa Umma ikiwemo kudhibiti vitendo vyote vya ukiukaji wa Maadili. Aidha, Kanuni za Sheria ya Maadili ya Viongozi wa Umma (Udhibiti wa Mgongano wa Maslahi) za mwaka 2020

zinafafanua mgongano wa maslahi kwa mujibu wa kanuni hizi ni pale kiongozi anapokuwa na maslahi binafsi ambayo yanaathiri utekelezaji wa majukumu yake kwa umma; yanayoweza kuathiri utekelezaji wa majukumu yake kwa umma; na yanayoonekana kuathiri utekelezaji wa majukumu yake kwa umma.

i) **Sheria ya Kanuni ya Adhabu Sura ya 16.**

Kifungu cha 129A – 162 vinazuia makosa na kutoa adhabu ya makosa ya ubakaji, kujaribu kubaka, udhalilishaji wa kingono, uzinzi,

## 1.5 UHALALI WA KUANDAA MKAKATI

Uandaaji wa Mkakati wa Taifa wa Kukabiliana na Mmomonyoko wa Maadili kwa kipindi cha 2026/27–2036/37 umetokana na haja ya dharura ya kukabiliana na changamoto inayoendelea ya kuporomoka kwa maadili katika jamii ya Kitanzania. Mmomonyoko wa maadili umejitokeza katika nyanja za kijamii, kiuchumi, kisiasa, kiutamaduni na kiteknolojia, na kuathiri ustawi wa jamii, mshikamano wa kitaifa, ufanisi wa taasisi na maendeleo endelevu ya Taifa (Mwongozo wa Maadili, 2022).

Katika miaka ya hivi karibuni, kumekuwapo ongezeko la vitendo vinavyokiuka maadili, ikiwemo kudhoofika kwa malezi ya familia, matumizi mabaya ya lugha, mitindo isiyozingatia staha, rushwa, ukatili wa kijinsia, matumizi ya dawa za kulevya, uhalifu wa kimtandao, na kupungua kwa uwajibikaji katika utoaji wa huduma za jamii (Sera ya Taifa ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya, 2024; Sheria ya Makosa ya Mtandao, Sura ya 443).

Vilevile, mabadiliko yanayotokana na utandawazi, maendeleo ya teknolojia na ushawishi wa tamaduni za kigeni yameathiri urithishaji wa maadili kutoka kizazi kimoja hadi kingine. Hali hii imesababisha kupungua kwa nafasi ya familia na mifumo ya kijadi katika malezi ya watoto na vijana (Sera ya Utamaduni, 1997).

Ingawa kuna Sera, Sheria na Kanuni mbalimbali zinazolinda maadili, utekelezaji wake umekuwa wa kisekta na usio na uratibu wa pamoja. Hali hii imesababisha kukosekana kwa mfumo wa kitaifa unaoelekeza wajibu wa Serikali, sekta binafsi, taasisi za dini, familia, jamii na wadau wengine katika kulinda na kuimarisha maadili ya Mtanzania (Sera ya Utamaduni, 1997; Sera ya Taifa ya Maendeleo ya Vijana, 2007). Aidha, tafiti na maoni ya wadau mbalimbali yameonesha kuwa jitihada zinazofanywa bila uratibu wa kitaifa hazijafanikiwa kikamilifu kudhibiti mmomonyoko wa maadili.



Vilevile, uandaaji wa Mkakati huu ni utekelezai wa maelekezo ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, aliyoyatoa wakati wa kilele cha Tamasha la Tatu la Kitaifa la Utamaduni tarehe 24 Septemba, 2024 mkoani Ruvuma ambapo aliiagiza Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo kwa kushirikiana na wadau kuandaa mkakati wa taifa wa kukabiliana na mmomonyoko wa maadili. Agizo hilo lililenga kuweka mfumo wa kitaifa unaoaunganisha wajibu wa Serikali na wadau wengine katika kurithisha, kulinda na kuenzi maadili ya Mtanzania.

Mkakati huu unalenga kuwa nyenzo madhubuti ya kujenga jamii yenye msingi imara wa kimaadili, uwajibikaji, uzalendo na mshikamano wa kitaifa, sambamba na kukuza maendeleo endelevu ya Taifa katika muktadha wa mabadiliko ya kijamii na kiteknolojia.

## 1.6 METHODOLOJIA ZILIZOTUMIKA KUANDAA MKAKATI

Uandaaji wa Mkakati huu umeongozwa na methodolojia jumuishi, shirikishi na inayozingatia ushahidi. Njia zilizotumika ziliwezesha ukusanyaji wa taarifa kutoka vyanzo mbalimbali, uchambuzi wa kina, na kushirikisha wadau ili kuhakikisha mkakati unakidhi mahitaji halisi ya jamii. Mbinu zilizotumika ni pamoja na mapitio ya nyaraka, mahojiano ya ana kwa ana, ujazaji wa dodoso, majadiliano ya makundi, kuangalia hali halisi, na vikao vya wadau.

### 1.6.1 Mapitio ya Nyaraka

Taarifa kuhusu hali ya maadili nchini zilikusanywa na kuchambuliwa kupitia mapitio ya nyaraka mbalimbali za kisheria na kimaendeleo. Nyaraka zilizopitiwa ni pamoja na Sera, Sheria, Kanuni, Mipango ya Kitaifa, machapisho ya kitaaluma, Hotuba za Viongozi Wakuu, na miongozo ya kisekta ili kuhakikisha Mkakati huu unaoana na mwelekeo wa nchi.

### 1.6.2 Mahojiano ya Ana kwa Ana

Mbinu hii ilitumika kukusanya taarifa za msingi (primary data) kutoka kwa wadau wa kada mbalimbali. Mahojiano hayo yalihusisha Wakurugenzi,

wataalamu wa sekta husika, watumishi wa umma, wasanii, waandishi wa habari, wazalishaji wa maudhui (content creators), waendesha bodaboda, wahadhiri na wanafunzi. Njia hii imewezesha kupata ushuhuda wa moja kwa moja, mitazamo, na uzoefu ambao umeongeza uhalisia na ubora wa taarifa za Mkakati.

### 1.6.3 Ujazaji wa Dodoso

Madodoso yaliandaliwa na kusambazwa kwa wahojiwa ili kuwapa fursa ya kutoa maoni yao kwa uhuru na faragha. Mbinu hii ilisaidia kukusanya takwimu na maoni kutoka kwa idadi kubwa ya watu kwa muda mfupi, huku ikihakikisha kuwa taarifa zinazopatikana hazina ushawishi wa nje.

### 1.6.4 Vikao vya Wadau

Wadau muhimu ambao ni Serikali, sekta binafsi, taasisi za kidini, jamii na wataalamu walihusishwa ili kupata maoni, mapendekezo, ushauri na mitazamo tofauti ili Mkakati uweze kutekelezeka. Vilevile, vikao vya uhakiki na mapitio vilifanyika ili kuboresha Mkakati. Mkakati uliwasilishwa kwa wadau mbalimbali kwa ajili ya kufanya mapitio, kutoa maoni na mapendekezo ya kuboresha Mkakati huo kwa ajili ya uandaaji wa toleo la mwisho, uchapishaji na utekelezaji.

### 1.6.5 Kuangalia Hali Halisi


Uchunguzi wa moja kwa moja ulifanyika kuangalia hali halisi ya maadili katika ngazi ya familia hadi taifa. Matukio yaliyoonesha mmomonyoko wa maadili ni pamoja na kutokutekeleza wajibu wa kijamii, mavazi yasiyofaa, matumizi ya lugha chafu, rushwa, wizi, ubakaji, matumizi ya madawa ya kulevya, ulawiti, mahusiano ya jinsia moja, uongo na udanganyifu. Mbinu hii ilisaidia kuelewa kiwango cha mmomonyoko wa maadili katika jamii na maeneo yanayohitaji kipaumbele cha kuboresha.

### 1.6.6 Majadiliano ya Makundi

Majadiliano ya makundi yalifanyika kati ya wataalam, wanafunzi wa ngazi zote za elimu, viongozi wa kimila, viongozi wa dini, na vijana. Mbinu hii ililenga kupata mitazamo mbalimbali, uzoefu, maoni na mapendekezo kuhusu mmomonyoko wa maadili, na kutoa taarifa za kina zinazosaidia katika uandaaji wa Mkakati madhubuti unaozingatia tofauti za kiumri na kijiografia.

## 1.7 NUKUU NA MITIZAMO YA VIONGOZI KUHUSU MAADILI NA UZALENDO

Viongozi Wakuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, tangu enzi za Waasisi hadi sasa, wamekuwa na mtazamo mmoja thabiti, kuwa Maadili ni uti wa mgongo wa Taifa. Uzalendo hautafsiriwi tu kama kuipenda nchi, bali kama kitendo cha kuishi kwa uadilifu, kulinda rasilimali za umma, na kurithisha fikra na mienendo sahihi kwa vizazi vijavyo. Mmomonyoko wa maadili unatazamwa kama tishio kwa usalama na ustawi wa Nchi kijamii na kiuchumi. Katika jedwali lifuatalo, ni baadhi ya nukuu za viongozi kuhusu maadili na uzalendo.



## Jedwali Na. 1 Nukuu na Mitazamo ya Viongozi Kuhusu Maadili na Uzalendo

| Na. | Nukuu | Jina la kiongozi | Mafunzo ya nukuu katika kuendeleza maadili na uzalendo kuhusu mitazamo ya viongozi |
|---|---|---|---|
| 1. | "Uzalendo ni upendo wa dhati kwa nchi yako, na unaambatana na kutambua majukumu yako kama raia". | Hayati, Mwalimu Julius Kambarage Nyerere, Rais wa awamu ya kwanza, Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. | Serikali ni watu. Kila mmoja wetu ana jukumu la kuwajibika kwa maendeleo ya nchi yetu." - Hii inasisitiza umuhimu wa ushiriki wa raia katika kuleta mabadiliko chanya. |
| 2. | "Nchi inaweza kuwa na rasilimali nyingi, lakini bila maadili mema, haitakuwa na uwezo wa kuendelea". | Hayati, Mwalimu Julius Kambarage Nyerere, Rais wa awamu ya kwanza, Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. | Mwalimu alikumbuka kuwa maadili yanahitajika ili rasilimali zitumike vizuri. |
| 3. | "Tunapaswa kujifunza kuheshimu, kusaidia, na kujali wenzetu ili kuweza kuendeleza umoja na mshikamano wa taifa." | Hayati, Mwalimu Julius Kambarage Nyerere, Rais wa awamu ya kwanza, Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. | Taifa lolote ili liweze kuendelea linahitaji umoja na mshikamano. |
| 4. | "Taifa lisilo na maadili haliwezi kudumu, hata kama lina utajiri mkubwa". | Hayati, Mwalimu Julius Kambarage Nyerere, Rais wa awamu ya kwanza, Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. | Maadili yanahitajika ili rasilimali zitumike vizuri katika Taifa. |
| 5. | "Maendeleo ya kweli hayawezi kupatikana bila uadilifu na heshima kwa sheria". | Hayati, Alhaji Ally Hassan Mwinyi, Rais wa awamu ya pili, Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. | Jambo muhimu linaloweza kuchochea maendeleo ya jamii ni uadilifu na heshima ya sheria, kanuni, taratibu na miongozo. |
| 6. | "Uzalendo ni kujitolea kwa ajili ya watu wetu na kutafuta njia bora ya kuwakomboa". | Hayati, Benjamin William Mkapa, Rais wa awamu ya tatu, Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. | Kila mmoja ana wajibu wa kutafuta suluhisho bora la changamoto zinazoikabili jamii yake na ukombozi wa jamii unapatikana kupitia mshikamano, juhudi za pamoja na uwajibikaji. |

| | | | |
|---|---|---|---|
| 7. | "Rushwa ni adui wa haki, adui wa maendeleo, na adui wa maadili ya taifa". | Hayati, Benjamin William Mkapa, Rais wa awamu ya tatu, Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. | Wananchi na viongozi wanatakiwa kuepukana na rushwa ili kuwa na maadili na kupata maendeleo. |
| 8. | "Maadili ni nguzo muhimu katika kuimarisha uzalendo; tunahitaji viongozi waadilifu wanaoweza kutuongoza katika safari hii". | Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete Rais wa awamu ya nne, Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. | Viongozi wanatakiwa kusimamia maadili ya kazi, uadilifu, uwajibikaji na uzingatiaji wa sheria, kanuni na miongozo ya utumishi wa umma |
| 9. | "Katika kujenga uzalendo, lazima tuweke mbele maslahi ya wananchi wetu na kuhakikisha rasilimali za taifa zinawanufaisha wote". | Hayati, Dkt. John Pombe Magufuli, Rais wa awamu ya tano, Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. | Uzalendo wa kweli hauishii kwenye maneno, bali unaonekana kupitia vitendo vinavyolenga maslahi ya wananchi wote viongozi na raia wanapaswa: -<br>(i) Kuweka mbele maslahi ya umma badala ya maslahi binafsi au ya kikundi fulani.<br>(ii) Kulinda na kusimamia rasilimali za taifa kwa haki, ili ziwafikie na kuwanufaisha wananchi wote kwa usawa.<br>(iii) Kuwajibika katika maamuzi, kwani rasilimali ni mali ya taifa zima, si watu wachache.<br>(iv) Kujenga mshikamano na haki ya kijamii, jambo linaloimarisha umoja wa kitaifa. |

| | | | |
|---|---|---|---|
| 10. | “Kiongozi asiye mwadilifu hana haki ya kuwaongoza wengine”. | Hayati, Dkt. John Pombe Magufuli, Rais wa awamu ya tano, Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. | Serikali ni mali ya wananchi, na viongozi ni watumishi wa wananchi. |
| 11. | “Uzalendo wetu unapaswa kuonekana katika vitendo vyetu vya kila siku ni wajibu wetu kuimarisha umoja na mshikamano”. | Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa awamu ya sita, Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. | Kupenda nchi kunatakiwa kuonekane kwa vitendo vya kila siku vya kuimarisha umoja na mshikamano. |
| 12. | “Maadili mema ni msingi wa amani, mshikamano, na maendeleo ya taifa”. | Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa awamu ya sita, Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. | Taifa bila maadili mema haliwezi kuwa na maendeleo. |
| 13. | "Tusiruhusu utandawazi utufanye tuteleze na kuacha asili yetu. Maendeleo ya sayansi na teknolojia yasitumike kuharibu mila, desturi, na staha ya Mtanzania. Ni lazima tulinde watoto wetu dhidi ya maudhui yanayochafua akili zao." | Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa awamu ya sita, Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. | Teknolojia itumike kulinda maslahi ya mwanchi mmoja mmoja na taifa kwa ujumla na siyo kuchochea mmomonyoko wa maadili. |
| 14. | "Wizara na wadau lazima washirikiane kuandaa mikakati ya makuzi bora; maadili si jukumu la Serikali pekee, ni jukumu la familia kwanza." | Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa awamu ya sita, Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. | Kurithisha na kulinda maadili ni jukumu la jamii, wadau na serikali. |

## 1.8 MATUMIZI YA SEMI ZA KISWAHILI KATIKA KUJENGA MAADILI KWA WANAJAMII

Semi za Kiswahili ni hazina muhimu ya maarifa ya kijamii, kiutamaduni na kimaadili iliyorithishwa kizazi hadi kizazi kupitia mapokeo ya simulizi. Semi hizi, zinazojumuisha methali, nahau, vitendawili na misemo, zilitumiwa na wahenga kama nyenzo kuu ya malezi, elimu ya tabia na uongozi wa kijamii. Katika muktadha wa Mkakati wa Kukabiliana na Mmomonyoko wa Maadili, semi za Kiswahili zinatambuliwa kama chombo cha kimkakati cha kujenga, kurejesha na kuimarisha maadili chanya miongoni mwa wananchi.

Kihistoria, semi za Kiswahili zilikuwa mfumo usioandikwa wa kanuni za jamii, uliotumika kusimamia mwenendo wa watu binafsi na makundi bila kutumia adhabu kali au lugha ya amri. Kupitia lugha ya picha, mafumbo na busara, semi zilihamasisha utii, heshima, uwajibikaji na mshikamano wa kijamii. Hivyo, matumizi ya semi katika mkakati huu yanalenga kuhuisha mbinu za jadi za malezi kwa kuzilinganisha na mazingira ya sasa ya kijamii, kiuchumi na kiteknolojia.

Kwa ujumla, mafundo yanayopatikana kupitia semi za Kiswahili yalilenga kujenga misingi ifuatayo ya kimaadili: Kutambua thamani ya mtu kulingana na nafasi na wajibu wake katika jamii; Kukuza utamaduni wa kufanya kazi kwa bidii na uadilifu; Kuheshimu wakubwa, viongozi na mamlaka halali; Kulinda na kuheshimu taasisi ya ndoa na familia; na Kuhimiza utekelezaji wa wajibu wa kijamii na kitaifa.

Miongoni mwa semi hizo, methali zimekuwa na nafasi ya kipekee katika ujenzi wa maadili. Methali ni usemi mfupi wa hekima na busara unaofumbata tajriba ya muda mrefu ya maisha ya jamii. Zina muundo wa kisanaa unaotumia lugha ya picha na mafumbo kuelezea ukweli wa maisha, changamoto na matarajio ya jamii. Asili ya methali nyingi za Kiswahili inahusishwa na mwingiliano wa binadamu na mazingira yake, ikiwamo shughuli za kilimo, uvuvi, ufugaji na biashara, hususan katika ukanda wa Pwani ya Afrika Mashariki.

Katika mazingira ya jadi, methali zilitumika kama rejea ya maamuzi, usuluhishi wa migogoro, na mwongozo wa mwenendo wa kijamii. Umuhimu wake katika kulinda maadili unatokana na uwezo wake wa kutoa mafunzo, onyo na marekebisho ya tabia kwa staha, bila kuibua migogoro au kudhalilisha mhusika. Kwa njia hii, methali zimeendelea kuwa "mwalimu wa kimya" anayelinda misingi ya utu, uadilifu, unyenyekevu na heshima, hata katika nyakati za mabadiliko ya kasi ya kijamii.

### 1.8.1 Uchambuzi wa Methali Kimaadili

Zifuatazo ni baadhi ya methali teule za Kiswahili na mchango wake katika kujenga na kuimarisha maadili ya jamii. Methali hizo zimegawanywa katika makundi ya kimaadili kama ifuatavyo:

## A. Maadili ya Familia na Uhusiano

- Mke ni nguo, mume ni kilemba: Inasisitiza kuwa mume na mke ni taasisi moja inayotegemeana, mke husitiri siri za ndani na mume hubeba heshima na hadhi ya familia.
- Asiyefunzwa na mamae, hufunzwa na ulimwengu: Inasisitiza kuwa elimu ya awali na malezi huanzia nyumbani. Inatahadharisha kuwa maisha (ulimwengu) yana adhabu kali kwa wasio na malezi ya msingi.
- Eda ni ada ya faida: Inahimiza kufuata taratibu na sheria za mpito (kama baada ya kufiwa au talaka) ili kupata heri na usalama wa kijamii.

## B. Uongozi, Hekima, na Uzoefu

- Mti mkuu hukigwa, wana wa ndege huyumbayumba: Inasisitiza umuhimu wa wazee na viongozi kama nguzo za jamii. Ikiwa mifumo ya kiongozi/mzee itavunjika, kizazi kipya kinapoteza mwelekeo.
- Makukuu ya mwewe si mapya ya kengewa: Inafundisha heshima kwa wazee na wastaafu. Inasisitiza kuwa uzoefu wa mzee aliyechakaa una thamani kubwa kuliko nguvu za kijana asiye na maarifa.
- Chungu kidogo huchemsha mapema: Huonya dhidi ya hasira za haraka na ukosefu wa subira, hasa kwa vijana au watu wenye mamlaka madogo.

## C. Utambulisho, Uzalendo na Tabia Binafsi

- Mwacha asili ni mtwana: Huonya dhidi ya kukumbatia tamaduni za kigeni na kudharau asili ya Kitanzania. Inasisitiza kuwa utu wa mtu upo kwenye mizizi yake.
- Chanda chema huvikwa pete: Inahimiza uadilifu binafsi, fursa na heshima huenda kwa wenye tabia njema na waliojiandaa.
- Ghururi na binadamu hawaachani: Inahimiza unyenyekevu na kutahadharisha dhidi ya kiburi kinachotokana na mafanikio ya muda mfupi.

### D. Riziki, Haki na Tahadhari

- Kila mtoto na koja lake: Inafundisha kuridhika na kutooneana wivu. Kila mwanadamu ana kipaji na riziki yake ya kipekee, hivyo kuzuia mashindano yasiyo na tija.
- Mambo ni kangaja, huenda yakaja: Inasisitiza umuhimu wa kufanyia kazi dalili ndogo za mmomonyoko wa maadili kabla hazijawa janga kubwa la kitaifa.

Kwa ujumla, matumizi ya semi za Kiswahili ni nyenzo muhimu na yenye uhalali wa kitamaduni katika kujenga, kulinda na kuendeleza maadili ya Mtanzania. Semi hizi zimebeba hekima, busara na uzoefu wa kihistoria unaoelekeza mwenendo wa mtu binafsi na jamii kwa misingi ya utu, heshima, uwajibikaji na mshikamano. Katika mazingira ya sasa yanayokabiliwa na changamoto za mabadiliko ya kijamii, kiteknolojia na kiutamaduni, semi za Kiswahili zinaendelea kuwa daraja kati ya maadili ya jadi na mahitaji ya jamii ya kisasa.

Mkakati huu unatambua kuwa kuimarisha maadili hakuhitaji mbinu za kisheria na kiutawala pekee, bali pia matumizi ya lugha na falsafa inayokubalika kijamii na kueleweka kwa urahisi. Kupitia semi, ujumbe wa maadili unaweza kufikishwa kwa staha, kwa kina na kwa ufanisi mkubwa, hususan kwa vijana na jamii za msingi. Hivyo, kuzijumuisha semi za Kiswahili katika elimu, uhamasishaji wa umma, vyombo vya habari na programu za malezi ni hatua ya kimkakati ya kuhakikisha kuwa maadili ya Mtanzania yanabaki hai, yanarithiwa kizazi hadi kizazi, na yanatumika kama msingi wa maendeleo endelevu ya kijamii na kitaifa.

## 1.9 MSINGI WA KINADHARIA WA MKAKATI

Mkakati wa Taifa wa Kukabiliana na Mmomonyoko wa Maadili umejikita katika misingi madhubuti ya kinadharia inayolenga kuelewa chanzo, muktadha na mienendo ya mmomonyoko wa maadili pamoja na namna bora ya kuleta mabadiliko chanya na endelevu katika jamii. Sura hii inaeleza nadharia kuu mbili zitakazotumika kuongoza utekelezaji wa mkakati huu, ambazo ni Nadharia ya Mabadiliko ya Kijamii na Kimfumo (Social–Ecological Theory of Change) na Nadharia ya Mabadiliko ya Kijamii Yanayojengwa juu ya Maadili (Value-based Theory of Change)

Nadharia hizi mbili zinakamilishana kwa kuwa moja inalenga mifumo na mazingira ya kijamii yanayoathiri tabia za watu, huku nyingine ikisisitiza nafasi ya maadili, misingi ya utu na dhamira ya ndani katika kuleta mabadiliko ya kijamii.

### 1.9.1 Nadharia ya Mabadiliko ya Kijamii na Kimfumo (Social–Ecological Theory of Change-SETC)

Nadharia ya Mabadiliko ya Kijamii na Kimfumo inaeleza kuwa tabia, mienendo na maadili ya watu huathiriwa na mwingiliano wa mifumo mbalimbali ya kijamii inayomzunguka mtu. Nadharia hii inatambua kuwa ili kuleta mabadiliko chanya ya kimaadili, ni lazima hatua zichukuliwe katika ngazi nne za jamii kama ifuatavyo:-

- Ngazi ya Mtu Binafsi: Kulenga maarifa, mitazamo, na stadi za maisha kupitia elimu ya uraia na uzalendo.
- Ngazi ya Mahusiano (Familia na Marika): Kuimarisha malezi chanya na nafasi ya wazee wa mila na viongozi wa dini katika urithishaji maadili.
- Ngazi ya Taasisi na Jamii: Kuhakikisha shule, sehemu za kazi, na vyombo vya habari vinakuwa na kanuni madhubuti za uadilifu.
- Ngazi ya Kitaifa na Kimfumo: Kuboresha sera, sheria, na mifumo ya utawala ili kutoa mwelekeo wa kisheria na kijamii katika kulinda tunu za Taifa.

### 1.9.2 Nadharia ya Mabadiliko ya Kijamii Yanayojengwa Juu ya Maadili (Value-Based Social Change Theory - VBCT)

Nadharia ya Mabadiliko ya Kijamii Yanayojengwa juu ya Maadili inasisitiza kuwa mabadiliko ya kweli na endelevu ya kijamii hayawezi kupatikana kwa sheria, adhabu au mifumo pekee bali yanategemea dhamira ya ndani (Intrinsic motivation). Nadharia hii inaeleza kuwa maadili ndiyo msingi wa maamuzi, tabia na mahusiano ya kijamii. Kwa mujibu wa nadharia hii, jamii yenye maadili imara hujengwa kwa:- kukuza dhamira ya ndani ya kutenda mema; kuheshimu utu wa binadamu; na kujenga uwajibikaji wa hiari badala ya kulazimishwa. Misingi mikuu ya nadharia ya VBCT ni:-

- Utu na Heshima: Kuchukulia "Utu" kama kigezo kikuu cha maamuzi yote ya kijamii.

- Uwajibikaji wa Hiari: Kujenga jamii inayotenda haki kwa sababu ni jambo sahihi, si kwa sababu inashurutishwa.
- Uongozi wa Mfano: Kutumia viongozi kama vielelezo hai (role models) vya maadili yanayohubiriwa.
- Umiliki wa Jamii: Kuhakikisha jamii haioni maadili kama shinikizo kutoka nje, bali kama mali yao ya asili.

### 1.9.3 Muunganiko wa Nadharia Mbili Katika Mkakati


Mkakati wa Taifa wa Kukabiliana na Mmomonyoko wa Maadili umeunganisha nadharia hizi mbili kwa mtazamo jumuishi. Nadharia ya Mabadiliko ya Kijamii na Kimfumo inasaidia kuelewa wapi na kwa nini mmomonyoko wa maadili hutokea, ambpo imejikita katika kubadili mazingira (sheria, sera, miundombinu ya elimu na mifumo mbalimbali). Nadharia ya Mabadiliko ya Kijamii Yanayojengwa juu ya Maadili inaeleza jinsi mabadiliko chanya ya kimaadili yanavyoweza kupatikana na kudumishwa kwa kuzingatia kubadili mtu (malezi, imani, utamaduni na uongozi wa mfano).

Hivyo basi, kwa pamoja, nadharia hizi zinaongoza uundaji wa malengo ya Mkakati, uchaguzi wa mikakati na shughuli, ufuatiliaji na tathmini ya matokeo, na uhakikisho wa uendelevu wa mabadiliko ya kimaadili. Kwa msingi huo, Mifumo SETC inalinda maadili yasichezewe na Imani za watu (VBC) zinalisha na kuhuisha mifumo hiyo.

Hivyo basi, kupitia nadharia hizi, Mkakati huu unahama kutoka kwenye kutoa matamko pekee na kuelekea kwenye mabadiliko ya kimfumo na kifikra. Lengo ni kutengeneza Taifa ambalo kila mfumo unahimiza uadilifu, na kila mwananchi ana dhamira ya ndani ya kuishi kwa staha, uzalendo, na utu.

### 1.9.4 Mfumo wa Dhana wa Mkakati

Mkakati huu unatekelezwa kwa kuzingatia mfumo wa dhana ambao umeundwa kutokana na nadharia mbili za uundaji wa mkakati huu.




**Mchoro Na.1 Mfumo wa Dhana wa Mkakati**

# SURA YA PILI
# HALI HALISI YA MAADILI ILIVYO NCHINI

## 2 UTANGULIZI

Kuporomoka kwa maadili nchini Tanzania ni changamoto inayozidi kuongezeka kadri mabadiliko ya kijamii, kiuchumi na kiteknolojia yanavyotokea, ikiacha alama ya mashaka kwa mustakabali wa taifa. Hali hii inachangiwa kwa kiasi kikubwa na kupuuzwa, kubezwa na kudharauliwa kwa mila na desturi za Kitanzania ambazo kwa muda mrefu zimekuwa msingi wa maadili ya taifa letu. Kumekuwapo na mwelekeo wa kasi wa kuiga tamaduni za kigeni ambazo baadhi yake zinakinzana waziwazi na misingi ya utu, staha na utamaduni wa Mtanzania.

Uzito wa changamoto hii unadhihirika zaidi tunapoangalia muundo wa idadi ya watu nchini. Kwa mujibu wa matokeo ya Sensa ya Watu na Makazi ya Mwaka 2022, asilimia 34.5 ya Watanzania wote ni vijana (wenye umri wa miaka 15–35), huku kundi la watoto na vijana walio chini ya umri wa miaka 15 likiwa ni takriban asilimia 43. Hii ina maana kuwa zaidi ya robo tatu ya nguvu kazi na taifa la kesho lipo mikononi mwa kizazi kinachokua katikati ya dhoruba hii ya mmomonyoko wa maadili. Ikiwa kundi hili kubwa halitalindwa dhidi ya mmomonyoko huo, tunahatarisha kupoteza utambulisho wetu kama taifa katika miaka michache ijayo.

Sura hii inaelezea kwa kina hali halisi ya mmomonyoko wa maadili nchini, ikichambua sababu zinazochochea hali hiyo, viashiria vinavyoonesha kuporomoka kwa maadili, pamoja na athari zake pana kwa jamii, uchumi, utawala na utambulisho wa taifa. Aidha, sura hii inaweka msingi wa kuelewa ukubwa wa tatizo hili kwa kutazama takwimu hizi za idadi ya watu, ili kuwezesha uandaaji wa mikakati madhubuti na yenye uhalisia katika kukabiliana na hali hii kabla haijaleta madhara yasiyoweza kurekebishika.

## 2.1 KUPOROMOKA KWA MAADILI NCHINI

### 2. 1. 1 Sababu za Kuporomoka kwa Maadili Nchini

Kuporomoka kwa maadili katika taifa letu kunasababishwa na mchanganyiko wa sababu za kijamii, kiuchumi, kitamaduni na kiteknolojia. Sababu hizo ni pamoja na:

i. Kudharauliwa kwa mifumo ya asili: Kupuuza mila, desturi, na taratibu za malezi ya asili zilizokuwa zikidhibiti mwenendo wa wanajamii.

ii. Athari hasi za utandawazi: Ukuaji wa kasi wa teknolojia na mitandao ya kijamii umewafanya vijana kuiga mitindo ya maisha na tamaduni za kigeni zisizo na staha.

iii. Malezi holela: Ukosefu wa usimamizi thabiti katika ngazi ya familia na kutoa uhuru uliopitiliza kwa watoto na vijana.

iv. Imani potofu na ushirikina: Ongezeko la ukatili wa kingono (ubakaji na ulawiti) unaochochewa na imani za kishirikina kwa lengo la kutafuta mali.

v. Mabadiliko ya mifumo ya kiuchumi: Mpito kutoka mfumo wa kijamaa kuelekea ubepari umesababisha ari ya ubinafsi, ulafi, na tamaa ya mali kuzidi utu.

vi. Migogoro ya kifamilia: Utengano wa wazazi na kukosekana kwa uangalizi wa karibu kumesababisha watoto kukosa dira ya kimaadili.

vii. Umaskini: Hali duni ya maisha inayopelekea baadhi ya watu kujiingiza katika vitendo visivyo vya kimaadili ili kujikimu.



## 2.2 VIASHIRIA VYA KUPOROMOKA KWA MAADILI NCHINI

### 2.2.1 Mapenzi ya Jinsia Moja

Katika muktadha wa Tanzania, hoja ya kuporomoka kwa maadili hujadiliwa kwa kuzingatia historia ya kijamii, misingi ya kitamaduni, na Imani za dini katika maisha ya umma. Tanzania ni jamii inayotambulika kwa kuunganisha maadili ya mila za Kiafrika na misingi ya dini kuu, ambapo familia ya kijadi, ndoa ya jinsia tofauti, na malezi ya watoto yamekuwa nguzo za mshikamano wa kijamii. Maadili ya Tanzania yamejengwa juu ya dhana ya familia pana, heshima kwa wazee, uwajibikaji wa kijamii, na uendelezaji wa kizazi. Ndoa huchukuliwa si suala la watu wawili pekee bali ni taasisi ya kijamii inayounganisha koo na jamii kwa ujumla

Hata hivyo, katika siku za hivi karibuni, kumejitokeza mwelekeo usio wa kawaida wa baadhi ya watu kujihusisha na mapenzi ya jinsia moja, jambo ambalo ni kinyume kabisa na utamaduni, mila, na maadili ya Mtanzania. Hali hii imefikia hatua ya baadhi ya watu kutaka kuhalalisha ndoa kati ya mwanamume na mwanamume au mwanamke na mwanamke. Vitendo hivi havishambulii tu misingi ya kijamii, bali ni ukiukaji wa wazi wa misingi ya kisheria na kiroho inayoliongoza taifa.

Mbali na misingi ya kiutamaduni, kisheria, Tanzania haitambui muungano wowote wa jinsia moja kwa kuwa ni kinyume na sheria na tamaduni za nchi. Kwa mujibu wa Sheria ya Ndoa, Sura ya 29 Kifungu cha 9 (1), ndoa inatafsiriwa kuwa ni muungano wa hiari baina ya mwanamume na mwanamke kwa kusudi la kuishi pamoja kwa kudumu. Aidha, Sheria ya Kanuni ya Adhabu, Sura ya 16, inatamka bayana kuwa vitendo vya mapenzi ya jinsia moja au kinyume na maumbile, uwe kwa faragha au kwa makubaliano, ni kosa la jinai. Chini ya Kifungu cha 154 cha sheria hiyo, adhabu kwa kosa hili ni kifungo cha maisha gerezani, huku sheria ikilinda watoto dhidi ya udhalilishaji huu na kuweka adhabu kali kwa majaribio yoyote ya kutenda makosa hayo.

Sambamba na hayo, Serikali imeweka mifumo thabiti ya kudhibiti usambazaji wa tamaduni hizi kupitia teknolojia. Kanuni za Maudhui ya

Mtandaoni (EPOCA) za mwaka 2020 (G.N. Na. 538), zinakataza vikali uwekaji wa maudhui yanayoonesha au kuhamasisha mahusiano ya jinsia moja. Vilevile, Sheria ya Makosa ya Kimtandao, Sura ya 22, inazuia kutangaza au kusambaza machapisho ya ngono na matusi kupitia mifumo ya kompyuta na teknolojia nyinginezo, lengo likiwa ni kulinda jamii dhidi ya mmomonyoko wa kimaadili unaochochewa na utandawazi.

Mbali na misingi ya kisheria, vitabu vitakatifu vinachukulia vitendo hivi kama chukizo mbele za Mwenyezi Mungu. Biblia Takatifu (Mambo ya Walawi 20:13) inabainisha kuwa mwanamume akilala na mwanamume kama alalavyo na mwanamke, wote wawili wamefanya machukizo. Vivyo hivyo, Qur'an Tukufu (Surat Al-A'raf 7:80-81) inakemea vitendo hivyo kwa kuhoji: "Hakika nyinyi mnawaingilia wanaume kwa matamanio badala ya wanawake? Bali nyinyi ni watu wapindukia mipaka."

Kutokana na misingi hiyo imara ya kisheria, kiutamaduni, na kidini, ni dhahiri kuwa mapenzi na ndoa za jinsia moja hayana nafasi katika jamii ya Tanzania. Ni wajibu wa kila mdau, mzazi, na kiongozi kukemea na kupinga vikali vitendo hivi ili kulinda utu, heshima, na mustakabali wa Taifa letu kwa ajili ya vizazi vya sasa na vijavyo.

### 2.2.2 Matumizi ya Dawa za Kulevya na Pombe Kupita Kiasi

Matumizi ya dawa za kulevya na unywaji wa pombe kupita kiasi, hususan miongoni mwa vijana, yameendelea kuongezeka. Tabia hizi husababisha watu kupoteza uwezo wao wa kufikiri kwa busara na madhara yake husababisha wahusika kujiingiza katika vitendo viovu kama ubakaji, uzinzi, ulawiti, uporaji wa mali, lugha chafu na uharibifu wa amani ya jamii.

### 2.2.3 Mimba za Utotoni na Kutupa Watoto Wachanga

Vitendo vya kuwapa mimba wasichana walio chini ya umri wa miaka 18 vimeendelea kushamiri, jambo linalokatisha ndoto za elimu na maisha ya baadaye ya wasichana hao. Katika baadhi ya matukio, mimba hizo husababisha wasichana kuchukua maamuzi hatarishi ya kutupa watoto wachanga au kuchukua maamuzi ya kujiua. Hili ni uthibitisho wa kiwango cha juu cha kuporomoka kwa maadili na utu katika jamii.

### 2.2.4 Rushwa, Ufisadi, na Uhujumu Uchumi

Rushwa na ufisadi vinaendelea kuwa tatizo kubwa linaloathiri ustawi wa taifa. Vitendo vya kuomba, kutoa na kupokea rushwa, matumizi mabaya ya madaraka na kujilimbikizia mali isiyo halali vinahujumu haki, usawa na maendeleo ya nchi. Kwa mujibu wa ripoti ya TAKUKURU ya mwaka 2020/2021, jumla ya malalamiko 5,173 ya vitendo vya rushwa yaliripotiwa katika sekta mbalimbali, hali inayoonesha ukubwa wa tatizo hili.

### 2.2.5 Ujambazi, Wizi, na Uporaji wa Mali

Kumekuwepo na ongezeko la matukio ya ujambazi kwa kutumia silaha, wizi na uporaji wa mali za wananchi. Vitendo hivi ni dalili ya kuporomoka kwa misingi ya utu, heshima na udugu, ambavyo vinazaa kizazi katili na kinachosababisha maangamizi kwa jamii na taifa. Takwimu za Ofisi ya Taifa ya Takwimu (2024) zinaonesha kuongezeka kwa uhalifu katika baadhi ya wilaya, huku vijana na hata watoto wakihusishwa na makosa makubwa ya jinai. Katika orodha hiyo, wilaya ya Kinondoni inaongoza kwa kuwa na matukio 2678, Dodoma ikiwa na 772, Arusha 699 na Tanga 660. Kwa mujibu wa Jeshi la Magereza takwimu za mwaka 2025 zinaonesha kuwa watoto waliofungwa gerezani ni 120 kwa makosa mbalimbali yakiwemo wizi, kubaka, kulawiti, udhalilishaji wa kingono, uzururaji, na kuharibu mali.

### 2.2.6 Ukatili wa Kijinsia: Ubakaji, Ulawiti na Ukeketaji

Jamii inaendelea kushuhudia vitendo vya udhalilishaji wa kijinsia dhidi ya wanawake, watoto na hata wanaume. Ukeketaji, ubakaji na ulawiti ni vitendo vinavyokiuka haki za binadamu na maadili ya taifa. Takwimu za TDHS (2022/2023) zinaonesha kuwa kiwango cha kitaifa cha ukeketaji ni asilimia 8.2, huku mikoa ya Arusha na Manyara ikiongoza kwa asilimia 43%, ikifuatiwa na Mara kwa asilimia 28%.

Aidha, ukatili dhidi ya wanaume na unyanyasaji wa wafanyakazi wa ndani vimeongezeka. Mathalani, baadhi ya wanaume wanapigwa na wake zao na wanashindwa kuweka wazi matendo hayo. Vilevile kumekuwa na matukio mengi ya unyanyasaji kwa mabinti wa kazi majumbani. Pia, baadhi ya watoto wa kiume wanafanyiwa matendo ya ulawiti na watu wazima. Halikadhalika, kumekuwa na matukio ya ubakaji kwa watoto, vijana na

watu wazima.  Kwa mujibu wa Ofisi ya Taifa ya Takwimu (2024) kumekuwa na matukio ya ubakaji 4331 nchi nzima.

### 2.2.7 Mauaji ya Vikongwe na Watu Wenye Ulemavu wa Ngozi

Imani potofu za kishirikina zimeendelea kusababisha mauaji ya vikongwe na watu wenye ulemavu wa ngozi kwa madai ya kujipatia mali. Watu wenye umri mkubwa au vikongwe wakiwa na macho mekundu wamekuwa wakihisiwa kuwa wachawi na hivyo kufanyiwa vitendo vya kikatili ikiwemo kuchoma nyumba zao na kuwaua kwa kuwachoma moto au kuwakata kata kwa mapanga. Aidha, imejitokeza tabia ya baadhi ya watu kukata viungo vya watu wenye ulemavu wa ngozi (albino) kwa kudhani kuwa wangepata utajiri kwa kuwa na viungo vya mwili vya watu hao. Vitendo hivi ni vya kinyama, vinakiuka haki ya kuishi na ni kinyume na maadili, utamaduni na sheria za nchi.

### 2.2.8 Uvaaji Usio na Stara

Kumekuwa na ongezeko kubwa la uvaaji wa mtindo wa mavazi yasiyokuwa na stara miongoni mwa vijana na watu wazima. Uvaaji huo ni pamoja na nguo kuonesha sehemu za viungo vya mwili au nguo za ndani, nguo kubana sana, nguo kutobolewa au kuchanwa, nguo fupi sana au zenye mipasuo mirefu kupita juu ya magoti, nk. Uvaaji wa namna hii unashawishi watu kuingia katika vitendo viovu ikiwemo ukahaba, ubakaji, uasherati na uzinzi. Aidha, uvaaji wa mavazi ya utupu ni kielelezo cha kukosekana kwa maadili katika jamii.

### 2.2.9 Uongo na Udanganyifu

Tabia ya kusema uongo na kufanya udanganyifu imekuwa ya kawaida katika baadhi ya jamii na taasisi. Baadhi ya watu katika jamii wana tabia ya kusema uongo ili kujitetea au kutetea waliofanya makosa au kukiuka taratibu wasichukuliwe hatua stahiki. Aidha, wengine wanafanya vitendo vya udanganyifu ili kujenga mazingira ya kuaminiwa kwa kitu ambacho siyo kweli.

Ukweli umeanza kuonekana kama tishio badala ya msingi wa uadilifu, hali ambayo ni hatari kwa ustawi wa taifa. Mtu anayesema kweli anaonekana au

kutafsiriwa kuwa mtu hatari na anayechukiwa na watenda maovu. Badala yake watu wanaosema uongo wanakubalika zaidi.

### 2.2.10 Wizi na Uharibifu wa Miundombinu ya Maendeleo

Serikali imekuwa ikifanya kazi kubwa ya kujenga miundombinu kama vile barabara za lami mjini na vijijini; kuzalisha nguzo kwa ajili ya umeme; kujenga reli; kujenga majengo ya hospitali na shule na miundombinu mingine kwa lengo la kurahisisha utoaji wa huduma kwa wananchi na kukuza uchumi. Pamoja na jitihada hizo, wamejitokeza watu wasioitakia mema nchi yetu wanaoharibu miundombinu hiyo kwa kuiba vifaa na kuviuza kama vyuma chakavu. Baadhi ya watu wanang'oa miundombinu hiyo na wengine wanaiba vifaa vya ujenzi. Mambo kama haya yanaonesha kwamba hali ya maadili katika nchi yetu imeporomoka sana. Aidha takwimu zinaonesha ongezeko la makosa makubwa ya jinai. Mathalani, Takwimu za Jeshi la Polisi (2024/2025) zinaonesha kuwa katika kipindi cha kuanzia Julai 2024 hadi Aprili 2025, makosa makubwa ya jinai yaliyotolewa taarifa ni 40,022 katika vituo vya Polisi nchini. Aidha, taarifa hiyo inaonesha kuwa silaha 184 na risasi 429 zilikamatwa katika kipindi cha Julai 2024 hadi Aprili 2025. Pia, nyara za Serikali 2,092 zenye uzito wa kilogramu 23,459.75 zilikamatwa na watuhumiwa 769 walifikishwa mahakamani na kesi zao zipo katika hatua mbalimbali.

### 2.2.11 Makosa ya Usalama Barabarani

Makosa ya usalama barabarani yanayosababisha ajali, vifo na majeruhi yanatokana na uzembe, ulevi, mwendo kasi na kutokuzingatia sheria yanazidi kuongezeka. Takwimu zinaonesha kuwa katika kipindi cha mwezi Julai 2024 hadi Aprili, 2025, jumla ya matukio ya makosa ya usalama barabarani 1,322 yameripotiwa katika vituo vya Polisi. Aidha, katika kipindi hicho watu 1,275 walifariki kutokana na ajali za barabarani na watu 2,278 walijeruhiwa.

### 2.2.12 Ukahaba na Madanguro

Kumekuwapo na ongezeko la ukahaba na mandanguro nchini. Vitendo hivi ni viashiria vya mmomonyoko wa maadili kwa kuwa vinakinzana na maadili ya jamii yanayosisitiza heshima ya utu wa binadamu, udhibiti wa mienendo ya kingono, na uimara wa taasisi ya familia. Takwimu za shirika la

afya na ushirikiano wa kimataifa UNAIDS (2023) zinaonyesha kwamba, Tanzania ina makadirio ya takriban watu 155,450 ambao ni wafanyakazi wa ngono katika nchi nzima

### 2.2.13 Usafirishaji haramu wa binadamu

Kumekuwapo na ongezeko la Usafirishaji haramu wa binadamu, jambo ambalo ni moja ya viashiria vinavyoonyesha kwa uzito mmomonyoko wa maadili ndani ya jamii. Biashara hii haramu inakiuka kwa kiasi kikubwa haki za binadamu, heshima ya utu, na taratibu za kisheria za ulinzi wa maisha na shughuli za maendeleo. Kwa mujibu wa taarifa za utafiti uliofanywa na Mtandao wa Kupinga Usafirishaji Haramu wa Binadamu (Tanzania Relief Initiatives – TRI), zaidi ya matukio 2,400 ya usafirishaji haramu wa binadamu yaliripotiwa nchini Tanzania bara mwaka 2025, huku watoto na vijana wakiwa kundi kubwa zaidi la wahanga, na mikoa ya Dar es Salaam, Morogoro na Pwani ikibainika kuwa miongoni mwa maeneo yenye visa vingi zaidi.

## 2.3 ATHARI ZA KUPOROMOKA KWA MAADILI NCHINI


Kuporomoka kwa maadili ni tatizo mtambuka linaloathiri mnyororo mzima wa maisha ya mwanadamu na jamii kwa ujumla. Maadili kama uaminifu, uwajibikaji, heshima, na mshikamano ndiyo msingi mkuu wa maendeleo endelevu ya taifa lolote. Kudhoofika kwa misingi hii husababisha athari mbaya na pana katika nyanja za kijamii, kiutamaduni, kiuchumi, kisiasa, na kiteknolojia, hali inayorudisha nyuma jitihada za maendeleo ya taifa kwa ujumla.

### 2.3.1 Athari za Kijamii

Jamii ndiyo mwathirika mkuu wa mmomonyoko wa maadili kwani ndilo chimbuko la malezi ya binadamu. Kuporomoka huku husababisha kudhoofika kwa taasisi za msingi kama familia na mifumo ya elimu. Familia inapokosa misingi imara, malezi ya watoto huwa hafifu, jambo linalochochea ongezeko la talaka, migogoro ya ndoa, na kutelekezwa kwa watoto. Hali hii inatengeneza kizazi kinachokua bila malezi bora na mwelekeo sahihi wa maisha. Aidha, taasisi za elimu zinapokosa misingi ya

kimaadili, zinashindwa kujenga raia wenye nidhamu na uzalendo, na badala yake huzalisha wahitimu wenye ujuzi lakini wasio na uadilifu wa kuutumia ujuzi huo kwa manufaa ya umma.

Kudhoofika kwa taasisi za msingi ikiwemo familia, shule na jamii, kunadhihirishwa na kudorora kwa jitihada za jamii za kuwaandaa watoto na vijana wa kiume ili wawe wanajamii bora wanaowajibika kiuchumi na kijamii kuanzia ngazi ya familia mpaka ngazi ya jamii. Chamgamoto hiyo inadhihirishwa na kuongezeka kwa idadi ya wanaume na wanawake wasiowajibika kwa sababu ya kuogopa majukumu. Kwa mfano nchini Tanzania, katika matokeo ya sensa ya watu na makazi ya Mwaka 2022 yanabainisha kwamba, asilimia 61.5 ya wakazi wa mjini walio kwenye umri wa kuoa au kuolewa hawajaingia kwenye ndoa na asilmia 55.5 ya wakazi wa vijijini walio kwenye umri wa kuoa au kuolewa hawajaingia kwenye ndoa. Hali hiyo inaonesha uwepo wa idadi kubwa ya wanajamii wa kiume wasiowajibika kijamii kwa sababu suala la maamuzi ya kuingia kwenye ndoa kwa utamaduni wa Watanzania huanza na maamuzi ya wanaume kuchukua hatua kabla ya ridhaa wa wanawake.



Vilevile, ukosefu wa maadili unachochea ukatili na uhalifu uliokithiri, ikiwa ni pamoja na vitendo vya ubakaji, ulawiti, na mauaji ya kinyama, hali inayofanya hofu kutawala badala ya upendo. Heshima na adabu kwa wakubwa na mamlaka hutoweka, huku mshikamano wa kijamii ukidhoofika na nafasi yake kuchukuliwa na mashaka, migogoro ya kikabila, kidini, au kitabaka. Kisaikolojia, kuongezeka kwa msongo wa mawazo na kukata tamaa kwa mtu binafsi, hasa vijana, ambao hujikuta wakishindwa kutofautisha mema na mabaya katika kufanya maamuzi muhimu ya maisha yao.

### 2.3.2 Athari za Kiutamaduni

Kuporomoka kwa maadili huathiri kwa kiasi kikubwa utamaduni wa jamii. Jamii huanza kuiga tamaduni za kigeni zisizo na tija kutokana na kasi ya maendeleo ya sayansi na teknolojia. Hali hii husababisha kupotea kwa mila na desturi za asili, ambapo watu huanza kuona aibu kutumia tamaduni zao kama kusimulia hadithi za jadi, misemo, nyimbo za asili, majigambo, miviga, visakale na visasili. Vijana wengi huvutwa na tamaduni za kigeni kupitia filamu, muziki na mitindo ya mavazi, jambo linalozifanya tamaduni za kiasili kuonekana kuwa za kizamani.

Aidha, maendeleo ya teknolojia yamechangia kuenea kwa mavazi yasiyo na staha miongoni mwa vijana na hata watu wazima, huku mavazi ya asili yenye heshima na staha yakipuuzwa. Matokeo yake ni kudhoofika kwa utambulisho wa kitamaduni na kupotea kwa urithi wa jamii kwa vizazi vijavyo.

### 2.3.3 Athari za Kiuchumi

Uchumi wa taifa hutegemea sana jamii yenye wananchi wenye uwajibikaji wa hiari na ari ya kufanya kazi, wanaozalisha na kuwa chachu ya maendeleo ya kiuchumi katika taifa husika. Uadilifu ni rasilimali muhimu ndani ya taifa lolote ili kuhakikisha uendelevu na usalama wa rasilimali za nchi. Kuporomoka kwa maadili husababisha kushuka kwa uchumi kwani

maendeleo hayawezi kupatikana bila uadilifu na uwajibikaji. Taifa hupoteza nguvu kazi, mapato na uwapo wa matumizi makubwa ya Serikali katika kukabiliana na madhira yanayoletwa na mmomonyoko wa maadili.

Pia, nchi zenye viwango vya juu vya rushwa na ukosefu wa uadilifu hukosa mvuto wa uwekezaji kutokana na hofu ya udanganyifu na ukosefu wa usalama wa mitaji. Ufisadi na rushwa husababisha fedha za umma zinazopaswa kujenga miundombinu kama barabara, hospitali na shule kuishia mikononi mwa watu wachache. Hali hii hupunguza tija kazini, kwani watu hukosa bidii na ubunifu na badala yake hutafuta njia za mkato za kujipatia utajiri. Matokeo yake ni ongezeko la umasikini, usambazaji usio sawa wa rasilimali na kupungua kwa fursa za ajira.

### 2.3.4 Athari Kisiasa

Siasa safi na uongozi bora hutegemea kwa kiasi kikubwa misingi ya kimaadili ya viongozi na wananchi. Kuporomoka kwa maadili kunapoingia katika siasa, husababisha viongozi wasiokuwa waadilifu kushika madaraka, hali inayoongeza rushwa, ubadhirifu na kutojali maslahi ya wananchi. Matokeo yake ni kupungua kwa uaminifu wa wananchi kwa serikali, kuongezeka kwa migogoro ya kisiasa na kudhoofika kwa utawala wa sheria.

Aidha, mmomonyoko wa maadili huongeza unyanyasaji wa madaraka na kuharibu misingi ya demokrasia kwa kuchochea siasa za chuki, ubaguzi na uchochezi. Hali hii pia huharibu taswira ya nchi kimataifa na kudhoofisha mahusiano ya kidiplomasia pamoja na fursa za uwekezaji wa kimataifa.

### 2.3.5 Athari za Kiteknolojia

Ingawa teknolojia ni chombo muhimu cha maendeleo, matumizi yake hutegemea dira ya kimaadili ya mtumiaji. Teknolojia inapokosa mwongozo wa kimaadili, huleta mmomonyoko wa maadili katika jamii. Mfano halisi ni kuongezeka kwa uhalifu wa mtandaoni kama wizi wa fedha, utapeli na udukuzi wa mifumo ya usalama. Aidha, mitandao ya kijamii hutumiwa vibaya kusambaza picha zisizo na maadili, habari za uongo na lugha za matusi, hali inayoharibu saikolojia ya jamii, hususan watoto na vijana.

Zaidi ya hayo, matumizi mabaya ya teknolojia husababisha kudumaa kwa ubunifu chanya, kwani badala ya kutumika kutatua changamoto za kijamii kama kilimo na afya, teknolojia hutumika zaidi katika anasa na michezo ya kamari ya mtandaoni. Hali hii husababisha upotevu wa muda, rasilimali na nguvu kazi ya vijana, jambo linaloathiri maendeleo ya taifa kwa ujumla.

## 2.4 JITIHADA ZILIZOFANYIKA KATIKA KUKABILIANA NA MMOMONYOKO WA MAADILI NCHINI

Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kupitia wizara zenye dhamana ya utamaduni, pamoja na Wizara na taasisi mbalimbali, imekuwa ikichukua hatua madhubuti za kukabiliana na mmomonyoko wa maadili nchini. Mikakati hii inajumuisha uundaji wa miongozo ya kitaifa, utoaji wa elimu kupitia vyombo vya habari, makongamano ya kijamii, na uimarishaji wa mifumo ya malezi na makuzi. Lengo kuu ni kurejesha misingi ya uzalendo, uadilifu, na staha miongoni mwa Watanzania, hususani kizazi cha vijana na watoto.

### 2.4.1 Mwongozo wa Maadili na Utamaduni wa Mtanzania

Kufuatia kukithiri kwa vitendo vinavyoashiria mmomonyoko wa maadili, Serikali kupitia iliyokuwa Wizara ya Utamaduni, Sanaa na Michezo iliandaa Mwongozo Maalumu wa Maadili na Utamaduni wa Mtanzania toleo la kwanza mwaka 2022. Mwongozo huu uliandaliwa kwa lengo la kuwarejesha Watanzania katika misingi ya maadili ya taifa kwa kusisitiza umuhimu wa kuheshimu, kuthamini na kudumisha mila na desturi za asili. Mwongozo huu umeendelea kusambazwa katika taasisi za umma na binafsi ili kutoa fursa kwa wananchi kuufahamu na kuutekeleza katika maisha yao ya kila siku.

### 2.4.2 Mwongozo wa Uzingatiaji wa Maadili katika Kazi za Sanaa

Sekta ya sanaa imeonekana kuwa miongoni mwa sekta zinazoathiriwa kwa kiwango kikubwa na mmomonyoko wa maadili, hasa kupitia maudhui ya muziki, filamu na matumizi ya mitandao ya kijamii. Baadhi ya wasanii wamejihusisha na vitendo vinavyokiuka maadili kwa kuwasilisha kazi au picha zisizo na staha. Kutokana na hali hiyo, Serikali kupitia Baraza la Sanaa la Taifa (BASATA) iliandaa Mwongozo wa Uzingatiaji wa Maadili katika Kazi

za Sanaa uliozinduliwa mwaka 2023. Mwongozo huu unalenga kuhimiza uzingatiaji wa maadili miongoni mwa wasanii, kulinda heshima ya sanaa ya Tanzania na kuweka utaratibu wa kuchukua hatua dhidi ya uvunjifu wa maadili kwa mujibu wa sheria na kanuni zilizopo.

### 2.4.3 Kuendesha Makongamano ya Kukabiliana na Mmomonyoko wa Maadili

Serikali kupitia Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo imeendelea kuendesha makongamano na semina mbalimbali kama jukwaa la kitaifa la kujadili na kutafuta suluhisho la tatizo la mmomonyoko wa maadili. Makongamano hayo yamewahusisha wanafunzi wa vyuo vikuu, viongozi wa dini, vijana na wadau wa jamii katika maeneo mbalimbali nchini. Kupitia makongamano haya, jamii imekuwa ikielimishwa kuhusu athari za kuporomoka kwa maadili na wajibu wa kila mmoja katika kulinda misingi ya maadili ya taifa, huku Serikali ikiendelea kusisitiza kuwa makongamano hayo yataendelezwa ili kuongeza uelewa wa jamii.

### 2.4.4 Kutoa Elimu ya Maadili na Utamaduni Kupitia Vyombo vya Habari

Utoaji wa elimu ya maadili na utamaduni wa Mtanzania kupitia vyombo vya habari ni miongoni mwa mikakati muhimu ya Serikali. Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo imekuwa ikitumia redio na televisheni kuhamasisha jamii kulinda na kudumisha maadili. Katika kipindi cha mwaka 2021 hadi 2025, jumla ya vipindi vya redio 187 na vipindi vya televisheni 77 vimerushwa kwa lengo la kuhimiza kurejea katika misingi ya maadili. Utoaji wa elimu hii unaendelea kuwa endelevu kutokana na mchango wake mkubwa katika kufikia wananchi wengi kwa wakati mmoja.

### 2.4.5 Kujumuishwa kwa Somo la Maadili katika Mitaala Mipya ya Kufundishia kwa Shule za Msingi

Serikali kupitia Wizara yenye dhamana ya Elimu kwa kushirikiana na Wizara yenye dhamana ya Utamaduni, kupitia Taasisi ya Elimu Tanzania (TET), imejumuisha somo la Maadili katika mitaala mipya ya shule za msingi. Hatua hii inalenga kuwajengea wanafunzi msingi imara wa kimaadili tangu wakiwa wadogo, ili kukuza kizazi chenye heshima, nidhamu, uwajibikaji na uzalendo kwa taifa.

### 2.4.6 Programu ya Malezi kwa Vijana

Katika kukabiliana na changamoto za vijana wakati wa balehe, Serikali kupitia Wizara yenye dhamana ya Maendeleo ya Jamii inatekeleza Programu ya Malezi ya Vijana inayojulikana kama Furaha Teen. Programu hii inayotekelezwa kwa majaribio katika mikoa ya Songwe na Mbeya inalenga kuwawezesha wazazi kwa kuwapatia mbinu za kuwalea na kuwaongoza vijana wao ili kukabiliana na changamoto za kijamii, kisaikolojia na kiuchumi, na hivyo kuwakinga dhidi ya tabia na mienendo isiyofaa.

### 2.4.7 Urithishaji wa Elimu ya Maadili, Mila na Desturi Kutoka kwa Wazee

Serikali kupitia Wizara yenye dhamana ya Maendeleo ya Jamii imeratibu uanzishwaji wa mabaraza ya wazee 20,768 kuanzia ngazi ya kijiji hadi taifa. Mabaraza haya yanalenga kurithisha watoto na vijana maarifa, mila na desturi chanya pamoja na maadili ya jadi, hivyo kuchangia katika uhifadhi wa utamaduni na mshikamano wa kijamii.

### 2.4.8 Kampeni za Kijamii zinazolenga Kuhamasisha Ushiriki wa Jamii

Katika kukabiliana na kupinga vitendo vya ukatili, Serikali kwa kushirikiana na Wadau husussan Vikundi vya Shujaa wa Maendeleo na Ustawi wa Jamii (SMAUJATA), Sauti ya Watoto Tanzania (SAWATA), Malezi Bora Network na Leta Mabadiliko Chanya Ulipo (LEMACHU) vimeweza kuibua, kukemea na kutoa elimu kwa jamii kuhusu vitendo vya ukatili. Aidha, tangu kuanzishwa kwa kampeni hizo jumla ya matukio 799 yameripotiwa na kushughulikiwa.

### 2.4.9 Kuwajengea uwezo Wataalamu wa Sekta Mbalimbali

Serikali kupitia Wizara yenye dhamana ya Maendeleo ya Jamii imeendelea kuwajengea uwezo wataalamu wa sekta mbalimbali kuhusu masuala ya kukabiliana na vitendo vya ukatili. Katika kipindi cha kuanzia 2022 hadi 2025 makundi mbalimbali yalijengewa uwezo ikiwemo Polisi Jamii 4,542; Wasimamizi wa mashauri ya watoto wa kujitolea 15,255; Wahudumu wa Afya 10,534; Maofisa Ustawi wa Jamii 1,342; Walimu wa unasihi/malezi 13,636; na wasimamizi wa mashauri katika ngazi ya jamii 2,755. Mafunzo hayo yamewawezesha wataalamu kupata mbinu na maarifa ya kukabiliana na vitendo vinavyosababisha mmomonyoko wa maadili katika jamii.

### 2.4.10 Uanzishaji wa Vituo vya Kulelea Watoto Mchana na Huduma ya Malezi Mbadala

Serikali kupitia Wizara yenye dhamana ya Ustawi wa Jamii imeendelea kusajili na kufuatilia makao ya watoto na vituo vya kulelea watoto wadogo mchana. Hadi Novemba 2025, jumla ya makao ya watoto 404 na vituo vya kulelea watoto mchana 4,595 vilikuwa vimesajiliwa. Vituo hivi vinatoa huduma za malezi kwa kuzingatia misingi ya maadili, mila na desturi za Mtanzania.

## 2.5 CHANGAMOTO ZINAZOKABILI JITIHADA ZA KUKABILIANA NA MMOMONYOKO WA MAADILI

Pamoja na jitihada mbalimbali zinazotekelezwa na Serikali na wadau wa maendeleo, mapambano dhidi ya mmomonyoko wa maadili bado yanakabiliwa na changamoto kadhaa. Mojawapo ya changamoto hizo ni kutokuwekwa kwa suala la maadili kama ajenda ya kipaumbele cha juu katika baadhi ya mipango ya maendeleo ya Serikali na jamii kwa ujumla. Hali hii imepelekea utekelezaji wa programu za maadili kutokuwa na msukumo wa kutosha na, katika baadhi ya maeneo, kuachwa mikononi mwa taasisi chache bila ushiriki mpana wa jamii.

Changamoto nyingine ni utegemezi mkubwa kwa Serikali na vyombo vyake pekee katika masuala ya malezi na maadili, hali inayopunguza uwajibikaji wa familia na jamii kwa ujumla. Kutokuwepo kwa ushirikiano wa kijamii katika malezi ya watoto kumechangia kuibuka kwa malezi holela, ambapo watoto na vijana huathiriwa zaidi na makundi rika kuliko mwongozo wa wazazi au jamii. Athari za hali hii zinaonekana katika kuongezeka kwa mienendo isiyofaa miongoni mwa vijana, ikiwemo nidhamu duni na kuporomoka kwa heshima.

Aidha, matumizi holela ya vifaa vya kiteknolojia kama vile simu za mkononi, kompyuta na vishikwambi kwa watoto yamekuwa changamoto kubwa katika kudhibiti mmomonyoko wa maadili. Kutokuwepo kwa uangalizi wa karibu kutoka kwa wazazi na walezi kumeruhusu watoto kufikia maudhui yasiyofaa, huku athari za utandawazi zikichochea uigaji wa tamaduni za

kigeni zisizolingana na maadili ya Mtanzania. Vilevile, baadhi ya familia hushindwa kutoa elimu ya kutosha ya maadili kutokana na changamoto za kiuchumi, mabadiliko ya mitindo ya maisha na kupungua kwa mawasiliano ya karibu ndani ya familia.

Kwa upande mwingine, jamii kwa ujumla imeonekana kukosa uwajibikaji wa pamoja katika kusimamia malezi na maadili, hali inayodhoofisha dhana ya malezi ya kijamii ambayo hapo awali ilikuwa nguzo muhimu ya ujenzi wa tabia njema. Kukosekana kwa mifumo madhubuti ya kijamii ya kukemea mienendo mibaya kumeacha nafasi kwa vitendo vinavyoharibu maadili kuendelea kushamiri.

Ili kukabiliana na changamoto hizo na kunusuru jamii dhidi ya mmomonyoko wa maadili, ni muhimu kwa wazazi, familia na jamii kwa ujumla kuchukua jukumu la msingi katika malezi ya watoto na vijana. Ujenzi wa jamii yenye utu, nidhamu na bidii ya kufanya kazi unapaswa kuanzia katika ngazi ya familia kwa kujenga misingi imara ya maadili. Aidha, kunahitajika kuanzishwa kwa mifumo ya kuwatambua na kuwatuza watoto na vijana wanaoonesha mwenendo mzuri wa kimaadili ili kuwahamasisha na kuwafanya kuwa mfano bora kwa wenzao.

Vilevile, matendo yote yanayoharibu maadili yanapaswa kukemewa kwa uwazi na uthabiti ili kuimarisha uwajibikaji wa kijamii na kudhibiti mmomonyoko wa maadili nchini. Hatua hizi, zikitekelezwa kwa pamoja, zinaweza kuchangia kwa kiasi kikubwa katika kujenga jamii yenye maadili imara na yenye mwelekeo chanya wa maendeleo.

Jitihada za kukabiliana na mmomonyoko wa maadili zinakumbwa na changamoto mbalimbali ikiwemo kukosa kipaumbele kama ajenda muhimu katika mipango ya Serikali na Jamii; utegemezi kwa Serikali pekee na vyombo vyake; kutokuwepo kwa ushirikiano wa kijamii katika malezi ya watoto; malezi holela ya watoto na makundi rika ya vijana; matumizi holela ya vifaa vya kiteknolojia kama vile kompyuta, simu na vishikwambi kwa watoto; utandawazi; familia kutokutoa elimu ya kutosha ya maadili; na jamii kukosa uwajibikaji katika masuala ya malezi na maadili.

Ili kukabiliana na changamoto hizi na kunusuru jamii dhidi ya mmomonyoko wa maadili, wazazi na jamii kwa ujumla wana wajibu wa kuchukua jukumu la kuwalea watoto na vijana katika njia ambazo zitawezesha taifa kupata vijana wanaohitajika, wenye sifa za maadili yanayofaa na ujuzi wa maisha unaotakiwa ili wafanikiwe wao binafsi na jamii kwa ujumla. Aidha, msisitizo wa kujenga jamii yenye utu na inayopenda kufanya kazi lazima uanzie ngazi ya familia ili kujenga misingi imara na kulinda maadili ya jamii husika.

Pia, uanzishwe mfumo wa kuwatambua watoto na vijana wanaofanya vizuri katika maadili na kuwatuza ili kuwahamasisha kufanya vizuri zaidi na kuwa mfano (model) bora kwa watoto na vijana wengine. Halikadhalika, matendo yanayoharibu maadili yakemewe vikali ili kukabiliana na mmomonyoko wa maadili nchini.

# SURA YA TATU
# MALENGO YA MKAKATI

## 3 UTANGULIZI

Sura hii inaainisha lengo kuu na malengo mahsusi ya Mkakati huu wa Taifa. Aidha, sura inafafanua afua za kimkakati zitakazotekelezwa ili kujenga jamii yenye maadili, uzalendo, uwajibikaji, na mshikamano wa kitaifa kwa kuzingatia misingi ya kitamaduni na kisheria.

## 3.1 LENGO KUU

Kujenga jamii yenye maadili, uzalendo, uwajibikaji, na mshikamano wa kitaifa kwa kuimarisha misingi ya kimaadili inayozingatia mila na desturi katika ngazi ya familia, mifumo ya elimu, jamii, na mifumo ya utawala



## 3.2 MALENGO MAHSUSI

i. Kuimarisha wajibu wa wazazi, walezi, familia na jamii katika malezi na makuzi ya watoto na vijana;

ii. Kuimarisha mifumo ya ujifunzaji na ufundishaji wa elimu ya maadili ,uraia na uzalendo;

iii. Kusimamia uadilifu, uwajibikaji na uzingatiaji wa sheria, kanuni na miongozo ya utumishi wa umma na sekta binafsi;

iv. Kusimamia maudhui katika vyombo vya habari na mitandao ya kijamii ili kuhakikisha yanazingatia maadili ya Mtanzania;

v. Kuimarisha programu za kuwawezesha vijana kutambua, kuthamini na kuendeleza maadili na utamaduni wa Mtanzania;

vi. Kuimarisha ushirikiano kati ya Serikali, taasisi za dini na asasi za kiraia katika kakukabiliana na mmomonyoko wa maadili;

vii. Kuimarisha uwezo wa jamii katika kukabiliana na athari hasi za utandawazi na ushawishi wa tamaduni ngeni zinazopingana na misingi ya utu na maadili ya Mtanzania; na

viii. Kutambua mchango wa watu/taasisi kwenye uhamasishaji wa jamii, utoaji wa elimu ya maadili, pamoja na kuchukua hatua za kisheria na kijamii kwa ukiukwaji wa maadili.



## 3.3 AFUA ZA KIMKAKATI

| Na | Lengo mahususi | Afua za kimkakati |
|---|---|---|
| 1. | Kuimarisha wajibu wa wazazi, walezi, familia na jamii katika malezi na makuzi ya watoto na vijana. | (i) Kuandaa na kutekeleza programu za elimu ya malezi bora kwa wazazi na walezi kupitia ngazi za jamii, vituo vya afya, taasisi za dini na vyombo vya habari;<br>(ii) Kufanya mapitio ya miongozo ya malezi iliyopo na kuandaa mwongozo wa Kitaifa unaozingatia maadili na utamaduni wa Mtanzania;<br>(iii) Kuandaa na kutekeleza programu za kujenga uelewa wa Umma kuhusu maadili na utamaduni wa Mtanzania ;<br>(iv) Kujumuisha ajenda ya kukabiliana na mmomonyoko wa maadili kwenye mikutano yote ya ngazi ya Kijiji/mtaa hadi Taifa.<br>(v) Kuandaa na kutekeleza programu za huduma ya malezi mbadala kwa watoto ikijumuisha watoto walio katika mazingira hatarishi.<br>(vi) Kushirikisha viongozi wa kimila, kijamii na kidini katika kampeni za kupinga mila na desturi zisizofaa katika malezi na makuzi ya watoto na vijana . |
| 2. | Kuimarisha mifumo ya ujifunzaji na ufundishaji wa elimu ya maadili, uraia na uzalendo. | (i) Kufanya mapitio ya mitaala ya elimu ili kuimarisha maudhui ya maadili, uraia, na uzalendo;<br>(ii) Kuwajengea uwezo walimu na wasimamizi wa elimu kuhusu ufundishaji wa somo la maadili;<br>(iii) Kuanzisha program za mafunzo elekezi za kuwajengea uwezo walimu wapya na waliopo kazini katika stadi za malezi na makuzi ya watoto kwa kuzingatia haki, usawa wa kijinsia na mbinu chanya za malezi; |

| | | |
|---|---|---|
| | | (iv) Kuboresha miundombinu ya shule na mazingira ya kujifunzia kwa kuzingatia mahitaji ya ujinsia na rika;<br>(v) Kuimarisha klabu za ulinzi wa watoto zilizopo shuleni na vyuoni kwa kujumuisha masuala ya maadili, uzalendo na uraia katika shughuli za klabu husika;<br>(vi) Kuimarisha uwezo wa mamlaka za uthibiti ubora wa shule binafsi katika uzingatiwaji wa maadili na utamaduni wa Mtanzania; na<br>(vii) Kujumuisha kipengele cha upekuzi wa hali ya kimaadili katika kanuni na taratibu za ajira za walimu wa shule za umma na binafsi |
| 3. | Kusimamia uadilifu, uwajibikaji na uzingatiaji wa sheria, kanuni na miongozo ya utumishi wa umma na sekta binafsi. | (i) Kutoa mafunzo ya mara kwa mara kuhusu maadili ya kazi, uadilifu na uwajibikaji wa hiari kwa watumishi wa umma na sekta binafsi;<br>(ii) Kuimarisha utekelezaji wa kanuni za maadili ya utumishi wa umma na taaluma mbalimbali;<br>(iii) Kujumuisha kipengele cha upekuzi wa hali ya kimaadili katika utaratibu wa ajira za watumishi wa umma, sekta binafsi pamoja na teuzi za viongozi wa kisiasa.<br>(iv) Kuimarisha mifumo ya uwajibikaji, uwazi na utoaji taarifa zinahusu ukiukwaji wa maadili; na<br>(v) Kuimarisha taasisi simamizi za maadili. |
| 4. | Kusimamia maudhui katika vyombo vya habari na mitandao ya kijamii ili kuhakikisha yanazingatia maadili ya Mtanzania. | (i) Kuimarisha ushirikiano baina ya mamlaka na wadau muhimu wa uthibiti wa makosa ya kimtandao katika usimamizi wa sheria, kanuni na miongozo ya maudhui ya habari na mawasiliano ya mtandaoni;<br>(ii) Kufanya mapitio ya sheria na mifumo rekebu mara kwa mara ili kuhakikisha zinazingatia mabadiliko ya teknolojia na maadili yanazingatiwa katika uzalishaji na usambazaji wa maudhui; |

| | | |
|---|---|---|
| | | (iii) Kuratibu mafunzo na mazingativu kuhusu maadili kwa waandishi wa habari; na<br>(iv) Kuratibu mafunzo na mazingativu kuhusu maadili kwa wazalishaji na wasambazaji wa maudhui mitandaoni (digital contents creators) |
| 5. | Kuimarisha programu za kuwawezesha vijana kutambua , kuthamini na kuendeleza maadili na utamaduni wa Mtanzania | (i) Kutoa mafunzo ya stadi za maisha, na maadili kwa vijana wanaomaliza kidato cha sita kupitia program za Jeshi la Kujenga Taifa;<br>(ii) Kutoa mafunzo ya stadi za maisha, na maadili kwa vijana wanaomaliza elimu ya msingi, kidato cha nne na walio nje na mfumo rasmi wa elimu kupitia program za Chama cha Skauti na Kamandi ya Jeshi la Akiba;<br>(iii) Kuanzisha na kuboresha programu za mafunzo ya urekebu na ukuzaji maadili kwa vijana mahabusu waliopo katika magereza;<br>(iv) Kuimarisha vituo vya vijana, michezo, sanaa na ubunifu kama njia mbadala ya kuzuia mmomonyoko wa maadili; na<br>(v) Kujumuisha katika matukio makubwa yanayowavutia vijana programu za huduma ya unasihi na msaada wa kijamii kwa makundi yaliyo hatarini kukiuka maadili. |
| 6. | Kuimarisha ushirikiano kati ya Serikali, taasisi za dini na asasi za kiraia katika kakukabiliana na mmomonyoko wa maadili. | (i) Kuanzisha kikosi kazi cha kitaifa cha utekelezaji wa masuala ya maadili pamoja na Mkakati huu kwa kujumuisha wajumbe kutoka Wizara na Taasisi Wadau; na<br>(ii) Kuanzisha kalenda ya kudumu ya Mwaka ya Mkutano wa Kitaifa wa wadau wa Maadili nchini. |
| 7 | Kuimarisha uwezo wa jamii wa kukabiliana na athari hasi za utandawazi na ushawishi wa tamaduni ngeni zinazopingana na misingi ya utu na maadili ya Mtanzania | (i) Kutoa elimu ya maadili kwa wananchi hususani watoto na vijana kuhusu matumizi salama ya mitandao ya kijamii na teknolojia ya habari na mawasiliano;<br>(ii) Kuanzisha kampeni ya kuzalisha na kusambaza kitaifa na kimataifa maudhui chanya ya Tanzania na utamaduni wa Mtanzania; |

| | | |
|---|---|---|
| | | (iii) Kuteua watu wenye ushawishi katika jamii (mtandaoni, michezoni, kwenye uga wa imani n.k) kuwa mabalozi wa utamaduni wa Mtanzania wanaoshiriki kampeni ya kuwashawishi watoto na vijana wa Kitanzania kuthamini, kuenzi na kuona fahari ya utamaduni wao. |
| 8. | kutambua mchango wa watu/taasisi kwenye uhamasishaji wa jamii, utoaji wa elimu ya maadili, pamoja na kuchukua hatua za kisheria na kijamii kwa ukiukwaji wa maadili. | (i) Kuanzisha kampeni ya kutoa tuzo na zawadi kila baada ya miaka miwili kwa watu/taasisi zenye ushawishi kwenye jamii zilizoongoza katika kuhamasisha uwajibikaji wa jamii, kutoa elimu ya maadili, pamoja na kuchukua hatua za kisheria na kijamii kwa ukiukwaji wa maadili (wazalishaji maudhui, watu maarufu, shule, vyuo na vyombo vya habari) |

## 3.4 MIKAKATI YA UTEKELEZAJI KWA KILA LENGO MAHUSUSI

### Jedwali na. 2 Mkakati wa utekelezaji

| Mkakati | Shabaha | Kiashiria | Njia za uthibitishaji | Mhusika |
|---|---|---|---|---|
| **Lengo la Mahsusi 1**: Kuimarisha wajibu wa wazazi, walezi, familia na jamii katika malezi na makuzi ya watoto na vijana; | | | | |
| Kuanzisha na kuimarisha programu za kutoa elimu ya malezi na hamasa ya uwajibikaji kwa wazazi, walezi,familia na jamii katika malezi na makuzi ya watoto na vijana | Kuanzishwa kwa programu za utoaji elimu ya maadili na malezi pamoja na hamasa ya uwajibikaji wa wazazi, walezi, familia na jamii katika malezi na makuzi ya watoto na vijana ifikapo 2031 | Asilimia ya wazazi/walezi wanaoshiriki programu za elimu ya maadili na malezi bora<br><br>Idadi ya programu au kampeni za uelimishaji na hamasa ya uwajibikaji kuhusu urithishaji (malezi, makuzi, matumizi sahihi ya mtandao na teknolojia) na usimamizi wa maadili zilizotekelezwa | Taarifa za Utekelezaji | WMJWM<br>WHUSM<br>WEST<br>WMNN<br>WA<br>WMTH |
| Kufanya mapitio ya miongozo ya malezi iliyopo na kuandaa mwongozo wa Kitaifa unaozingatia maadili na utamaduni wa Mtanzania | Uwapo wa mwongozo wa kitaifa wa malezi na makuzi ya watoto unaozingatia maadili ifikapo 2029 | Mwongozo wa kitaifa wa malezi na makuzi ya watoto uliotolewa | Taarifa za Utekelezaji | WHUSM<br>WMJJWM<br>WEST<br>OWM-TAMISEMI |
| Kuandaa na kutekeleza programu za kujenga uelewa wa Umma kuhusu maadili na utamaduni wa Mtanzania | Uwapo wa kampeni za kutoa elimu ya maadili na utamaduni wa Mtanzania pamoja na kuhamasisha uwajibikaji wa hiari wa jamii ifikapo 2031 | Idadi ya programu/kampeni za kujenga uelewa na kuhamasisha uwajibikaji wa hiari kwa Umma zitakazoanzishwa | Taarifa za utekelezaji | WMJJWMM,<br>OWM TAMISEMI,<br>WEST<br>WMNN |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| Kuandaa na kutekeleza programu za kujenga uelewa wa Umma kuhusu maadili na utamaduni wa Mtanzania | Uwapo wa kampeni za kutoa elimu ya maadili na utamaduni wa Mtanzania pamoja na kuhamasisha uwajibikaji wa hiari wa jamii ifikapo 2031 | Idadi ya programu/kampeni za kujenga uelewa na kuhamasisha uwajibikaji wa hiari kwa Umma zitakazoanzishwa | Taarifa za utekelezaji | WMJJWMM,<br>OWM TAMISEMI,<br>WEST<br>WMNN |
| Kujumuisha ajenda ya kukabiliana na mmommonyoko wa maadili katika mikutano yote ya ngazi ya Kijiji/mtaa hadi Taifa | Mikutano yote ya kijamii, kiserikali na kidini katika ngazi zote (kijiji, kata,Wilaya, Mkoa, Taifa) ijumuishe ajenda ya maadili ifikapo 2029 | Idadi ya mikutano yenye ajenda ya maadili iliyofanyika | Taarifa za Utekelezaji | WHUSM<br>OWM- - TAMISEMI<br>WMNN-Msajili wa jumuiya |
| Kuandaa na kutekeleza programu za huduma ya malezi mbadala kwa watoto ikijumuisha watoto walio katika mazingira hatarishi | Program zitakazo boresha urithishwaji wa maadili kwa watoto walio katika vituo vya kulelea watoto wadogo mchana,ifikapo 2031.<br>Program zitakazo boresha urithishwaji wa maadili kwa watoto walio katika mazingira hatarishi na walio katika malezi mbadala<br>,ifikapo 2031. | Idadi ya programu za urithishwaji wa maadili kwa watoto zilizoanzishwa.<br>Idadi ya watoa huduma ya malezi mbadala waliojengewa uwezo wa kurithisha maadili kwa watoto. | Taarifa za utekelezaji | WMJJWMM,<br>OWM TAMISEMI,<br>WEST<br>WMNN-Msajili wa Jumuiya,<br>WHUSM |
| Kushirikisha viongozi wa kimila, kijamii na kidini katika kampeni za kupinga mila na desturi zisizofaa katika malezi na makuzi ya watoto na vijana . | Uwapo wa kampeni za kuongeza uwajibikaji wa viongozi wa kijamii, kimila, na kidini katika kuhamasisha urithishaji na usimamizi wa maadili kwa kuzingatia mila na desturi zinazofaa ifikapo 2031 | Idadi ya programu/kampeni za kuongeza ushiriki na uwajibikaji wa viongozi wa kijamii, kimila na kidini katika kuhamaisisha uwajibikaji wa jamii zitakazoanzishwa | Taarifa za utekelezaji | WMJJWMM,<br>OWM TAMISEMI,WEST<br>WMNN,<br>WHUSM |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| **Lengo la Mahsusi 2**: kuimarisha Mifumo ya ujifunzaji na ufundishaji wa elimu ya maadili ,uraia na uzalendo . | | | | |
| Kufanya mapitio ya mitaala ya elimu ili kuimarisha maudhui ya maadili, uraia, na uzalendo | Uwapo wa programu za kuimarisha mitaala ya somo la maadili na nyenzo za mafunzo kwa kuzingatia mahitaji ya wakati ifikapo 2031 | Idadi ya mitaala iliyofanyiwa mapitio | Taarifa za utekelezaji | WEST (TET)<br>WHUSM |
| Kuwajengea uwezo walimu na wasimamizi wa elimu kuhusu ufundishaji wa somo la maadili | Walimu na wasimamizi wa elimu kujengewa uwezo katika ufundishaji wa somo la maadili ifikapo 2031 | Asilimia ya walimu na wasimamizi wa elimu waliopata mafunzo ya ufundishaji wa somo la maadili na malezi jumuishi<br><br>Idadi ya mafunzo ya kuwajengea uwezo walimu na wasimamizi wa elimu yaliyotolewa | Taarifa za utekelezaji | OWM – TAMISEMI<br>WEST<br>WMJJWM<br>WHUSM |
| Kuanzisha programu za mafunzo elekezi za kuwajengea uwezo walimu wapya na waliopo kazini katika stadi za malezi na makuzi ya watoto kwa kuzingatia haki, usawa wa kijinsia na mbinu chanya za malezi | Uwapo wa programu za mafunzo elekezi za kuwajengea uwezo walimu wapya na waliopo kazini katika stadi za malezi na makuzi ya watoto kwa kuzingatia haki, usawa wa kijinsia na mbinu chanya za malezi ifikapo 2031 | Idadi ya programu za mafunzo elekezi za kuwajengea uwezo walimu wapya na waliopo kazini katika stadi za malezi na makuzi ya watoto | Taarifa za utekelezaji | OR-MUUB<br>OWM – TAMISEMI<br>WEST<br>WMJJWM<br>WHUSM |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| Kuimarisha klabu za ulinzi wa watoto zilizopo shuleni na vyuoni kwa kujumuisha masuala ya maadili, uzalendo na uraia katika shughuli za klabu husika. | Uwapo wa programu ya kuunganisha klabu zilizopo katika shule za msingi na sekondari zinazotekeleza shughuli zenye maudhui yanayolenga kurithisha na kusimamia maadili ya mtanzania. Na kujumuisha zaidi maudhui ya maadili ifikapo 2029 | Kutekelezwa kwa programu ya kujumuisha maudhui ya maadili na kuunganisha klabu zilizopo katika shule za msingi na sekondari zinazotekeleza shughuli zenye maudhui yanayolenga kurithisha na kusimamia maadili ya mtanzania. | Taarifa za utekelezaji | OWM – TAMISEMI<br>WEST<br>WMJJWM<br>WHUSM<br>WMNN-TAKUKURU |
| Kuimarisha uwezo wa mamlaka za uthibiti ubora wa shule binafsi katika uzingatiwaji wa maadili na utamaduni wa mtanzania | Uwapo wa programu ya kuimarisha Idara ya udhibiti ubora wa shule kikanuni, kibajeti na rasilimali watu ifikapo 2031 | Kutekelezwa kwa programu ya kuimarisha Idara ya udhibiti ubora wa shule kikanuni, kibajeti na rasilimali watu ifiakapo 2031 | Taarifa za utekelezaji | OWM – TAMISEMI<br>WEST |
| Kujumuisha kipengele cha upekuzi wa hali ya kimaadili katika kanuni na taratibu za ajira za walimu wa shule za umma na binafsi | Uwapo wa kanuni za ajira za walimu zinazojumuisha takwa la upekuzi wa hali ya kimaadili kwa walimu wanaoajiriwa kufundisha shule za umma na shule binafsi ifikapo 2028 | Kuimarishwa kwa kanuni za ajira za walimu kwa kujumuisha takwa la upekuzi wa hali ya kimaadili kwa walimu | Taarifa za utekelezaji | OR-MUUB<br>OWM – TAMISEMI |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| **Lengo la Mahsusi 3**: Kusimamia uadilifu, uwajibikaji na uzingatiaji wa sheria, kanuni na miongozo ya utumishi wa umma na sekta binafsi | | | | |
| Kutoa mafunzo ya mara kwa mara kuhusu maadili ya kazi, uadilifu na uwajibikaji kwa watumishi wa umma na sekta binafsi | Mafunzo kuhusu kanuni za maadili ya utumishi wa umma na taaluma mbalimbali kutolewa kwa watumishi wa umma na binafsi ifikapo 2031 | Idadi ya mafunzo ya maadili ya kazi yaliyotolewa | Taarifa za utekelezaji | OR - MUUB |
| Kuimarisha utekelezaji wa Kanuni za maadili ya utumishi wa umma na taaluma mbalimbali | Utekelezaji wa Kanuni za maadili ya utumishi wa umma na taaluma kuimarishwa ifikapo 2031 | Idadi ya matoleo ya Kanuni za maadili zilizoboreshwa | Taarifa za utekelezaji | OR - MUUB |
| Kujumuisha kipengele cha upekuzi wa hali ya kimaadili katika utaratibu wa ajira za watumishi wa umma, sekta binafsi pamoja na teuzi za viongozi wa kisiasa | Uwapo wa kanuni za ajira za walimu zinazojumuisha takwa la upekuzi wa hali ya kimaadili kwa watumishi wa umma na sekta binafsi wanaoajiriwa pamoja na teuzi za viongozi wa kisiasa ifikapo 2028 | Kuimarishwa kwa kanuni za ajira za watumishi wa umma na sekta binafsi pamoja na teuzi za viongozi wa kisiasa kwa kujumuisha takwa la upekuzi wa hali ya kimaadili | Taarifa za utekelezaji | OR-MUUB<br>OWM – TAMISEMI |
| Kuimarisha mifumo ya uwajibikaji, uwazi na utoaji taarifa zinahusu ukiukwaji wa maadili | Uwapo wa mifumo iliyoimarika ya uwajibikaji, uwazi na utoaji taarifa zinazohusu ukiukwaji wa maadili kwa watumishi na viongozi ifikapo 2031 | Kuimarika kwa mifumo iliyoimarika ya uwajibikaji, uwazi na utoaji taarifa zinazohusu ukiukwaji wa maadili kwa watumishi na viongozi wa umma, kijamii na kisiasa | Taarifa za utekelezaji | OR-MUUB |
| Kuongeza juhudi za kuzuia na kudhibiti rushwa, ikiwemo kuimarisha taasisi za usimamizi na nidhamu | Juhudi za kuzuia na kudhibiti vitendo vya rushwa kuongezeka ifikapo 2031 | Asilimia ya kupungua kwa makosa ya rushwa | Taarifa za utekelezaji | OR – IKULU<br>WMNN<br>OR - MUUB |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| **Lengo la Mahsusi 4**: Kusimamia maudhui katika vyombo vya habari na mitandao ya kijamii ili kuhakikisha yanazingatia maadili ya Mtanzania | | | | |
| Kuimarisha ushirikiano baina ya mamlaka na wadau muhimu wa uthibiti wa makosa ya kimtandao katika usimamizi wa sheria, kanuni na miongozo ya maudhui ya habari na mawasiliano ya mtandaoni | Uwapo wa afua pamoja baina ya mamlaka ya mawasiliano (TCRA), Jeshi la Polisi, mahakama na wadau wengine muhimu wa udhibiti wa makosa ya kimtandao ili kuongeza ufanisi katika usimamizi wa maudhui mtandaoni ifikapo 2031 | Kuimarika kwa ushirikiano wa kiutendaji baina ya mamlaka na wadau muhimu wa uthibiti wa makosa ya kimtandao katika usimamizi wa sheria, kanuni na miongozo ya maudhui | Taarifa za utekelezaji | WMTH-TCRA<br>WMNN<br>WKS<br>WHUSM |
| Kufanya mapitio ya sheria na mifumo rekebu mara kwa mara ili kuhakikisha zinazingatia mabadiliko ya teknolojia na maadili yanazingatiwa katika uzalishaji na usambazaji wa maudhui | Uwapo wa mapitio ya mara kwa mara ya sheria na mifumo rekebu ili kwenda sambamba na mabadiliko ya teknolojia na maadili na utamaduni wa Mtanzania unaendelea kulindwa ifikapo 2031 | Idadi ya mapitio ya sheria na mifumo rekebu yaliyofanyika | Taarifa za utekelezaji | WMTH -TCRA<br>WMNN<br>WKS |
| Kuratibu mafunzo na mazingativu kuhusu maadili kwa waandishi wa habari | Kuongeza uelewa na maarifa ya waandishi wa habari katika kudhibiti maudhui yaliyozingatia maadili kupitia mafunzo ifikapo 2031 | Idadi ya mafunzo yaliyofanyika<br>Idadi ya waandishi wa habari waliohudhuria mafunzo hayo | Taarifa za utekelezaji | WMTH<br>WHUSM |
| Kuratibu mafunzo na mazingativu kuhusu maadili kwa wazalishaji na wasambazaji wa maudhui mitandaoni (digital contents creators) | Kuongeza uelewa na maarifa ya wazalishaji na wasambazaji wa maudhui mitandaoni katika uzalishaji na usambazaji wa maudhui unaozingatia maadili kupitia mafunzo ifikapo 2031 | Idadi ya mafunzo yaliyofanyika<br>Idadi ya washiriki waliohudhuria mafunzo hayo | Taarifa za utekelezaji | WMTH<br>WHUSM |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| **Lengo la Mahsusi 5**: Kuimarisha programu za kuwawezesha vijana kutambua , kuthamini na kuendeleza maadili na utamaduni wa Mtanzania | | | | |
| Kutoa mafunzo ya stadi za maisha, na maadili kwa vijana wanaomaliza kidato cha sita kupitia programu za Jeshi la Kujenga Taifa | Kuimarishwa kwa programu za mafunzo ya Jeshi la Kujenga Taifa (JKT) zinazojumuisha utoaji elimu ya stadi za maisha, maadili na hamasa ya uzalendo kwa vijana wanaomaliza kidato cha 6 | Kuimarishwa kwa programmu na idadi ya vijana wanaoshiriki mafunzo | Taarifa za utekelezaji | OR-MV<br>OWM-TAMISEMI<br>WHUSM<br>WEST<br>WUJKT |
| Kutoa mafunzo ya stadi za maisha, na maadili kwa vijana wanaomaliza elimu ya msingi, kidato cha nne na walio nje na mfumo rasmi wa elimu kupitia programu za Chama cha Skauti, Kituo cha Urithi wa Ukombozi wa Bara la Afrika (ALHC) na Kamandi ya Jeshi la Akiba | Uwapo wa programu za mafunzo ya stadi za maisha, maadili na hamasa ya uzalendo kwa vijana wanaomaliza elimu ya msingi, kidato cha nne na walio nje ya mfumo rasmi wa elimu kupitia programu za Chama cha Skauti, Kituo cha Urithi wa Ukombozi wa Bara la Afrika (ALHC) na kamandi ya Jeshi la Akiba katika Halmashauri 184 nchini ifikapo 2031 | Idadi ya Halmashauri ambazo programu zimeanzishwa<br><br>Idadi ya vijana wanaoshiriki | Taarifa za utekelezaji | OR – MV<br>OWM-TAMISEMI<br>WEST<br>WUJKT<br>WHUSM |
| Kuanzisha na kuboresha programu za mafunzo ya urekebu na ukuzaji maadili kwa vijana mahabusu waliopo katika magereza | Uwapo wa programu za mafunzo ya urekebu na ukuzaji maadili kwa vijana mahabusu waliopo katika magereza yote nchini ifikapo 2031 | Idadi ya vijana walioshiriki mafunzo na programu za urekebu | Taarifa za utekelezaji | OR-MV<br>WMNN<br>WMJWM |
| Kuimarisha vituo vya vijana, michezo, sanaa na ubunifu kama njia mbadala ya kuzuia mmomonyoko wa maadili | Uwapo wa vituo vya vijana, michezo, sanaa na ubunifu katika Halmashauri 100 nchini ifikapo 2031 | Idadi vituo vilivyojengwa | Taarifa za utekelezaji | OR-MV<br>OWM-TAMISEMI<br>WHUSM |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| Kujumuisha katika matukio ya makubwa yanayowavutia vijana programu za huduma ya unasihi na msaada wa kijamii kwa makundi yaliyo hatarini kukiuka maadili | Uwapo wa matukio yanayowavutia vijana na yanayojumuisha huduma za unasihi kwa vijana ifikapo 2031 | Idadi ya matukio na vijana walipokea huduma za unasihi | Taarifa za utekelezaji | OR-MV<br>WHUSM<br>OWM-TAMISEMI |
| **Lengo la Mahsusi 6**: Kuimarisha ushirikiano kati ya Serikali, taasisi za dini na asasi za kiraia katika kakukabiliana na mmomonyoko wa maadili | | | | |
| Kuanzisha kikosi kazi cha kitaifa cha utekelezaji wa masuala ya maadili pamoja na Mkakati huu kwa kujumuisha wajumbe kutoka Wizara na Taasisi Wadau | Uwapo wa kamati za uratibu wa masuala ya maadili kuanzia ngazi ya kijiji mpaka Taifa ifikapo 2028 | Kuanzishwa kwa kamati katika ngazi zote<br>Kujumuishwa kwa shughuli za kamati husika katika kalenda, mipango na bajeti za Wizara na Taasisi wadau , Sekretarieti za Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa zote Nchini | Taarifa za Utekelezaji | WHUSM<br>OWM-TAMISEMI<br>Wizara na Taasisi wadau wa Mkakati<br>Sekretarieti za Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa |
| Kuanzisha kalenda ya kudumu ya Mwaka ya Mkutano wa Kitaifa wa wadau wa Maadili nchini | Uwapo wa kalenda ya kudumu ya Mkutano wa Mwaka wa wadau wa maadili nchini ifikapo 2027 | Kufanyika kwa Mkutano wa Mwaka wa Wadau wa Maadili Nchini | Taarifa za Utekelezaji | WHUSM |
| **Lengo la Mahsusi 7**: Kuimarisha uwezo wa jamii wa kukabiliana na athari hasi za utandawazi na ushawishi wa tamaduni ngeni zinazopingana na misingi ya utu na maadili ya Mtanzania | | | | |
| Kutoa elimu ya maadili kwa wananchi hususani watoto na vijana kuhusu matumizi salama ya mitandao ya kijamii na teknolojia ya habari na mawasiliano | Uwapo wa kampeni ya matumizi salama ya mitandao ya kijamii na teknolojia ya habari na mawasiliano kwa jamii ifikapo 2031 | Kufanyika kwa kampeni na idadi ya wananchi waliofikiwa | Taarifa za Utekelezaji | OR-MV<br>WHUSM<br>OWM-TAMISEMI<br>Sekretarieti za Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| Kuanzisha kampeni ya kuzalisha na kusambaza kitaifa na kimataifa maudhui chanya ya Tanzania na utamaduni wa Mtanzania | Uwapo wa kampeni ya kuzalisha na kusambaza kitaifa na kimataifa maudhui chanya ya Tanzania na utamaduni wa Mtanzania ifikapo 2029 | Kutekelezwa kwa kampeni | Taarifa za Utekelezaji | OR-MV<br>WHUSM |
| Kuteua watu wenye ushawishi katika jamii (mtandaoni, michezoni, kwenye uga wa imani n.k) kuwa mabalozi wa Maadili na utamaduni wa Mtanzania wanaoshiriki kampeni ya kuwashawishi watoto na vijana wa Kitanzania kuthamini, kuenzi na kuona fahari ya utamaduni wao | Uwapo wa Mabalozi wa Maadili na Utamaduni wa Mtanzania ifikapo 2028 | Kuteuliwa kwa Mabalozi<br>Kutekelezwa kwa shughuli za Mabalozi | Taarifa za Utekelezaji | WHUSM |
| **Lengo Mahsusu 8**: Kutambua mchango wa watu/taasisi kwenye uhamasishaji wa jamii, utoaj wa elimu ya maadili, pamoja na kuchukua hatua za kisheria na kijamii kwa ukiukwaji wa maadili | | | | |
| Kuanzisha kampeni ya kutoa tuzo na zawadi kila baada ya miaka miwili kwa watu/taasisi zenye ushawishi kwenye jamii zilizoongoza katika kuhamasisha uwajibikaji wa jamii, kutoa elimu ya maadili, pamoja na kuchukua hatua za kisheria na kijamii kwa ukiukwaji wa maadili | Uwapo wa kampeni ya kutoa tuzo na zawadi kila baada ya miaka miwili kwa watu/taasisi zenye ushawishi kwenye jamii (wazalishaji maudhui, watu maarufu, viongozi wa dini, kijamii na kisiasa, shule, vyuo na vyombo vya habari) zilizongooza katika kuhamasisha uwajibikaji wa jamii, kutoa elimu ya maadili, pamoja na kuchukua hatua za kisheria na kijamii kwa ukiukwaji wa maadili | Kutekelezwa kwa kampeni | Taarifa za Utekelezaji | WHUSM |

# SURA YA NNE
# MAJUKUMU YA WADAU

## 4 UTANGULIZI

Ufanisi wa Mkakati huu unategemea ushirikiano wa karibu na uratibu makini kati ya sekta mbalimbali. Wadau wakuu wamegawanywa kulingana na nafasi zao katika jamii, mamlaka yao kisheria, na uwezo wao wa kushawishi mabadiliko ya tabia ili kuhakikisha kila taasisi inawajibika katika ujenzi wa jamii yenye maadili. Mgawanyo wa majukumu utakuwa kama ifuatavyo:

## 4.1 MGAWANYO WA MAJUKUMU YA WIZARA NA WADAU MBALIMBALI KATIKA UTEKELEZAJI WA MKAKATI

### Jedwali na. 3 Kazi na Majukumu ya wadu mbalimbali katika utekelezaji wa Mkakati

| Na. | WIZARA | MAJUKUMU |
|---|---|---|
| 1. | Ofisi ya Waziri Mkuu - Sera, Bunge,Uratibu na Wenye Ulemavu | (i) Kuratibu utekelezaji wa Mkakati<br>(ii) Kuwaunganisha Wizara na Taasisi wadau katika utekelezaji wa Mkakati; na<br>(iii) Kuweka mazingira wezeshi yanayohusisha maadili kwa watu wenye mahitaji maalum. |
| 2. | Ofisi ya Waziri Mkuu-TAMISEMI | (i) Kuratibu utekelezaji wa Mkakati katika ngazi za Mikoa, Halmashauri, Kata na Vijiji/Mtaa;<br>(ii) Kusimamia ujumuishaji wa afua za kukabiliana na mmomonyoko kama zilivyobainishwa katika Mkakati katika mipango na bajeti za Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa;<br>(iii) Kupokea na kuunganisha taarifa za utekelezaji wa Mkakati kutoka Mikoani na Halmashauri na kuziwasilisha kwa Sekretarieti ya Taifa ya Uratibu wa Mkakati;<br>(iv) Kuboresha miundombinu ya shule na mazingira ya kujifunzia kwa kuzingatia mahitaji ya ujinsia na rika; |

| | | |
|---|---|---|
| | | (v) Kuimarisha klabu za ulinzi wa watoto zilizopo shuleni kwa kujumuisha masuala ya maadili, uzalendo na uraia katika shughuli za klabu husika;<br>(vi) Kujumuisha kipengele cha upekuzi wa hali ya kimaadili katika kanuni na taratibu za ajira za walimu wa shule za umma na binafsi;<br>(vii) Kuwezesha uandaaji wa sheria ndogo zinazoiwezesha mamlaka za Serikali za Mitaa na jamii kukabiliana na mmomonyoko wa maadili;<br>(viii) Kuteua mmoja wa waratibu watano wa Mkakati na kugharamia shughuli za mratibu huyo ikiwemo na kumpatia ofisi na gari kwa ajili ya utekelezaji wa shughuli za kila siku za Mkakati (kama ilivyobainishwa katika sehemu ya 5.2.4 ya Mkakati); na<br>(ix) Kufanya na kushiriki ziara za pamoja za usimamizi, ufuatiliaji, tathmini na mafunzo yanayohusu utekelezaji wa Mkakati katika Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa. |
| 3. | Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora | (i) Kuratibu utoaji elimu ya maadili na hamasa ya uwajibikaji kwa watumishi wa umma;<br>(ii) Kujumuisha kipengele cha upekuzi wa hali ya kimaadili katika utaratibu wa ajira za watumishi wa umma, sekta binafsi pamoja na teuzi za viongozi katika utumishi wa umma na viongozi wa kisiasa;<br>(iii) Kuimarisha mifumo ya uwajibikaji, uwazi na utoaji taarifa zinahusu ukiukwaji wa maadili; na<br>(iv) Kuimarisha taasisi simamizi za maadili ikiwemo kusimamia mchakato wa kuanzisha idara maalumu inayoratibu masuala ya Maadili ya Taifa katika ngazi ya Wizara yenye dhamana na Utamaduni, Uzalendo na Utaifa. |
| 4. | Ofisi ya Rais-Maendeleo ya Vijana | (i) Kujumuisha afua za kimkakati za utoaji elimu ya maadili na hamasa ya uwajibiakaji wa jamii kwenye Mbio za Mwenge wa Uhuru;<br>(ii) Kushirikiana na wadau wengine kuratibu shughuli mahususi za utoaji elimu ya maadili na hamasa ya uwajibikaji kwa vijana;<br>(iii) Kuanzisha kampeni ya vijana kuhusu fursa na matumizi salama ya mitandao ya kijami yanayoendana na maadili ya Mtanzania;<br>(iv) Kuanzisha jukwaa la kitaifa la wadau wa malezi na maadili ya vijana; na<br>(v) Kuwaelimisha vijana kuishi kwa kuzingatia na kufuata mila na desturi za maadili ya Kitanzania. |

| | | |
|---|---|---|
| 5. | Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo | (i) Kusimamia na kutoa msaada wa kitaalam katika utekelezaji wa Mkakati;<br>(ii) Kuratibu kampeni za kitaifa za maadili za kutoa elimu ya maadili na hamasa ya uwajibikaji wa jamii katika kukabiliana na mmomonyoko wa maadili kupitia matukio ya sekta mbalimbali, vyombo vya habari na mitandao ya kijamii;<br>(iii) Kuratibu mafunzo na mazingativu kuhusu maadili kwa waandishi wa habari pamoja na wazalishaji na wasambazaji wa maudhui mitandaoni (digital contents creators)<br>(iv) Kuanzisha kampeni ya kuzalisha na kusambaza kitaifa na kimataifa maudhui chanya ya Tanzania na utamaduni wa Mtanzania;<br>(v) Kuteua watu wenye ushawishi katika jamii (mtandaoni, michezoni, kwenye uga wa imani n.k) kuwa mabalozi wa utamaduni wa Mtanzania wanaoshiriki kampeni ya kuwashawishi watoto na vijana wa Kitanzania kuthamini, kuenzi na kuona fahari ya utamaduni wao.<br>(vi) Kuanzisha na kuratibu kampeni ya kutoa tuzo na zawadi kila baada ya miaka miwili kwa watu/taasisi zenye ushawishi kwenye jamii zilizoongoza katika kuhamasisha uwajibikaji wa jamii, kutoa elimu ya maadili, pamoja na kuchukua hatua za kisheria na kijamii kwa ukiukwaji wa maadili. Walengwa ni pamoja na wazalishaji maudhui, watu binafsi, shule, vyuo na vyombo vya habari;<br>(vii) Kufanya midahalo na mijadala ya kitaifa kuhusu athari za mmomonyoko wa maadili na mbinu za kukabiliana nazo;<br>(viii) Kuratibu Mkutano wa Mwaka wa Kitaifa wa Wadau wa Maadili nchini kwa kila mwaka;<br>(ix) Kutoa miongozo na ufafanuzi kuhusu maadili ya Taifa;<br>(x) Kudhibiti maudhui ya vyombo vya Habari, filamu, muziki na sanaa ili kuhakikisha hayakiuki maadili ya Mtanzania;<br>(xi) Kutoa mapendekezo ya sera, sheria na mikakati inayolenga kuimarisha maadili katika sekta mbalimbali nchini; na<br>(xii) Kufanya ufuatiliaji na tathimini ya utekelezaji wa Mkakati. |
| 6. | Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum | (i) Kuandaa na kutekeleza programu za elimu ya malezi bora kwa wazazi na walezi kupitia programu ya MTAKUWWA, kampeni za vyombo vya habari, na shughuli mbalimbali za wadau ikiwemo Taasisi za Dini, Taasisi za Elimu na Mafunzo (Makongamano shuleni na vyuoni na vikao vya wazazi shuleni); |

| | | |
|---|---|---|
| | | (ii) Kuratibu ufanyaji wa mapitio ya miongozo ya malezi iliyopo na kuandaa mwongozo wa Kitaifa wa unaozingatia maadili na utamaduni wa Mtanzania;<br>(iii) Kuandaa na kutekeleza programu za huduma ya malezi mbadala kwa watoto ikijumuisha watoto walio katika mazingira hatarishi;<br>(iv) Kushirikisha viongozi wa kimila, kijamii na kidini katika kampeni za kupinga mila na desturi zisizofaa katika malezi na makuzi ya watoto na vijana;<br>(v) Kujumuisha katika matukio makubwa yanayowavutia vijana programu za huduma ya unasihi na msaada wa kijamii kwa makundi yaliyo hatarini kukiuka maadili;<br>(vi) Kuteua mmoja wa waratibu watano wa Mkakati na kugharamia shughuli za mratibu huyo ikiwemo na kumpatia ofisi na gari kwa ajili ya utekelezaji wa shughuli za kila siku za mkakati (kama ilivyobainishwa katika sehemu ya 5.2.4 ya Mkakati); na<br>(vii) Kushirikiana na wadau wa maadili kutekeleza afua zote za kimkakati zinazohusiana moja kwa moja na wizara na zinazowahusu wadau wengine. |
| 7. | Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia | (i) Kufanya mapitio ya mitaala ya elimu ili kuimarisha maudhui ya maadili, uraia, na uzalendo;<br>(ii) Kuwajengea uwezo walimu na wasimamizi wa elimu kuhusu ufundishaji wa somo la maadili;<br>(iii) Kuanzisha programu za mafunzo elekezi za kuwajengea uwezo walimu wapya na waliopo kazini katika stadi za malezi na makuzi ya watoto kwa kuzingatia haki, usawa wa kijinsia na mbinu chanya za malezi;<br>(iv) Kuimarisha klabu na vyama vya kitaaluma na kijamii vilivyopo vyuoni kwa kujumuisha masuala ya maadili, uzalendo na uraia katika shughuli za klabu husika;<br>(v) Kuimarisha uwezo wa mamlaka za uthibiti ubora wa shule binafsi katika uzingatiwaji wa maadili na utamaduni wa Mtanzania;<br>(vi) Kuteua mmoja wa waratibu watano wa Mkakati na kugharamia shughuli za mratibu huyo ikiwemo na kumpatia ofisi na gari kwa ajili ya utekelezaji wa shughuli za kila siku za Mkakati (kama ilivyobainishwa katika sehemu ya 5.2.4 ya Mkakati); na<br>(vii) Kujumuisha kipengele cha upekuzi wa hali ya kimaadili katika kanuni na taratibu za ajira za walimu wa shule za umma na binafsi. |

| | | |
|---|---|---|
| 8. | Wizara ya Katiba na Sheria | (i) Kuhakikisha mifumo ya kisheria inalinda maadili na kushughulikia makosa yanayochochea mmomonyoko wa maadili;<br>(ii) Kusimamia misingi ya utawala wa sheria kama nguzo ya maadili nchini;<br>(iii) Kuhakikisha adhabu kwa makosa ya kimaadili zinatekelezwa ipasavyo;<br>(iv) Kuratibu utoaji wa msaada wa kitaalam kwa wadau wa Mkakati ikiwemo Mamlaka za Serikali za Mitaa zenye wajibu wa msingi wa kuandaa na kusimamia utekelezaji wa sheria ndogo zinazoziwezesha Mamlaka hizo na Jamii kukabiliana na mmomonyoko wa maadili kwa ufanisi; na<br>(v) Kushiriki katika utoaji mafunzo kwa kamati na vikosi kazi vinavyohusiana na utekelezaji wa Mkakati kuanzia ngazi ya Kijiji/Mtaa hadi ngazi ya Taifa. |
| 9. | Wizara ya Mambo ya ndani ya Nchi | (i) Kusimamia vyombo vya dola, idara ya uhamiaji na mamlaka ya vitambulisho vya taifa kutenda haki kwa kuzingatia maadili na utu;<br>(ii) Kuimarisha na kuwezesha programu za Idara ya Polisi Jamii ili iongeze ufanisi katika operesheni za kukabiliana na ukiukwaji wa maadili ya jamii;<br>(iii) Kuimarisha upelelezi wa mashauri yanayohusu vitendo vilivyosababishwa na mmomonyoko wa maadili;<br>(iv) Kuanzisha operesheni za mara kwa mara za kukabiliana na vitendo vya mmomonyoko wa maadili vinavyofanyika uwandani na mtandaoni;<br>(v) Kuimarisha Idara ya Jeshi la Polisi linalohusika na kukabiliana na uhalifu na makosa ya kimtandao;<br>(vi) Kuanzisha na kuboresha programu za mafunzo ya urekebu na ukuzaji maadili kwa vijana mahabusu waliopo katika magereza<br>(vii) Kuimarisha mfumo wa ukasanyaji takwimu za uhalifu unaohusiana moja kwa moja na ukiukwaji wa maadili ya jamii;<br>(viii) Kuhakikisha sheria zinazolinda maadili ya jamii zinatekelezwa; na<br>(ix) Kutoa mafunzo ya maadili kwa askari na maafisa mbalimbali wa vyombo vya dola. |

| | | |
|---|---|---|
| 10. | Wizara ya Afya | (i) Kuandaa na kutekeleza programu za elimu ya malezi bora kwa wazazi na walezi kupitia huduma zitolewazo katika vituo vya mama na mtoto katika zahanati na vituo vya afya;<br>(ii) Kuanzisha programu za mafunzo elekezi ya kuwajengea uwezo watumishi wa afya wapya na waliopo kazini wanaohudumia wazazi na walezi katika stadi za malezi na makuzi ya watoto kwa kuzingatia haki, usawa wa kijinsia na mbinu chanya za malezi; na<br>(iii) Kuanzisha kampeni za kitaifa za afya ya akili kwa lengo la kukabiliana na mmomonyoko wa maadili. |
| 11. | Wizara ya Mawasiliano na Teknolojia ya Habari | (i) Kuimarisha ushirikiano baina ya mamlaka na wadau muhimu wa uthibiti wa makosa ya kimtandao katika usimamizi wa sheria, kanuni na miongozo ya maudhui ya habari na mawasiliano ya mtandaoni;<br>(ii) Kufanya mapitio ya sheria na mifumo rekebu mara kwa mara ili kuhakikisha zinazingatia mabadiliko ya teknolojia na maadili yanazingatiwa katika uzalishaji na usambazaji wa maudhui;<br>(iii) Kuanzisha kampeni za matumizi bora ya mitandao ya kijamii na teknolojia kwa kuzingatia maadili ya Kitanzania;<br>(iv) Kuweka mifumo ya ulinzi wa mtoto mitandaoni; na<br>(v) Kuweka mifumo ya ufuatiliaji wa shughuli za kutuma na kupokea maudhui katika mitandao ya kijamii. |
| 12. | Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa | (i) Kutoa mafunzo ya stadi za maisha, na maadili kwa vijana wanaomaliza kidato cha sita kupitia programu za Jeshi la Kujenga Taifa; na<br>(ii) Kutoa mafunzo ya stadi za maisha, na maadili kwa vijana wanaomaliza elimu ya msingi, kidato cha nne na walio nje na mfumo rasmi wa elimu kupitia programu za Chama cha Skauti na Kamandi ya Jeshi la Akiba. |
| 13. | Sekta Binafsi | (i) Kuimarisha ushirikiano kati ya sekta za umma katika utekelezaji wa afua za kimkakati zinazohusiana na mapambano dhidi ya mmomonyoko wa maadili nchini;<br>(ii) Kufadhili utekelezaji wa Mkakati<br>(iii) Kujumuisha elimu ya athari za mmomonyoko wa maadili na hatua za udhibiti katika mipango kazi, bajeti na utekelezaji wa shughuli zote za kisekta; na<br>(iv) Kuwekeza katika miradi ya kijamii kama vile elimu, utamaduni, sanaa na michezo inayojenga maadili ya vijana. |

| | | |
|---|---|---|
| 14. | Asasi za Kiraia (Taasisi za Kidini,Taasisi za Kijamii, Vyama vya Wafanyakazi, Viongozi wa Kimila na Vyama vya Siasa) | (i) Kuanzisha, kushiriki na kutekeleza programu za kutoa hamasa ya uwajibikaji na mabadiliko kwa jamii;<br>(ii) Kuratibu programu za kuimarisha taasisi ya familia, hamasa ya vijana wa kiume kuoa na vijana wakike kuolewa na kuthamini ndoa;<br>(iii) Kutoa huduma ya elimu kwa viwango na mikakati inayoandaa watoto na vijana kuwa wanajamii wanaowajibika kijamii na kiuchumi;<br>(iv) Kushiriki katika mijadala na mazungumzo yanayojumuisha wadau wote kuhusu utekelezaji wa Mkakati na kuimarisha jitihada za kukabiliana na mmomonyoko wa maadili;<br>(v) Kushiriki na kuwezesha kampeni za maadili ya taifa na utawala bora zinazoandaliwa na kuratibiwa na wadau mbalimbali katika ngazi ya jamii ikiwemo Mamlaka za Serikali za Mitaa;<br>(vi) Kutoa mafundisho ya kiroho kwa makundi yote kwenye jamii ambayo yatasaidia kudhibiti mmomonyoko wa maadili;<br>(vii) Kuhamasisha ujumuishaji wa ajenda ya kukabiliana na mmomonyoko wa maadili katika mikutano yote na matukio ya Taasisi za Dini na Kijamii;<br>(viii) Kuishauri Serikali kuhusu masuala ya maadili; na<br>(ix) Kuhamasisha Asasi za Kiraia kutenga bajeti zinazojumuisha programu za masuala ya maadili. |
| 15. | Vyombo Vya Habari | (i) Kurusha na kuchapisha vipindi, makala na habari zinazohamasisha maadili kama uadilifu, uzalendo, haki, heshima na uwajibikaji;<br>(ii) Kutoa elimu ya maadili ya taifa kwa makundi yote ya jamii;<br>(iii) Kuripoti habari kwa ukweli, uaminifu, uwiano na bila upendeleo<br>(iv) Kuepuka uchochezi, lugha ya matusi, habari za uongo na maudhui yanayokiuka maadili ya jamii;<br>(v) Kukuza utamaduni wa Kitanzania, mila na desturi zenye maadili;<br>(vi) Kupinga vitendo vya ukiukwaji wa maadili ya jamii kupitia maudhui ya kimkakati yasiyodhalilisha utu wa binadamu;<br>(vii) Kufichua vitendo vya rushwa, uonevu na ukiukwaji wa maadili kwa njia ya kitaaluma na kimaadili;<br>(viii) Kuhamasisha viongozi na wananchi kuwajibika kwa matendo yao;<br>(ix) Kushirikiana na taasisi za umma na binafsi katika kampeni za kitaifa za maadili; |

| | | |
|---|---|---|
| | | (x) Kusaidia utekelezaji wa sera, sheria na mikakati ya maadili ya taifa; na<br>(xi) Kuelimisha umma juu ya matumizi salama na yenye maadili ya mitandao ya kijamii. |
| 16. | Taasisi Za Elimu Ya Juu | (i) Kutoa elimu ya maadili, uraia, uzalendo kwa vijana na makundi yote vyuoni;<br>(ii) Kukuza maadili ya uadilifu, nidhamu, uwajibikaji na heshima katika maisha ya chuo na baadaye kazini;<br>(iii) Kupambana na wizi wa kitaaluma (plagiarism), udanganyifu katika mitihani na vitendo vya rushwa;<br>(iv) Kusimamia kanuni na taratibu za maadili ya kitaaluma kwa wanafunzi na wahadhiri;<br>(v) Kukuza uongozi wenye maadili kupitia vyama vya wanafunzi na programu za uongozi;<br>(vi) Kuelimisha wanafunzi juu ya wajibu wao kwa taifa na mchango wao katika maendeleo ya nchi;<br>(vii) Kufanya tafiti kuhusu changamoto za maadili katika jamii na kutoa mapendekezo ya sera;<br>(viii) Kuishauri Serikali na taasisi mbalimbali kuhusu masuala ya maadili na mienendo ya kijamii;<br>(ix) Kutumia programu za huduma kwa jamii (community outreach) kuelimisha umma kuhusu maadili;<br>(x) Kulinda haki za wanafunzi na kuhakikisha mazingira salama, yenye heshima na yasiyo na unyanyasaji; na<br>(xi) Kupinga vitendo vya ubaguzi, unyanyasaji wa kijinsia na ukiukwaji wa maadili vyuoni. |
| 17. | Familia Na Jamii | (i) Kutoa fursa toshelevu kwa watoto na vijana KUJIFUNZA na KUFUNDWA fikra na mienendo sahihi kupitia huduma bora na toshelevu ya malezi na makuzi;<br>(ii) Kutoa muda toshelevu kwa watoto na vijana pamoja na kufanya ufuatiliaji wa karibu wa maendeleo yao kimaadili, kielimu na kijamii;<br>(iii) Kuimarisha ushirikiano baina ya wanajamii katika kukabiliana na vitendo vilivyo kinyume na maadili vinavyotendekea kwenye jamii;<br>(iv) Kuimarisha uwajibikaji wa pamoja katika kurithisha maadili kwa watoto na kuwalinda dhidi ya vitendo vya ukatili na hatari ya kukiuka maadili;<br>(v) Kuimarisha uwajibikaji wa pamoja baina ya wanajamii katika kulinda na kuenzi mila na desturi za jamii; na<br>(vi) Kutoa taarifa kwenye mamlaka husika juu ya makosa ya kimaadili yanayojitokeza katika jamii. |

# SURA YA TANO
# URATIBU

## 5 UTANGULIZI

Utekelezaji wa Mkakati wa Taifa wa Kukabiliana na Mmomonyoko wa Maadili utakuwa wa kishirikishi, ukihusisha Wizara, Taasisi za Umma, Wadau wa Maendeleo, Mashirika ya Kiraia, Sekta Binafsi pamoja na jamii kwa ujumla. Lengo kuu la uratibu huu ni kuhakikisha kuwa afua zote za kimkakati zinatekelezwa kwa ufanisi, zinafuatiliwa na kutathminiwa kwa misingi ya uwajibikaji, uwazi na matokeo yanayopimika.

Mkakati huu utaunganishwa na mipango, sera na mikakati mingine ya Serikali ili kuhakikisha mshikamano wa utekelezaji na kuepusha mwingiliano au urudiaji wa shughuli. Aidha, utekelezaji wake utazingatia misingi ya ushirikiano wa wadau wote, mgawanyo wazi wa majukumu, upatikanaji wa rasilimali fedha na watu, matumizi ya takwimu sahihi, usimamizi madhubuti wa muda, pamoja na matumizi ya mbinu bora za mawasiliano.

## 5. 1 MUUNDO WA URATIBU WA UTEKELEZAJI WA MKAKATI

Ili kuhakikisha usimamizi madhubuti, muundo wa uratibu umegawanyika katika ngazi kuu mbili: Ngazi ya Kitaifa na Ngazi ya Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa (MSM).

### 1. Ngazi ya Kitaifa (Kikosi Kazi cha Pamoja)

- Kamati ya Mawaziri wa Wizara Wadau.
- Kamati Elekezi ya Taifa ya Utekelezaji (Makatibu Wakuu).
- Kamati Tendaji ya Taifa ya Uratibu (Wakurugenzi).
- Sekretarieti ya Taifa ya Uratibu.

### 2. Ngazi ya Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa

- Kamati ya Maadili ya Mkoa.
- Kamati ya Maadili ya Wilaya.
- Kamati ya Maadili ya Kata

Aidha, muundo huu unalenga kuwezesha uratibu wa juu hadi chini (top-down) na wa chini hadi juu (bottom-up), ili kuhakikisha kuwa ajenda ya maadili inatekelezwa kikamilifu katika ngazi zote za Serikali na jamii.

## 5.2 UCHAMBUZI WA MAJUKUMU YA VIKAO VYA KITAIFA

### 5.2.1 Kamati ya Mawaziri wa Wizara Wadau wa Mkakati

Kamati ya Mawaziri wa Wizara Wadau wa Mkakati ndiyo chombo cha juu zaidi cha maamuzi ya kisera kuhusu utekelezaji wa Mkakati katika ngazi ya Taifa. Kamati hii itatoa mwelekeo wa kisiasa na kimkakati, pamoja na kusimamia utekelezaji wa jumla wa ajenda ya maadili ya Taifa.

Mwenyekiti wa Kamati hii atakuwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu – Sera, Bunge na Uratibu. Kamati itakuwa na Makatibu wawili ambao ni Katibu Mkuu wa Ofisi ya Waziri Mkuu – Sera, Bunge na Uratibu, na Katibu Mkuu wa Wizara yenye dhamana na Utamaduni.

Kamati itakutana angalau mara moja kwa mwaka ili kupitia taarifa ya maendeleo ya utekelezaji wa Mkakati, pamoja na kutoa maelekezo ya kisera kulingana na mwenendo wa utekelezaji.

Wajumbe wa Kamati ya Mawaziri wa Wizara Wadau watakuwa Mawaziri wa Wizara zifuatazo:

i. Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora;
ii. Ofisi ya Rais, Mipango na Uwezeshaji;
iii. Ofisi ya Rais, Maendeleo ya Vijana
iv. Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera Bunge, Uratibu na Wenye Ulemavu;
v. Ofisi ya Waziri Mkuu, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa;
vi. Wizara ya Fedha;
vii. Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo
viii. Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum;
ix. Wizara ya Mawasiliano na Teknolojia ya Habari;
x. Wizara ya Afya;
xi. Wizara ya Ulinzi ya Jeshi la Kujenga Taifa;
xii. Wizara ya Katiba na Sheria;

xiii. Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi; na
xiv. Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia;

### Majukumu ya Kamati ya Mawaziri

i. Kushauri na kutoa maelekezo ya kisera yanayohitaji utashi na nguvu ya kisiasa kuhusu masuala ya maadili ya Taifa;
ii. Kuhamasisha upatikanaji wa rasilimali fedha na rasilimali watu kwa ajili ya utekelezaji wa Mkakati;
iii. Kuhamasisha Wadau wa Maendeleo na Sekta Binafsi kushiriki katika utekelezaji wa Mkakati;
iv. Kufanya ushawishi katika ngazi ya Taifa na kupitia sekta husika ili kuhakikisha ajenda ya maadili inapewa kipaumbele katika mipango na mikakati ya kitaifa.

## 5.2.2 Kamati Elekezi ya Taifa ya Utekelezaji wa Mkakati

Kamati Elekezi ya Taifa ya Utekelezaji wa Mkakati itaundwa na Makatibu Wakuu wa Wizara wadau. Kamati hii itakuwa kiungo cha msingi kati ya maamuzi ya kisera na utekelezaji wa kitaalam wa Mkakati.

Mwenyekiti wa Kamati atakuwa Katibu Mkuu wa Ofisi ya Waziri Mkuu – Sera, Bunge na Uratibu, na Makamu Mwenyekiti atakuwa Katibu Mkuu wa Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo. Kamati itakuwa na Makatibu wawili ambao ni Mkurugenzi wa Sera na Mipango kutoka Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo, na Mkurugenzi wa Uratibu wa Shughuli za Serikali kutoka Ofisi ya Waziri Mkuu – Sera, Bunge na Uratibu. Kamati itakutana mara mbili (2) kwa mwaka.

### Majukumu ya Kamati Elekezi ya Taifa

i. Kuratibu, kuwezesha na kufuatilia utekelezaji wa Mkakati katika ngazi zote;
ii. Kupitia mipango kazi ya mwaka ya afua za kimkakati na kutoa mapendekezo ya kuimarisha utekelezaji;
iii. Kupitia taarifa za utekelezaji kutoka Wizara na Taasisi wadau na kutoa maelekezo ya kitaalam;
iv. Kufanya ushawishi wa upatikanaji wa rasilimali kutoka Serikali Kuu na wadau wengine;

v. Kubainisha afua zenye matokeo chanya na kupendekeza kuendelezwa au kuigwa;
vi. Kuandaa na kuwasilisha taarifa za utekelezaji za robo mwaka, nusu mwaka na mwaka kwa Kamati Elekezi ya Taifa.

### 5.2.3 Kamati Tendaji ya Taifa ya Uratibu wa Mkakati

Kamati Tendaji ya Taifa ya Uratibu wa Mkakati itaundwa na Wakurugenzi wa Idara Wadau kutoka Wizara Wadau na Wakuu wa Taasisi Wadau. Mwenyekiti wa Kamati hii atakuwa ni Katibu Mkuu Wizara ya Habari Utamaduni Sanaa na Michezo na Katibu atakuwa ni Mkurugenzi wa Sera na Mipango Wizara ya Habari Utamaduni Sanaa na Michezo. Kamati itakutana mara moja kila robo mwaka

#### Wajumbe

Wajumbe wa Kamati ni Wakurugenzi na Wakuu wa Taasisi kutoka Wizara na Taasisi zifuatazo;

i. Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora;
ii. Ofisi ya Rais, Mipango na Uwezeshaji;
iii. Ofisi ya Rais, Maendeleo ya Vijana
iv. Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera Bunge, Uratibu na wenye Ulemavu;
v. Ofisi ya Waziri Mkuu, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa;
vi. Wizara ya Fedha;
vii. Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo
viii. Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum;
ix. Wizara ya Mawasiliano na Teknolojia ya Habari;
x. Wizara ya Afya;
xi. Wizara ya Ulinzi ya Jeshi la Kujenga Taifa;
xii. Wizara ya Katiba na Sheria;
xiii. Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi;
xiv. Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia;
xv. TAKUKURU;
xvi. Jeshi la Kujenga Taifa (JKT);
xvii. Kamandi ya Jeshi la Akiba-Mgambo;
xviii. Jeshi la Polisi (Dawati la Jinsia na Kitengo cha Makosa ya Mtandao);
xix. Msajili Mkuu wa Mahakama;

xx. Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA);
xxi. Jeshi la Magereza;
xxii. Ofisi ya Taifa ya Takwimu (NBS);
xxiii. Tume ya Vyuo Vikuu (TCU);
xxiv. Chama cha Skauti Tanzania;
xxv. Taasisi zilizo chini wa Wizara ya Habari (BASATA, BFT, TBC, ALHC, COSOTA, JABI)

**Majukumu ya Kamati Tendaji ya Taifa ya Uratibu wa Mkakati**

i. Kuratibu, kuwezesha na kufuatilia utekelezaji wa Mkakati katika ngazi zote;
ii. Kupitia mipango kazi ya mwaka ya afua za kimkakati na kutoa mapendekezo ya kuimarisha utekelezaji;
iii. Kupitia taarifa za utekelezaji kutoka Wizara na Taasisi wadau na kutoa maelekezo ya kitaalam;
iv. Kufanya ushawishi wa upatikanaji wa rasilimali kutoka Serikali Kuu na wadau wengine;
v. Kubainisha afua zenye matokeo chanya na kupendekeza kuendelezwa au kuigwa;
vi. Kuandaa na kuwasilisha taarifa za utekelezaji za robo mwaka, nusu mwaka na mwaka kwa Kamati Elekezi ya Taifa.
vii. Kuhakikisha kuwa vipengele vya mikataba ya kikanda na kimataifa kuhusiana masuala ya kijamii, kiuchumi na kimazingira vinazingatia maadili ya Mtanzania

### 5.2.4 Sekretarieti ya Taifa ya Uratibu wa Mkakati

Sekretarieti ya Taifa ya Uratibu ni chombo cha kuratibu na kusimamia shughuli za kila siku za utekelezaji wa Mkakati. Mwenyekiti wa Sekretarieti atakuwa Mkurugenzi wa Sera na Mipango kutoka Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo.

Aidha, kutakuwa na Waratibu watano wa shughuli za kila siku za Mkakati ambao watatoka; OWM-Sera, Bunge, Uratibu na Wenye Ulemavu (Mratibu Mkuu), Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo (Mratibu Mkuu Mwenza), OWM TAMISEMI (Mratibu Mwenza), OR – Maendeleo ya Vijana (Mratibu Mwenza), na Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na

Makundi Maalum (Mratibu Mwenza) na kila Wizara iliyotoa mratibu itagharamia shughuli za mratibu kutoka Wizara husika ikiwemo na kumpatia ofisi na gari kwa ajili ya utekelezaji wa shughuli za kila siku za Mkakati.

Sekretarieti itakutana mara moja kila mwezi au kwa dharula ya taarifa ya wiki 1 kujadili masuala mbalimbali ya utekelezaji wa Mkakati.

## Wajumbe

i. Mkurugenzi wa Sera na Mipango Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo-Mwenyekiti
ii. Mkurugenzi wa Idara ya Maendeleo ya Utamaduni-Makamu Mwenyekiti
iii. Mkurugenzi wa ufuatiliaji na Tathimini Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo
iv. Mkurugenzi anayesimamia Idara/kitengo yenye dhamana na maadili ya Taifa
v. Waratibu wa utekelezaji wa Mkakati
vi. Wajumbe 8 kutoka Wizara wadau (Watateuliwa na Makatibu Wakuu wa Wizara husika)
vii. Wajumbe 8 kutoka Taasisi wadau (Watateuliwa na wakuu wa Taasisi husika)

## Majukumu ya Sekretarieti:

i. Kuratibu maandalizi na uendeshaji wa vikao vyote vya kitaifa vinavyohusiana na utekelezaji wa Mkakati;
ii. Kuandaa na kuunganisha taarifa za utekelezaji wa Mkakati, ikijumuisha changamoto, mafanikio na mapendekezo;
iii. Kuratibu shughuli za ufuatiliaji, tathmini, tafiti na ujifunzaji;
iv. Kutoa msaada wa kitaalam kwa kamati zote za utekelezaji;
v. Kuandaa miongozo ya kurahisisha utekelezaji wa Mkakati katika ngazi zote;
vi. Kuratibu utekelezaji wa kila siku wa shughuli za Mkakati na kuhakikisha malengo yaliyopangwa yanafikiwa.

### 5.2.5 Uratibu katika ngazi Ya Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa

Ili mkakati utekelezwe kwa ufanisi katika ngazi ya jamii, uratibu utafanyika kama ifuatavyo:

### A. Uratibu ngazi OWM - TAMISEMI

Uratibu waMkakati kwa ujumla wake utasimamiwa na Ofisi ya Waziri Mkuu (Sera, Bunge, Uratibu na Wenye Ulemavu) na kusaidiwa na Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo. Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo itakuwa na jukumu la msingi la kusimamia na kuratibu shughuli za kitaalam katika utekelezaji wa Mkakati. Wizara za kisekta zitashirikiana na Taasisi, Idara na Wakala mbalimbali wa Serikali kutekeleza afua mbalimbali za kukabiliana na mmomonyoko wa maadili.

Ofisi ya Waziri Mkuu Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (OWM-TAMISEMI) itaratibu utekelezaji wa mkakati katika ngazi za Mikoa, Halmashauri, Kata na Vijiji/Mtaa.

#### Majukumu mahususi ya OWM TAMISEMI katika uratibu wa Mkakati:

i. Kuhakikisha kwamba afua za kukabiliana na mmomonyoko kama zilivyobainishwa katika Mkakati zinajumuishwa katika mipango na bajeti za Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa;
ii. Kuijumuisha ajenda ya kukabiliana na mmomonyoko wa maadili katika vikao vya Kamati za Ushauri za Mikoa, Kamati za Baraza la Madiwani, Kamati za wataalamu za Halmashauri, Kamati ya Maendeleo Kata na Halmashauri za Vijiji/Mitaa;
iii. Kupokea na kuunganisha taarifa za utekelezaji wa Mkakati kutoka Mikoani na Halmashauri na kuziwasilisha kwa Sekretarieti ya Taifa ya Uratibu wa Mkakati;
iv. Kuratibu na kusimamia shughuli za wadau wa maadili katika ngazi za Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa;
v. Kusimamia uratibu wa Mikutano ya Mwaka ya Wadau wa Maadili ngazi ya Mkoa na Halmashauri;
vi. Kutoa msaada wa kiufundi kwa Mikoa na Halmashauri itakayohitajika wakati wa utekelezaji wa Mkakati; na

vii. Kufanya na kushiriki ziara za pamoja za usimamizi, ufuatiliaji, tathmini na mafunzo yanayohusu utekelezaji wa Mkakati katika Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa.

## B. Kamati ya Maadili ya Mtanzania ya Mkoa

Kamati hii itasimamiwa na Katibu Tawala wa Mkoa na Katibu wake atakuwa ni Afisa Utamaduni wa Mkoa ambaye pia atakuwa Mratibu wa Mkoa wa uratibu wa Mkakati.

Mwenyekiti ambaye pia ni Katibu Tawala (M) (RAS) atawasilisha ajenda ya Taarifa ya Utekelezaji wa Mkakati katika Kikao cha Kamati ya Ushauri ya Mkoa (RCC) ambapo Mwenyekiti wake (Mkuu wa Mkoa) ataombwa ruhusa ya kuwajumuisha wajumbe wa kamati ya Maadili ya Mkoa kushiriki katika vikao vya RCC pindi inapojadili ajenda ya Maadili.

Kamati hii itakutana kila robo mwaka

### Wajumbe wa Kamati

i. Katibu Tawala Mkoa (RAS)-Mwenyekiti;
ii. Afisa Utamaduni Mkoa-Katibu;
iii. Katibu Tawala Msaidizi-Utawala
iv. Katibu Tawala Msaidizi -Elimu (M);
v. Katibu Tawala Msaidizi - Afya (M);
vi. Katibu Tawala Msaidizi – Uchumi (M);
vii. Katibu Tawala Msaidizi – Serikali za Mitaa (M);
viii. Katibu Tawala Msaidizi – Mipango na Uratibu (M);
ix. Katibu Tawala Msaidizi Uwekezaji, Viwanda na Biashara (M);
x. Afisa Maendeleo ya Jamii (M);
xi. Afisa Ustawi wa Jamii (M);
xii. Afisa kutoka Jeshi la Magereza;
xiii. Afisa Kutoka TAKUKURU;
xiv. Afisa kutoka Ofisi ya RSO;
xv. Mratibu wa Dawati la Jinsia na Watoto wa Jeshi la Polisi (M);
xvi. Wanasheria wa Mkoa; na
xvii. Hakimu Mkazi Mkuu.

### Wajumbe waalikwa pale inapobidi kufanya hivyo ili kurahisisha utekelezaji wa shughuli za kamati

i. Wawakilishi wa Viongozi wa Dini;
ii. Wawakilishi wa Viongozi wa Kimila;
iii. Wawakilishi 2 kutoka Baraza la Watoto (M);
iv. Wawakilishi 2 wa Vijana;
v. Wawakilishi wa Vikundi vya wanawake; na
vi. Wawakilishi kutoka kundi lolote lile ambalo Kamati itaazimia ijumuishwe kwenye kamati ili kurahisisha utekelezaji wa majukumu ya kamati.

### Majukumu ya Kamati

i. Kufuatilia na kufanya tathmini ya utekelezaji wa Mkakati ili kuhakikisha kuwa shughuli zilizopangwa kutekelezwa katika Halmashauri zote zinafanyika;
ii. Kusimamia ujumuishaji wa afua za kukabiliana na mmomonyoko wa maadili katika mipango na bajeti zote za Halmashauri zote zilizopo chini ya Mkoa;
iii. Kutoa maelekezo ya kisera, kikanuni na kitaalam kuhusiana na utekelezaji wa mkakati kwa Mamlaka za Serikali za Mitaa (MSM);
iv. Kupitia na kuidhinisha mpango wa mwaka wa utekelezaji wa Mkakati kutoka Kamati za Maadili za Halmashauri;
v. Kupitia, kuidhinisha na kuunganisha taarifa za utekelezaji wa Mkakati kutoka Mikoani na kuziwasilisha Ofisi ya Waziri Mkuu -TAMISEMI; na
vi. Kuratibu Mkutano Mkuu wa Mwaka wa Wadau wa Maadili wa Mkoa kwa kila mwaka mara moja kwa ajili ya kuwapa fursa ya kutoa maoni yao kuhusu utekelezaji wa Mkakati na afua mbalimbali za kukabiliana na mmomonyoko wa maadili.

## C. Kamati ya Maadili ya Mtanzania ya Halmashauri

Kamati hii itasimamiwa na Mkurugenzi wa Halmashauri na Katibu wake atakuwa ni Afisa Utamaduni wa Halmashauri ambaye pia atakuwa Mratibu wa Halmashauri wa uratibu wa Mkakati.

Mwenyekiti ambaye ambaye pia ni Mkurugenzi wa Halmashauri atawasilisha ajenda ya Taarifa ya Utekelezaji wa Mkakati katika Kikao cha Kamati ya Ushauri ya Wilaya (DCC) ambapo Mwenyekiti wake (Mkuu wa Wilaya) ataombwa ruhusa ya kuwajumuisha wajumbe wa Kamati ya Maadili ya Halmashauri kushiriki katika vikao vya DCC pindi inapojadili ajenda ya Maadili. Vilevile Mwenyekiti wa Kamati hii ataomba ridhaa ya kuwasilisha ajenda ya Taarifa ya Utekelezaji wa Mkakati mara mbili kwa Mwaka au zaidi katika kikao cha Kamati ya Ulinzi na Usalama ya Wilaya ambayo itapokea na kutoa maelekezo mahususi yatakayopaswa pia kuzingatia wa Kamati katika utekelezaji wa majukumu yake. Kamati hii itakutana kila robo mwaka.

### Wajumbe wa kamati

i. Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri-Mwenyekiti;
ii. Afisa Utamaduni wa Halmashauri-Katibu;
iii. Afisa Utumishi(W);
iv. Katibu Tawala Wilaya (DAS);
v. Afisa Maendeleo ya Jamii (W);
vi. Afisa Ustawi wa Jamii(W);
vii. Afisa Mipango(W);
viii. Afisa Takwimu na ufuatiliaji(W);
ix. Afisa Elimu Msingi
x. Afisa Elimu Sekondari(W);
xi. Afisa Biashara (W);
xii. Mganga Mkuu (W);
xiii. Mratibu wa Dawati la Jinsia na Watoto wa Jeshi la Polisi (W);
xiv. Hakimu Mkazi (W);
xv. Afisa Magereza (W);
xvi. Mwanasheria wa Halmashauri (W);
xvii. Mshauri wa Mgambo(W); na
xviii. Kamishna wa Chama cha Skauti(W)

### Wajumbe waalikwa pale inapobidi kufanya hivyo ili kurahisisha utekelezaji wa shughuli za kamati

i. Wawakilishi wa Viongozi wa Dini;
ii. Wawakilishi wa Viongozi wa Kimila;

iii. Wawakilishi 2 kutoka Baraza la Watoto (M);
iv. Wawakilishi 2 wa Vijana;
v. Wawakilishi wa Vikundi vya wanawake; na
vi. Wawakilishi kutoka kundi lolote lile ambalo Kamati itaazimia ijumuishwe kwenye kamati ili kurahisisha utekelezaji wa majukumu ya kamati.

### Majukumu ya Kamati

Kufuatilia na kufanya tathmini ya utekelezaji wa Mkakati ili kuhakikisha kuwa shughuli zilizopangwa kutekelezwa katika Kata zote zinafanyika;

i. Kuhakikisha kwamba bajeti inatengwa kwa ajili ya uratibu na utekelezaji wa mkakati;
ii. Kusimamia utekelezaji wa Mkakati ngazi ya Halmashauri;
iii. Kuandaa na kuwasilisha taarifa ya utekelezaji wa Mkakati kwa Baraza la Madiwa, Kamati ya ushauri ya Wilaya(DCC) na Kamati ya Maadili ya Mkoa;
iv. Kupitia na kuidhinisha mpango wa mwaka wa kamati za kila Kata;
v. Kuwezesha na kufuatilia mipango ya utekelezaji wa Mkakati inayoandaliwa kila mwaka katika ngazi za Kata;
vi. Kuhamasisha ujumuishaji wa ajenda ya kukabiliana na mmomonyoko wa maadili katika vikao, mikutano na matukio ya sekta ngazi ya Halmashauri, Kata na Vijiji/Mtaa; na
vii. Kubainisha wadau na kuandaa Mkutano wa Mwaka wa wadau wa Maadili mara moja kwa kila Mwaka.

## D. Kamati ya Maadili ya Mtanzania ya Kata

Kamati hii itakuwa na jukumu la kuratibu na kusimamia utekelezaji wa Mkakati katika ngazi ya kata. Afisa Mtendaji Kata atakuwa Mwenyekiti wa kamati na nafasi ya Katibu itakuwa chini ya Afisa Utamaduni/Afisa Elimu/Afisa Maendeleo ya Jamii /Afisa Ustawi wa Jamii ngazi ya kata. Afisa Mtendaji kama mwenyekiti wa kamati ataandaa na kuwasilisha Ajenda za maadili katika Kikao cha Kamati ya Maendeleo ya Kata ambapo idhini itaombwa kwa Mhe. Diwani ambaye ndiye mwenyekiti wa kikao hicho kuwajumuisha wajumbe wa kamati katika kikao hicho kulingana na Ajenda za kikao husika. Kikao cha Kamati hii kitafanyika kila robo mwaka na wajumbe wengine wa kamati ni kama ifuatavyo;

### Wajumbe wa kamati

i. Afisa Mtendaji Kata;
ii. Afisa Utamaduni;
iii. Afisa Maendeleo ya Jamii;
iv. Afisa Ustawi wa Jamii;
v. Mganga Mfawizi
vi. Mratibu wa Dawati la Jinsia na Watoto wa Jeshi la Polisi;
vii. Hakimu Mkazi wa Mahakama ya Mwanzo;
viii. Afisa Elimu Kata;
ix. Polisi Kata;
x. Mwakilishi wa Polisi Jamii Kata;
xi. Wawakilishi 2 wa Walimu wa Ushauri na Unasihi-Msingi;
xii. Wawakilishi 2 wa Walimu wa Ushauri na Unasihi-Sekondari;

### Wajumbe waalikwa pale inapobidi kufanya hivyo ili kurahisisha utekelezaji wa shughuli za kamati

i. Wamiliki na Wakuu wa Shule za Msingi na Sekondari za Umma na Binafsi zilizopo ndani ya Kata;
ii. Wawakilishi 4 wa Viongozi wa Dini;
iii. Wawakilishi 2 wa Viongozi wa Kimila/Baraza la Wazee;
iv. Wawakilishi 2 kutoka Baraza la Watoto (M);
v. Wawakilishi 2 wa Vijana;
vi. Wawakilishi 2 wa Vikundi vya wanawake; na
vii. Wawakilishi kutoka kundi lolote lile ambalo Kamati itaazimia ijumuishwe kwenye kamati ili kurahisisha utekelezaji wa majukumu ya kamati

### Majukumu ya Kamati

i. Kufuatilia na kufanya tathmini ya utekelezaji wa Mkakati katika ngazi za Kata;
ii. Kuandaa na kutunza kanzidata ya wadau wanaosaidia katika utekelezaji wa afua za kukabiliana na mmmonyoko wa maadili katika ngazi ya kata;
iii. Kujumuisha afua za kukabiliana na mmomonyoko wa maadili katika mipango na bajeti za Vijiji/Mitaa na Kata;

iv. Kujumuisha ajenda ya maadili katika mikutano na matukio yote ngazi ya Kata na Vijiji/Mtaa;
v. Kuhamasisha ushiriki wa wadau katika utekelezaji wa Mkakati ngazi ya Kata;
vi. Kutoa taarifa kwa wakati kuhusu utekelezaji wa Mkakati kwa Kamati ya Maadili ya Halmashauri;
vii. Kuandaa Mkutano wa Mwaka wa wadau wa Maadil katika ngazi ya Kata kujadili mafanikio, changamoto na muonombele katika utekelezaji wa Mkakati. Mkutano wa Mwaka utafanyika kila mwaka mara moja kwa kujumuisha wajumbe wa kamati za Vijiji/Mtaa za Kata husika pamoja na wajumbe waalikwa kwa kuzingatia mahitaji ya wakati.

## E. Kamati ya Maadili ya Mtanzania ya Kijiji/Mtaa

Kamati hii itakuwa na jukumu la kuratibu na kusimamia utekelezaji wa Mkakati katika ngazi ya Kijiji/Mtaa. Afisa Mtendaji Kijiji/Mtaa atakuwa Mwenyekiti wa kamati na nafasi ya Katibu itakuwa chini ya Mwalimu wa Malezi atakayeteuliwa na Mtendaji wa Kijiji/Mtaa na kuthibitishwa na Kamati ya Maadili ya Kijiji/Mtaa katika kikao cha awali cha Kamati. Kikao cha Kamati hii kitafanyika kila robo mwaka.

Mwenyekiti wa kamati ataandaa ajenda ya Maadili na taarifa ya utekelezaji wa Mkakati na kisha kuziwasilisha katika Vikao vyote vya Serikali ya Kijiji/Mtaa pamoja na Mkutano Mkuu wa Kijiji kwa ridhaa ya Mwenyekiti wa Kijiji/Mtaa. Vilevile kwa ridhaa ya Mwenyekiti wa Kijiji/Mtaa atawakaribisha wajumbe wa kamati kushiriki Vikao vya Serikali ya Kijiji/Mtaa pale ambapo Vikao husika vitajumuisha ajenda za maadili.

### Wajumbe wa kamati

i. Afisa Mtendaji wa Kijiji/Mtaa;
ii. Mwalimu wa Malezi na Unasihi;
iii. Afisa Afya;
iv. Walimu Wakuu kutoka shule za msingi zilizopo ndani ya kijiji au Mtaa;
v. Wakuu wa vituo vya malezi ya mchana (Day Care Centers) vilivyopo Kijijini/Mtaani;

vi. Walimu wa malezi na unasihi kutoka shule za Msingi zilizopo ndani ya kijiji au Mtaa; na
vii. Polisi Jamii.

### Wajumbe waalikwa pale inapobidi kufanya hivyo ili kurahisisha utekelezaji wa shughuli za kamati

i. Wamiliki na Wakuu wa Shule za Msingi na Sekondari za Umma na Binafsi zilizopo ndani ya Kijiji;
ii. Wawakilishi 4 wa Viongozi wa Dini;
iii. Wawakilishi 2 wa Viongozi wa Kimila/Baraza la Wazee;
iv. Wawakilishi 2 kutoka Baraza la Watoto (M);
v. Wawakilishi 2 wa Vijana;
vi. Wawakilishi 2 wa Vikundi vya wanawake; na
vii. Wawakilishi kutoka kundi lolote lile ambalo Kamati itaazimia ijumuishwe kwenye kamati ili kurahisisha utekelezaji wa majukumu ya kamati

### Majukumu ya Kamati

i. Kubaini makundi/mienendo/maeneo hatarishi (kichocheo cha mmomonyoko wa maadili) katika kijiji/mtaa na kupanga mikakati/mipango ya kukabiliana na mmomonyoko wa maadili unaochochewa na makundi/mienendo/maeneo husika.
ii. Kuratibu kampeni za kuhamasisha uwajibikaji wa wadau wa urithishaji maadili kwa watoto na Vijana ndani ya Kijiji/Mtaa. Uhamasishaji ufanyike kupitia majukwaa kama Vikao vya Wazazi Mashuleni, Programu za utoaji huduma katika zahanati na vituo vya Afya katika huduma za Mama na Mtoto (Kliniki), Mikutano ya Kijiji/Mtaa, matukio mengine ya kijamii kama Misiba na harusi pamoja na majukwaa mengine yanayokuwa na mikusanyiko kulingana na mazingira ya eneo husika]
iii. Kuhamaisha uwajibikaji wa Taasisi za kidini, asasi za kiraia na vikundi ya wanawake na vijana katika kuhamasisha uwajibikaji wa jamii katika kurithisha na kulinda maadili ya jamii;
iv. Kuwezesha utekelezaji wa pamoja wa Mkakati katika ngazi ya Kijiji/Mtaa;

v. Kutoa taarifa kwa wakati kuhusu utekelezaji wa Mkakati ngazi ya Kijiji/Mtaa;
vi. Kujumuisha Ajenda ya kukabiliana na mmomonyoko wa maadili katika mikutano ya Kijiji/Mtaa;
vii. Kuelimisha jamii kuhusu athari za mmomonyoko wa maadili kijamii, kiuchumi na kimazingira; na
viii. Kufanya kikao cha wadau wa maadili katika ngazi ya jamii kujadili mafanikio, changamoto na muonombele katika utekelezaji wa Mkakati ngazi ya jamii.

# SURA YA SITA
# MWONGOZO WA MAWASILIANO

## 6 UTANGULIZI

Uzoefu uliopatikana katika utekelezaji wa mikakati mbalimbali umeonyesha kuwa uboreshaji wa mawasiliano kati ya watekelezaji na jamii ni nguzo muhimu ya mafanikio. Hivyo, utekelezaji wa Mkakati wa Taifa wa Kukabiliana na Mmomonyoko wa Maadili utaongozwa na Mwongozo wa Mawasiliano wa pamoja kwa wadau wote, chini ya uratibu wa Wizara yenye dhamana ya Utamaduni.

## 6.1 MASUALA MUHIMU KATIKA MWONGOZO WA MAWASILIANO

Mwongozo wa Mawasiliano ni nyenzo ya kimkakati inayolenga kuhakikisha upatikanaji wa taarifa kwa wadau wote wanaohusika katika utekelezaji wa Mkakati wa Taifa wa Kukabiliana na Mmomonyoko wa Maadili. Masuala muhimu yanayozingatiwa katika Mwongozo huu ni pamoja na: kubainisha lengo kuu na malengo mahsusi ya mawasiliano; kufanya uchambuzi wa wadau na kuwapanga katika makundi kulingana na umuhimu na ushawishi wao; kubainisha hadhira lengwa na aina ya taarifa zinazohitajika; kuandaa maudhui yenye mvuto na ushawishi kwa makundi husika; kuchagua njia na mbinu sahihi za mawasiliano; pamoja na kuweka utaratibu madhubuti wa mrejesho.

## 6.2 LENGO KUU NA MALENGO MAHSUSI KATIKA MWONGOZO WA MAWASILIANO

### 6.2.1 Lengo Kuu

Kuimarisha uelewa na ushiriki wa Watanzania katika utekelezaji wa Mkakati wa Taifa wa Kukabiliana na Mmomonyoko wa Maadili.

### 6.2.2 Malengo Mahsusi

i) Kukuza uelewa wa umuhimu wa Mkakati wa Taifa wa Kukabiliana na Mmomonyoko wa Maadili na Taasisi zinazohusika;

ii) Kushirikisha wadau katika kuelimisha Umma kuhusu athari za mmomonyoko wa maadili kuanzia ngazi ya kaya hadi Taifa; na

iii) Kutoa mrejesho kwa Umma kuhusu mafanikio ya utekelezaji wa Mkakati wa Taifa wa Kukabiliana na Mmomonyoko wa Maadili.

## 6.3 WAHUSIKA WA MWONGOZO WA MAWASILIANO

Wahusika wa mwongozo wa mawasiliano wamegawanyika katika makundi mawili ambao ni wasimamizi na walengwa.

### 6.3.1 Wasimamizi wa Mwongozo wa Mawasiliano

Wizara yenye dhamana ya masuala ya Utamaduni itakuwa na jukumu la kusimamia na kuratibu utekelezaji wa Mwongozo wa Mawasiliano kwa kushirikiana na taasisi za umma na zisizo za kiserikali. Taasisi zote zitawajibika kuwasilisha taarifa zinazohitajika kwa mujibu wa Mpango wa Ufuatiliaji, Tathmini na Kujifunza, ili kuwezesha upatikanaji wa taarifa sahihi na kwa wakati.

### 6.3.2 Walengwa wa Mwongozo wa Mawasiliano

alengwa wamegawanywa katika makundi mawili: Warithishaji na Warithishwaji kama inavyoonekana katika jedwali Na. 3 hapa chini.

**Jedwali Na. 4 Walengwa wa Mwongozo wa mawasiliano**

| Na. | Kundi la kwanza (Warithishaji) | Kundi la pili (Warithishwaji) |
|---|---|---|
| 1. | Wazazi | Watoto na vijana |
| 2. | Walimu | Wanafunzi |
| 3. | Viongozi wa dini | Waumini Wa Dini Na Jamii |
| 4. | Machifu na viongozi wa kimi la | Vijana Na Jamii |
| 5. | Wazee | Watoto, Vijana Na Jamii |

## 6.4 MBINU NA NJIA ZA MAWASILIANO

Mwongozo huu utatumia mbinu zifuatazo katika kufanya mawasiliano na walengwa:

### 6.4.1 Mbinu za mawasiliano

a) Matumizi ya matoleo rahisi ya ujumbe katika lugha ya Kiswahili na Kiingereza kulingana na mahitaji ya makundi lengwa;
b) Kuandaa jumbe maalum kwa ajili ya
   i) Kujenga tabia ya kuhimiza uzingatiaji maadili kwa watoto kuanzia nyumbani, Taasisi za elimu na dini;
   ii) Kubadilisha na kudhibiti tabia za watu wazima zinazo chochea mmomonyoko wa maadili katika jamii kupitia vikao maalum mahali pa kazi (kama sehemu ya mafunzo elekezi na semina za kawaida) na mahubiri ya ibada ya watu wazima;
   iii) Kuelimisha umma katika maeneo ya usafiri wa umma ikiwemo mabasi, treni, vivuko, bandari, viwanja vya ndege na vituo vya usafiri.
c) Kuandaa Warsha, Semina na Makongamano kwa ajili ya uhamasishaji wa utekelezaji wa Mkakati wa Kukabiliana na Mmomonyoko wa Maadili;
d) Kuhamasisha Watanzania kushirikiana na Serikali kufichua tabia zinazoendeleza mmomonyoko wa maadili;
e) Kutumia wanahabari kufichua vitendo vinayodhoofisha jitihada za kukabiliana na mmomonyoko wa maadili nchini;
f) Kutumia kauli mbiu zenye jumbe za kupinga mmomonyoko wa Maadili kwenye barua pepe zote za watumishi wa taasisi za umma na binafsi; na
g) Kufanya mikutano ya mara kwa mara na vyombo vya habari kwa ajili ya kutoa taarifa kwa Umma kuhusu hali ya mmomonyoko wa maadili.

### 6.4.2 Njia za mawasiliano

Mwongozo huu utatumia njia mbalimbali za mawasiliano ikiwemo machapisho, redio, televisheni, mitandao ya kijamii, mikusanyiko ya kijamii, sanaa za maonesho, pamoja na mikutano na vyombo vya Habari kama inavyofafanuliwa katika jedwali hapa chini:

## Jedwali Na. 5 Njia ya mawasiliano

| Na. | Njia ya mawasiliano | Nyenzo | Walengwa |
|---|---|---|---|
| 1. | Machapisho | Magazeti, Majarida, Vipeperushi, na Mabango, | Wanaojua kusoma, vijana, wanafunzi, na Jamii kwa ujumla |
| 2. | Mitandao ya kijamii | Facebook, Whatsapp, Instagram, Twitter, YouTube, Blogs, LinkedIn, Tovuti, Wavuti, Barua-pepe, Intranet | Vijana, na Jamii kwa ujumla |
| 3. | Mikusanyiko ya Kijamii | mikutano, warsha, makongamano, semina, na mikutano kwa njia ya simu au video; na maonesho ya biashara ya kitaifa na kimataifa | Kundi lengwa na Jamii kwa ujumla |
| 4. | Sanaa | Sanaa bunifu na sanaa za maonesho ikiwemo Nyimbo, tamthiliya, ngoma, filamu, maigizo, vichekesho n.k) | Vijana na Jamii kwa ujumla |
| 5. | Vyombo vya habari | Redio, Televisheni, Wanahabari, Matangazo na taarifa kwa Umma | Jamii kwa ujumla |

# SURA YA SABA
# UFUATILIAJI, TATHMINI NA KUJIFUNZA

## 7 UTANGULIZI

Ufuatiliaji ni mchakato endelevu unaofanyika wakati wote wa utekelezaji wa Mkakati ili kuhakikisha shughuli zinatekelezwa kama zilivyopangwa. Lengo kuu ni kuhakikisha matumizi ya rasilimali yanashabihiana na kazi zilizofanyika, kubaini mapungufu mapema, kutoa mrejesho wa papo hapo, na kufanya marekebisho ya kiutendaji ili kuongeza tija.

Tathmini ni upimaji wa kina wa matokeo ya kazi zilizokamilika au zinazoendelea kulingana na malengo ya awali. Kwa kawaida, tathmini hufanyika katika kipindi cha kati au mwishoni mwa utekelezaji ili kupima tija, ufanisi, na athari ya Mkakati.

Kujifunza ni matumizi ya matokeo ya ufuatiliaji na tathmini katika kufanya maamuzi ya kimkakati, kuboresha mbinu za utendaji, na kuibua mbinu mpya za kukabiliana na mmomonyoko wa maadili nchini.

Utekelezaji wa Mkakati wa Taifa wa Kukabiliana na Mmomonyoko wa Maadili utazingatia Mpango wa Ufuatiliaji na Tathmini uliowekwa, ambapo taasisi zote tekelezi zinapaswa kuufuata ili kuhakikisha matokeo yanapimika kwa usahihi.

## 7.1 MADHUMUNI YA UFUATILIAJI NA TATHMINI

Madhumuni ya Mpango wa Ufuatiliaji, Tathmini na Kujifunza ni kuhakikisha kuwa Mkakati wa Taifa wa Kukabiliana na Mmomonyoko wa Maadili unatekelezwa kwa ufanisi, kwa wakati, na kwa kuzingatia malengo na matarajio yaliyowekwa. Mpango huu utatumika kama chombo cha kusimamia na kutoa mwelekeo wa ushiriki wa wadau katika utekelezaji na ufuatiliaji wa Mkakati; kudhibiti na kupima matumizi ya rasilimali fedha na rasilimali watu; pamoja na kupima uwajibikaji wa kila mdau na mchango wake katika utekelezaji wa Mkakati.

## 7.2 MISINGI YA KUZINGATIA KATIKA UFUATILIAJI NA TATHMINI

Ufuatiliaji na Tathmini ya utekelezaji wa Mkakati wa Taifa wa Kukabiliana na Mmomonyoko wa Maadili utazingatia misingi ifuatayo:

i) Kujenga na kuimarisha uwezo wa taasisi na wadau katika masuala ya Ufuatiliaji, Tathmini na Kujifunza;

ii) Kuhakikisha ulinganifu na uratibu wa Mpango wa Ufuatiliaji na Tathmini wa Mkakati na mifumo mingine ya kitaifa ya Ufuatiliaji na Tathmini;

iii) Kuweka mazingira wezeshi ya utekelezaji wa Mpango wa Ufuatiliaji na Tathmini, ikiwemo upatikanaji wa rasilimali watu, fedha na miundombinu husika.

## 7.3 VIASHIRIA VYA UTENDAJI

Viashiria vya utendaji ni nyenzo muhimu za kupima maendeleo na mafanikio ya utekelezaji wa Mkakati wa Taifa wa Kukabiliana na Mmomonyoko wa Maadili. Kazi kuu ya viashiria hivi ni kufuatilia kwa ukaribu utekelezaji wa shughuli na kupima kiwango ambacho malengo yaliyowekwa yanafikiwa. Ufanisi wa Ufuatiliaji na Tathmini ya Mkakati unategemea kwa kiasi kikubwa uimara na ubora wa mfumo wa upimaji wa viashiria vya utendaji. Viashiria vya matokeo ya Mpango wa Ufuatiliaji na Tathmini wa Mkakati vimeambatishwa katika Kiambatisho Na. 1.

## 7.4 UKUSANYAJI NA UCHAMBUZI WA TAKWIMU

Ukusanyaji wa takwimu utafanyika kwa kutumia mbinu mbalimbali ikiwemo tafiti, mapitio ya taarifa na kumbukumbu zinazohusiana na masuala ya maadili, pamoja na ziara za kutembelea maeneo yaliyoathiriwa na mmomonyoko wa maadili. Takwimu zitakazokusanywa zitachakatwa, kuchambuliwa na kusambazwa kwa wadau husika kwa madhumuni ya kufanya maamuzi, kuboresha utekelezaji wa Mkakati, na kukuza ujifunzaji wa pamoja miongoni mwa wadau wote.

## 7.5 TAARIFA YA UFUATILIAJI NA TATHIMINI

### 7.5.1 Aina za Taarifa za Ufuatiliaji na Tathmini

Kuna aina nne (4) za taarifa za Ufuatiliaji na Tathmini kuhusu Mkakati zitakazokuwa zinaandaliwa.

i) Taarifa za utekelezaji/Ufuatiliaji;
ii) Taarifa ya tathmini;
iii) Taarifa za tafiti mbalimbali zilizofanywa kuhusu mmomonyoko wa maadili nchini; na
iv) Taarifa za mapitio ya Mkakati wa Taifa wa Kukabiliana na Mmomonyoko wa Maadili.

### 7.5.2 Uwasilishwaji wa Taarifa

Taarifa za kila robo, nusu na mwaka mzima kama zilivyoainishwa (Jedwali Na. 5), kuhusu utekelezaji wa Mkakati wa Taifa wa kukabiliana na Mmomonyoko wa Maadili zitaandaliwa na Wizara na Taasisi Wadau na kuwasilishwa katika Wizara yenye dhamana ya Utamaduni na kisha kuwasilishwa Ofisi ya Waziri Mkuu - Sera, Bunge, Uratibu na wenye Ulemavu . Taarifa hizo zitafanyiwa mapitio na majumuisho kisha mrejesho utawasilishwa kwa wadau kwa lengo la kuwapa taarifa na kuboresha utendaji kazi katika masuala yanayohusu Mmomonyoko wa Maadili.

### Jedwali Na. 6 Taarifa za Ufuatiliaji na Tathmini

| Aina ya Taarifa | Maudhui Taarifa | Muda wa Uwasilishaji |
|---|---|---|
| Taarifa za utekelezaji/Ufuatiliaji | Taarifa za utekelezaji wa Mkakati. | Taarifa za robo, nusu na Mwaka mzima |
| Taarifa ya tathmini | Mafanikio, Mapungufu, Fursa na Changamoto zinazojitokeza wakati wa utekelezaji wa Mkakati. | Mara mbili (2028,2031) |
| Taarifa za tafiti mbalimbali zilizofanywa kuhusu Mmomonyoko wa maadili nchini | Matokeo na mapendekezo ya masuala maalum yaliyofanyiwa utafiti kuhusu maadili | Baada ya tafiti kufanyika. |
| Taarifa za mapitio ya Mkakati wa Taifa wa Kukabiliana na Mmomonyoko wa Maadili | Mafanikio ya jumla ya malengo ya Mkakati wa Taifa wa Kukabiliana na Mmomonyoko wa Maadili, Mapungufu, fursa na changamoto zilizojitokeza | Baada ya miaka mitatu tangu kuanza kutekelezwa kwa Mkakati |

| Na. | Malengo | Viashiria | Matokeo |
|---|---|---|---|
| 1. | Kukuza na kuimarisha wajibu wa wazazi, walezi na familia katika malezi ya watoto na vijana | Asilimia ya wazazi/walezi wanaoshiriki programu za elimu ya malezi bora. | Kuimarika kwa malezi bora kwa Watoto na vijana |
| | | Idadi ya programu au kampeni za uelimishaji kuhusu maadili, nidhamu na malezi | Kuongezeka kwa uelewa kuhusu maadili, nidhamu na malezi |
| | | Idadi ya programu au kampeni za uelimishaji kuhusu maadili, nidhamu na malezi bora zilizotekelezwa | Kuongezeka kwa uelewa kuhusu maadili, nidhamu na malezi |
| | | Idadi ya miongozo ya kitaifa ya malezi iliyotolewa. | Kukuza uelewa kwa wazazi na walezi namna bora kufanya malezi |
| | | Idadi ya mikutano yenye ajenda ya maadili iliyofanyika | Kujenga uelewa wa pamoja kwa jamii |
| | | Idadi ya programu/kampeni za kujenga uelewa kwa Umma zitakazoanzishwa | Kukuza na kuimarika kwa uelewa katika jamii kuhusu maadili |
| | | Asilimia ya wazazi/walezi wanaoshiriki programu za elimu ya malezi bora. | Kuongezeka kwa ushiriki wa wazazi/ walezi katika programu za malezi bora |
| 2. | Kuhuisha na kuimarisha mifumo ya elimu katika ufundishaji wa elimu ya maadili, uraia na uzalendo | Idadi ya mitaala iliyofanyiwa mapitio. | Kuimarika kwa ufundishaji na ujifunzaji wa elimu ya maadili nchini |
| | | Asilimia ya walimu na wasimamizi wa elimu waliopata mafunzo ya ufundishaji wa maadili | Kupatikana kwa walimu wenye ujuzi na maarifa kuhusu elimu ya maadili |
| | | Idadi ya mafunzo ya kuwajengea uwezo walimu na wasimamizi wa elimu yaliyotolewa | Kuongezeka kwa uelewa wa walimu na wasimamizi wa elimu katika ufundishaji na usimamizi wa maadili |

| | | | |
|---|---|---|---|
| | | Kuwepo kwa mifumo ya nidhamu<br><br>shuleni iliyoimarishwa | Kupungua kwa vitendo vya mmomonyoko wa maadili miongoni mwa wanafunzi<br><br>Kuimarika kwa usimamizi wa maadili shuleni |
| | | Idadi ya mabalozi wa maadili walioteuliwa. | Kuongezeka kwa hamasa ya ufundishaji wa elimu ya maadili katika jamiii |
| | | Idadi ya mafunzo yaliyotolewa | Kuongezeka kwa uelewa wa jamii |
| | | Idadi ya klabu za maadili na uzalendo zilizoanzishwa. | Kuongezeka kwa hamasa ya ufundishaji wa elimu ya maadili na uzalendo katika jamiii |
| 3. | Kusimamia maadili ya kazi, uadilifu, uwajibikaji na uzingatiaji wa sheria, kanuni na miongozo ya utumishi wa umma na sekta binafsi. | Idadi ya mafunzo ya maadili ya kazi yaliyotolewa | Kuongezeka kwa uelewa na uzingatiaji wa maadili ya utumishi wa umma |
| | | Idadi ya matoleo ya Kanuni za maadili zilizotolewa | Kuimarika kwa usimamizi na uzingatiaji wa maadili katika utumishi wa umma |
| | | Idadi ya mifumo ya uwajibikaji na utoaji taarifa iliyoimarishwa | Kuimarika kwa uwajibikaji na utoaji wa taarifa kwa umma |
| | | Asilimia ya kupungua kwa makosa ya rushwa | Kuongezeka kwa imani ya jamii kwa Serikali iliyoko madarakani |
| 4. | Kusimamia maudhui katika vyombo vya habari na mitandao ya kijamii ili kuhakikisha yanazingatia maadili ya Mtanzania | Idadi ya kampeni/ mafunzo ya elimu kwa umma kuhusu matumizi salama ya vyombo habari na mitandao ya kijamii iliyotolewa | Kuongezeka kwa uelewa na ujuzi kuhusu matumizi salama ya vyombo vya Habari na mitandao ya kijamii |
| | | Asilimia ya wananchi waliopewa elimu | Kupungua kwa mmonyoko wa maadili na kuongezeka kwa uzingatiaji wa maadili ya Mtanzania |
| | | Idadi ya Sheria, Kanuni na Miongozo ya maudhui iliyoboreshwa | Kuimarika kwa maadili katika jamii |
| | | Idadi ya watoa huduma za mawasiliano na majukwaa ya kidijiti | Kuimarika kwa uzingatiaji wa maadili |

| | | | |
|---|---|---|---|
| | | Idadi ya Sheria na mifumo rekebu iliyofanyiwa mapitio | Kupungua kwa vitendo vya mmomonyoko wa maadili |
| | | Idadi ya mafunzo yaliyotolewa kwa waandishi wa habari | Kuongezeka kwa maudhui yanayozingatia maadili ya Mtanzania |
| | | Idadi ya waandishi wa habari waliopatiwa mafundo na mazingativu ya maadili | Kuimarika kwa maadili ya waandishi wa Habari |
| | | Idadi ya programu za hamasa kuhusu maudhui chanya yanayolenga maadili | Kupungua kwa vitendo vya mmomnyoko wa maadili |
| 5. | Kulinda na kuendeleza mila na desturi zinazofaa za Kitanzania zinazojenga maadili | Idadi ya tafiti za mila na desturi zilizofanyika | Kubainishwa kwa mila na desturi zinazofaa kuendelezwa |
| | | Idadi ya tafiti za mila na desturi zilizoandikwa, kuchapishwa na kuhifadhiwa. | Kuendeleza mila na desturi zinazoimarisha maadili ya Mtanzania |
| | | Idadi ya programu za elimu zilizoandaliwa | Kuimarisha uzingatiaji wa maadili katika jamii |
| | | Idadi ya kampeni za kupinga mila na desturi zilizopitwa na wakati | Kudumishwa kwa mila na desturi zinazofaa katika jamii |
| | | Idadi ya viongozi wa kimila walioshirikishwa | Kuongezeka kwa uwajibikaji katika kurithisha maadili |
| 6. | Kuimarisha ushirikiano kati ya Serikali, taasisi za dini na asasi za kiraia katika malezi na makuzi | Idadi ya mafunzo yaliyotolewa | Kuongezeka kwa uelewa miongoni mwa jamii |
| | | Asilimia ya vijana waliofikiwa | Kupungua kwa vitendo vya mmomomyoko wa maadili hususani kwa vijana |
| | | Idadi ya vituo vya vijana vilivyoboreshwa | Kuongezeka kwa elimu ya maadili katika makuzi na malezi |
| | | Kuwepo kwa mifumo ya ushauri nasaha na misaada ya kijamii | Kuimarika kwa utoaji wa ushauri nasaha na nasihi pamoja na misaada ya kijamii |

| | | | |
|---|---|---|---|
| 7. | Kuimarisha ushirikiano kati ya Serikali, taasisi za dini na asasi za kiraia katika malezi na makuzi | Kuimarishwa kwa mifumo ya ushirikiano | Kuimarika kwa uwezeshaji wa vijana katika kutambua, kuthamini na kuendeleza maadili |
| | | Ushiriki wa viongozi wa dini na asasi za kiraia katika kampeni za maadili | Kuongezeka kwa uwajibikaji na hamasa katika kueendeleza maadili na utamaduni wa Mtanzania |
| 8. | Kuimarisha nidhamu, uadilifu na maadili kwa wasimamizi wa elimu, walimu, na wanafunzi | Idadi ya semina zilizotolewa | Kuimarika kwa uelewa wa maadili, uadilifu na nidhamu kwa wanafunzi, walimu na wasimamizi wa elimu |
| | | Idadi ya mafunzo yaliyotolewa | Kuimarika kwa uelewa wa maadili, uadilifu na nidhamu kwa wanafunzi, walimu na wasimamizi wa elimu |
| | | Idadi ya vyeti vya utambuzi vitakavyotolewa | Kuongezeka kwa jitihada za kuimarisha maadili, uadilifu na nidhamu kwa wadau wa elimu |
| | | Idadi ya tuzo zitakazotolewa | Kuongezeka kwa jitihada za kuimarisha maadili, uadilifu na nidhamu kwa wadau wa elimu |
| | | Asilimia ya walimu na wasimamizi wa elimu waliopatiwa mafunzo | Kuongezeka kwa ujuzi na weledi wa walimu na wasimamizi wa elimu |

| | | | |
|---|---|---|---|
| 9. | Kuanzisha programu za kuwawezesha vijana kutambua , kuthamini na kuendeleza maadili na utamaduni wa Mtanzania. | Idadi ya shule zilizofikiwa | Kuongezeka kwa uelewa na idadi ya vijana kuhusu umuhimu wa kuthamini na kulinda utamaduni wa Mtanzania |
| | | Idadi ya mitandao ya kijamii iliyosambaza maudhui ya maadili na utamaduni wa Mtanzania | Kupungua kwa maudhui ya kidijiti yanayoharibu maadili na Utamaduni wa Mtanzania |
| | | Asilimia ya vijana walioshiriki katika matamasha | Kuongezeka kwa uelewa na ushiriki wa vijana katika kutambua, kuthamini na kuendeleza maadili |
| | | Idadi matamasha ya utamaduni yaliyofanyika | Kuongezeka kwa uelewa miongoni mwa vijana kutambua, kuthamini na kuendeleza maadili |
| | | Asilimia ya vijana walioshiriki katika maonyesho | Kuongezeka kwa uelewa, ujuzi na maarifa miongoni mwa vijana wa kutambua, kuthamini na kuendeleza maadili |

# SURA YA NANE
# MAPENDEKEZO YA KISERA YA KISEKTA KATIKA KUKABILIANA NA MMOMONYOKO WA MAADILI

## 8 UTANGULIZI

Mmomonyoko wa maadili ni changamoto mtambuka inayojitokeza katika sekta mbalimbali za kijamii, kiuchumi, kisiasa, na kiutawala, na athari zake hudhoofisha utawala bora, mshikamano wa jamii, na maendeleo endelevu. Tafiti na nyaraka za sera zinaonesha kuwa mikakati ya kukabiliana na mmomonyoko wa maadili huwa na matokeo chanya pale inapochukua mkabala wa kisekta, unaojumuisha hatua za kinga, udhibiti, na urekebishaji wa mifumo (URT, 2014; OECD, 2020). Sura hii inaweka mapendekezo ya kisera kwa sekta mbalimbali muhimu, kwa lengo la kuimarisha maadili, uadilifu, na uwajibikaji, sambamba na kuzuia na kudhibiti vitendo vinavyoashiria mmomonyoko wa maadili katika jamii.

## 8.1 SEKTA YA ELIMU

Sekta ya elimu inatambulika kama chombo kikuu cha kurekebisha tabia na si tu kituo cha kutoa maarifa ya darasani. Hivyo, Sera za elimu zinapaswa kuimarisha ujumuishaji wa maadili, uzalendo, na uwajibikaji katika mitaala yote kuanzia elimu ya awali hadi elimu ya juu. Mafunzo ya maadili yawe sehemu ya lazima katika maandalizi ya walimu na tathmini za kitaaluma. Aidha, taasisi za elimu ziboreshe mifumo ya nidhamu, udhibiti wa udanganyifu wa kitaaluma, na ushirikishwaji wa wazazi na jamii katika malezi ya wanafunzi (UNESCO, 2015).

## 8.2 SEKTA YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA

Uongozi unapaswa kuwa kioo cha jamii, hivyo Sera zisisitize uzingatiaji wa kanuni za maadili ya utumishi wa umma, uwazi katika maamuzi, na uwajibikaji wa viongozi. Mifumo ya kutangaza mali na maslahi, pamoja na ulinzi wa watoa taarifa, iimarishwe. Mafunzo endelevu ya maadili na uongozi

wa kimaadili yawe ya lazima kwa watumishi wote, yakifungamanishwa na tathmini za utendaji (URT, 2020) wa elimu ya maadili, pamoja na kuchukua hatua za kisheria na kijamii kwa ukiukwaji wa maadili.

## 8.3 SEKTA YA SHERIA NA HAKI JINAI

Sheria itatumika kama mlinzi wa mwisho wa maadili pale ambapo mifumo mingine ya malezi inashindwa. Sera zielekeze kuboresha upatikanaji wa haki kwa wakati, kupunguza mianya ya rushwa, na kuimarisha uadilifu wa vyombo vya sheria. Matumizi ya mifumo ya kidijiti katika usimamizi wa mashauri yaimarishwe ili kuongeza uwazi na ufanisi. Hatua za nidhamu zichukuliwe kwa uthabiti dhidi ya ukiukwaji wa maadili (UNODC, 2018). Aidha, kufanyika kwa mapitio ya Sheria za Makosa ya Maadili ni jambo la lazima ili ziendeane na mazingira ya sasa, ikiwemo kudhibiti unyanyasaji wa kijinsia, matumizi ya dawa za kulevya, na ulinzi wa watoto. Vile vile, Sera ya Haki na Usawa iimarishwe ndani ya mahakama na vyombo vya ulinzi ili kuondoa rushwa, kwani mfumo wa haki unapokosa uadilifu, jamii hukata tamaa na kuanza kupuuza misingi ya kisheria na kimaadili.

## 8.4 SEKTA YA AFYA

Maadili yanajumuisha ustawi wa akili na utu katika utoaji huduma. Sera zisisitize maadili ya kitaaluma katika utoaji wa huduma za afya, ikiwemo heshima kwa wagonjwa, usiri wa taarifa, na uwajibikaji. Ukaguzi wa maadili katika vituo vya afya uimarishwe, pamoja na mifumo salama ya malalamiko. Mafunzo ya maadili ya kitabibu yahusishwe na taratibu za leseni na ithibati ya kitaaluma (WHO, 2017). Aidha, Sera ya Afya ya Akili iimarishwe ili kutoa huduma za ushauri nasaha katika jamii, ikitambua kuwa ukatili mwingi unatokana na msongo wa mawazo.

## 8.5 SEKTA YA HABARI NA MAWASILIANO

Sekta hii ina mchango mkubwa katika kutengeneza fikra na mienendo ya jamii kupitia taarifa zinazosambazwa. Sera za habari na mawasiliano zielekeze kulinda na kukuza maadili ya kitaaluma, ukweli, na uwajibikaji katika uzalishaji na usambazaji wa taarifa. Viwango vya maadili ya uandishi

wa habari viimarishwe ili kudhibiti upotoshaji, taarifa za uongo, lugha ya chuki, na maudhui yanayodhalilisha utu wa binadamu. Mamlaka za udhibiti ziboreshwe ili kusimamia maudhui ya kidijiti kwa uwiano unaolinda maadili ya jamii bila kukiuka uhuru wa kujieleza. Aidha, elimu ya uraia wa kidijiti (media and digital literacy) iendelezwe kwa umma, hasa vijana, ili kujenga uwezo wa kuchuja taarifa na kutumia vyombo vya habari kwa misingi ya maadili na uwajibikaji (UNESCO, 2019).

## 8.6 SEKTA ZA FEDHA, UCHUMI, BIASHARA NA MANUNUZI YA UMMA

Hali ya kiuchumi ina uhusiano wa moja kwa moja na uadilifu wa jamii. Sera zihimize Uwazi wa Kifedha na matumizi ya mifumo ya kidijiti ili kupunguza mianya ya rushwa na utakatishaji fedha. Vilevile, ianzishwe miogozo ya Elimu ya Maadili ya Biashara itakaolazimisha makampuni na sekta binafsi kuwa na kanuni za kimaadili zinazoeleweka kwa wafanyakazi wao, jambo litakalopunguza wizi na ukosefu wa uaminifu katika miamala ya kibiashara. Aidha, Sera zisisitize maadili ya biashara, ushindani wa haki, na uwajibikaji wa kampuni. Kanuni za maadili ziwe sharti kwa taasisi na kampuni zinazoshiriki katika manunuzi ya umma. Matumizi ya mifumo ya kielektroniki katika zabuni na ufuatiliaji wa matumizi ya fedha za umma yaimarishwe ili kupunguza rushwa (World Bank, 2021).

## 8.7 SEKTA YA VIJANA

Vijana ndio kundi kubwa na lenye nguvu zaidi katika taifa, hivyo ni lazima Sera za vijana zielekeze katika kujenga misingi ya maadili, uwajibikaji, na uzalendo kwa kuunganisha malezi ya kimaadili na programu za elimu, ajira, na ujasiriamali. Serikali na wadau waendeleze programu za uongozi wa vijana zinazojenga nidhamu, maamuzi yenye maadili, na uwajibikaji wa kijamii. Mifumo ya ushauri nasaha na malezi chanya iimarishwe ili kukabiliana na changamoto za mmomonyoko wa maadili zinazotokana na ukosefu wa ajira, matumizi ya dawa za kulevya, na matumizi mabaya ya mitandao ya kijamii. Ushirikishwaji wa vijana katika maamuzi ya kijamii na kisera uimarishwe ili kuongeza umiliki wa maadili wanayoishi nayo.

## 8.8 SEKTA YA UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO

Sanaa na michezo ni kioo cha jamii na chombo chenye nguvu katika kubadili mtazamo wa umma, hususan vijana. Sera zisisitize uhifadhi, ukuzaji, na matumizi ya utamaduni, sanaa, na michezo kama nyenzo za kuimarisha maadili ya jamii. Kanuni za maadili ziboreshwe kwa wasanii, wanamichezo, na wadau wa sekta hizi ili kudhibiti mienendo inayokiuka maadili ya jamii, ikiwemo lugha isiyofaa, maudhui yanayodhalilisha utu, na vitendo vya rushwa au upangaji wa matokeo (match-fixing) (UNDP, 2018). Serikali ihamasishe uzalishaji na usambazaji wa kazi za sanaa zinazokuza maadili chanya, mshikamano wa kijamii, na uzalendo. Miundombinu ya michezo na sanaa isimamiwe kwa uwazi na haki ili kuwa mfano wa maadili ya uongozi bora.

## 8.9 SEKTA YA MALIASILI NA UTALII

Sekta ya utalii ni kiungo muhimu kati ya utamaduni wa ndani na mataifa ya nje, hali inayohitaji sera madhubuti kulinda maadili ya taifa dhidi ya athari za utandawazi. Sera za maliasili na utalii zielekeze kuimarisha maadili ya uhifadhi, matumizi endelevu, na uwajibikaji wa kizazi cha sasa na kijacho. Taratibu za utoaji wa leseni, vibali, na mikataba ya uwekezaji ziwe wazi, shirikishi, na zinazoepuka migongano ya maslahi ili kudhibiti rushwa na unyonyaji wa rasilimali. Ushirikishwaji wa jamii zinazozunguka hifadhi na vivutio vya utalii uimarishwe kupitia mifumo ya kunufaika kwa haki, ili kujenga umiliki wa maadili ya uhifadhi. Mafunzo ya maadili ya uhifadhi, utalii endelevu, na heshima kwa tamaduni za wenyeji yawe ya lazima kwa watumishi wa sekta, wawekezaji, na waendeshaji wa shughuli za utalii.

## 8.10 SEKTA YA TEKNOLOJIA YA HABARI NA MAWASILIANO (TEHAMA)

Katika karne ya 21, teknolojia imekuwa kichocheo kikubwa cha mabadiliko ya tabia, hivyo kuhitaji udhibiti madhubuti wa maudhui ya kidijiti. Sera zielekeze maadili ya kidijiti, ulinzi wa faragha, na usalama mtandaoni. Miongozo ya matumizi bora ya teknolojia itungwe na kutekelezwa, ikijumuisha elimu ya maadili ya kidijiti kwa taasisi na umma kwa ujumla (OECD, 2019).

## 8.11 SEKTA YA MIUNDOMBINU NA USAFIRISHAJI

Maeneo ya usafiri wa umma na miundombinu ya miji mara nyingi huchochea au kudhibiti mienendo ya kimaadili kulingana na mazingira yalivyo. Sera za miundombinu na usafirishaji zielekeze maadili ya uwajibikaji, usalama, na uadilifu katika upangaji, utekelezaji, na uendeshaji wa miradi. Maadili ya usalama barabarani, reli, majini, na anga yajengewe mifumo ya elimu endelevu kwa watumishi na watumiaji wa huduma. Nidhamu ya kitaaluma isimamiwe kikamilifu kwa wahandisi, makandarasi, na waendeshaji wa vyombo vya usafiri ili kulinda maisha ya wananchi na rasilimali za umma.

## 8.12 SEKTA YA SERIKALI ZA MITAA NA JAMII

Sekta hii ndiyo kiungo mhimili kinachofika hadi ngazi ya familia na mtaa ambapo mmomonyoko wa maadili huanzia. Sera zisisitize uadilifu katika utoaji wa huduma za msingi na usimamizi wa rasilimali katika ngazi za chini. Ushirikishwaji wa wananchi katika maamuzi ya maendeleo uimarishwe, pamoja na uanzishwaji wa kamati za maadili katika jamii (URT, 2018).

## 8.13 SEKTA YA ARDHI NA MAZINGIRA

Maadili katika sekta ya ardhi yanajikita kwenye uaminifu, haki, na utunzaji wa urithi wa taifa kwa vizazi vijavyo. Sera za ardhi na mazingira zisisitize maadili ya haki, uwazi, na usawa katika umiliki, upangaji, na matumizi ya ardhi. Mifumo ya kidijiti ya usimamizi wa ardhi iimarishwe ili kupunguza rushwa, migogoro ya ardhi, na upendeleo katika utoaji wa hati na vibali. Utekelezaji wa sheria za mazingira uendane na misingi ya uadilifu, uwajibikaji, na ushirikishwaji wa wananchi, hususan katika tathmini za athari za mazingira (EIA). Elimu ya maadili ya uhifadhi wa mazingira iimarishwe kwa jamii, sekta binafsi, na serikali za mitaa ili kukuza matumizi endelevu ya ardhi na kulinda rasilimali kwa manufaa ya muda mrefu.

## 8.14 SEKTA YA DINI NA ASASI ZA KIRAIA


Taasisi za dini na asasi za kiraia ni walinzi wa msingi wa dhamiri ya taifa na dira ya maadili. Sera zitambue na kuimarisha mchango wa taasisi za dini na asasi za kiraia katika kujenga na kulinda maadili ya jamii. Ushirikiano wa kimkakati uanzishwe kati ya serikali, taasisi za dini, na asasi za kiraia katika kampeni za maadili, malezi ya familia, na uhamasishaji wa uwajibikaji wa kijamii. Mifumo ya uwajibikaji wa kifedha na kiutawala iimarishwe ndani ya taasisi hizi ili kuimarisha uaminifu wa umma. Aidha, sera zielekeze matumizi ya mafundisho ya dini na shughuli za kiraia katika kukuza amani, heshima, haki, na mshikamano wa kitaifa bila ubaguzi.

## 8.15 HITIMISHO

Kwa ujumla, mapendekezo ya kisera ya kisekta yaliyobainishwa katika sura hii yanakusudia kuimarisha mfumo wa kitaifa wa maadili kwa kutumia mkabala shirikishi, unaopimika, na endelevu. Utekelezaji wake unapaswa kuungwa mkono na uratibu wa taasisi, viashiria vya ufuatiliaji na tathmini, na dhamira ya kisiasa na kijamii katika ngazi zote.

# MAREJELEO


1. Biblia Takatifu
2. Dira ya Taifa ya Maendeleo 2050
3. Kanuni za Maadili ya Utendaji katika Utumishi wa Umma (2023)
4. Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania (1977)
5. Kuran Tukufu Surat Al-A'raf 7:80-81
6. Mwongozo wa Maadili na Utamaduni wa Mtanzania Toleo la 1 2022
7. Mkakati wa Tano wa Taifa wa Kudhibiti VVU na Ukimwi Tanzania 2021/22-2025/26
8. Mkakati wa Taifa wa Usimamizi Taka 2025-2030
9. Mkakati wa Taifa wa Matumizi ya Nishati Safi ya Kupikia (2024-2034)
10. Sera ya Elimu na Mafunzo ya Mwaka 2014 Toleo la Mwaka 2023
11. Sera ya Habari na Utangazaji ya Mwaka 2003
12. Sera ya Taifa ya Jinsia na Maendeleo ya Wanawake ya Mwaka 2023
13. Sera ya Maendeleo ya Mtoto ya Mwaka 1993
14. Sera ya Taifa ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya ya Mwaka 2024
15. Sera ya Taifa ya Maendeleo ya Vijana ya Mwaka 2007
16. Sera ya Taifa ya Wazee ya Mwaka 2003 Toleo la 2024
17. Sera ya Utamaduni ya Mwaka 1997
18. Sheria ya Filamu na Michezo ya Kuigiza, Sura ya 230
19. Sheria ya Huduma za Habari, Sura ya 229
20. Sheria ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa, Sura ya 329
21. Sheria ya Maadili ya Viongozi wa Umma, Sura ya 398
22. Sheria ya Makosa ya Mtandao, Sura ya 443
23. Sheria ya Mtoto, Sura ya 13
24. Sheria ya Ndoa, Sura ya 29
25. Utamaduni chombo cha maendeleo, 1979



*“Nchi inaweza kuwa na rasilimali nyingi, lakini bila maadili , haitakuwa na uwezo wa kuendelea”*

**Mwalimu Julius Kambarage Nyerere**
**RAIS WA KWANZA WA JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA.**

# UJUMBE WA

# WIZARA WADAU

# WIZARA YA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WANAWAKE NA MAKUNDI MAALUM



Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum inalo jukumu la kuhamasisha jamii kukabiliana na mmomonyoko wa maadili kwakuwa na malezi chanya kwa watoto na familia ili kuwa na jamii yenye maadili, uzalendo na moyo wa kujitolea kushiriki shughuli mbalimbali za maendeleo pamoja na kuwa na jamii yenye maendeleo endelevu na jumuishi. Katika kukabiliana na mmomonyoko wa maadili Wizara imeandaa miongozo na vitini vya mafunzo mbalimbali ikiwemo; Kitini cha kufundishia watoto na wazazi/walezi kuhusu Usalama wa Mtoto Mtandaoni (2022), wenye lengo la kudhibiti maudhui wanayotazama watoto kwenye mitandao ya kijamii na televisheni ili kuepuka ushawishi mbaya wa tamaduni za kigeni; Mwongozo wa Taifa wa Dawati la Ulinzi na Usalama wa Mtoto Ndani na Nje ya Shule (2022), Mwongozo wa Taifa wa Uundaji na Uendeshaji wa Mabaraza ya Watoto (2022), Mwongozo wa Taifa wa Kuendesha Majadiliano ya Mila na Desturi zenye Madhara katika Jamii (2022) pamoja na Mpango wa Taifa wa Kutokomeza Ukatili Dhidi ya Wanawake na Watoto - MTAKUWWA II (2024/2025-2028/2029). Kupitia wataalam wa Maendeleo ya Jamii waliopo ngazi ya Sekretarieti za Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa wataendelea kuhamasisha na kuelimisha jamii kuwa na mtazamo chanya, kubadili fikra zitakazochangia kuwepo kwa na maadili mema, moyo wa uzalendo na kuondokana na Imani potofu, mila, desturi na tamaduni zenye madhara kwa Maendeleo ya Jamii.

**Mhe. Dkt. Dorothy Gwajima**
**WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WANAWAKE NA MAKUNDI MAALUM**

**WIZARA YA HABARI, UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO**
**S.L.P 25**
**MJI WA SERIKALI MTUMBA**
**DODOMA**